




U N
D P

*Empowered lives.
Resilient nations*



MAZUNGUMZO YA JAMII KWA AMANI ENDELEU

KITABU CHA MWONGOZO WA KUANDAA USHIRIKI WA
RAIA KATIKA MAZUNGUMZO ENDELEU JUU YA KUZUIA
MIGOGORO, KUJENGA MSHIKAMANO NA USHIRIKIANO



*Empowered lives.
Resilient nations*



MAZUNGUMZO YA JAMII KWA AMANI ENDELEVU



KITABU CHA MWONGOZO WA KUANDAA USHIRIKI WA
RAIA KATIKA MAZUNGUMZO ENDELEVU JUU YA KUZUIA
MIGOGORO, KUJENGA MSHIKAMANO NA USHIRIKIANO

©2016

Tangu mwaka 1995 na kuendelea, historia ya uchaguzi wa vyama vingi nchini Tanzania imekuwa na matukio ya migogoro inayotokana na uchaguzi. Katika muktadha huu, wadau kadhaa wamekuwa wakishiriki katika mazungumzo ya kuleta amani, hasa kabla ya uchaguzi. Wakati ambapo mazungumzo haya yamechangia katika kuzuia migogoro, imebainika kwamba kwa kiasi kikubwa mazungumzo hayo huwa ya muda tu badala ya kuwa endelevu.

Kama mazungumzo hayo yangekuwa ya kudumu basi yangeleta athari njema. Zaidi ya hayo, mazungumzo katika ngazi ya jamii yamekuwa muhimu kwa namna ya pekee katika kushughulikia mivutano mingine katika eneo linalohusika kutokana na masuala ya kijamii na kiuchumi. Ili kuchangia katika mazungumzo endelevu juu ya amani, Mradi wa Uwezeshaji

Demokrasia wa UNDP kwa kushirikiana na waandaaji wa mazungumzo wa Tanzania waliandaa mwongozo huu kuhusu *“Mazungumzo ya Jamii kwa ajili ya Amani Endelevu Nchini Tanzania”*.

Mafunzo kuhusu mazungumzo ya amani endelevu yalifanywa kwa ajili ya wakufunzi wa waandaaji mazungumzo waliotoka katika asasi na mitandao mbalimbali ya kiraia kabla ya uchaguzi wa Oktoba, 2015. Mradi pia ulianza kuandaa kitabu cha mwongozo. Kitabu hiki kinakusudia kuimarisha utamaduni wa Tanzania wa mazungumzo katika kuzuia migogoro na kujenga amani hasa katika ngazi ya jamii kama chanzo cha kuunga mkono waandaaji mazungumzo ili kupunguza na kumudu mivutano katika ngazi ya jamii.

Kitabu hiki cha mwongozo ni matunda ya jitihada za ushirikiano wa watu na taasisi mbalimbali waliotoa muda, nguvu, ujuzi na maarifa yao ili kuhakikisha kuwa kinakamilika. Kwanza kabisa, shukurani zetu zinakwenda kwa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) ambalo liligharamia mwongozo huu wa Mazungumzo ya Jamii kwa ajili ya Amani Endelevu. Pia shukurani za pekee zimwendee Bi. Nirina Kiplagat ambaye hakuchoka kuunga mkono mchakato mzima wa kuandaa mwongozo huu.

Shukurani za pekee kwa wanachama wa taasisi zifuatazo: Chama cha Asasi Zisizo za Kiserikali Zanzibar (ANGOZA), Kituo cha Demokrasia cha Tanzania (TCD), Femina Hip, Taasisi ya Mwalimu Julius Nyerere, Karibu Tanzania, Baraza la Imani Mchanganyiko la Amani Tanzania (IRCPT) na Ofisi ya Mufti wa Zanzibar (OMZ), ambao walishiriki katika kongamano la awali kuhusu Mazungumzo kama chombo cha kuleta mabadiliko ya migogoro na kujenga amani na asasi hizo zilizoshiriki katika kongamano ili kuthibitisha yaliyomo kwenye mwongozo

huu, asasi hizo ni, Kituo cha Ushirikiano wa Nje, Kituo cha Huduma za Kisheria cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Zanzibar, ANGOZA, Kituo cha Ushirikiano wa Imani Mbalimbali, TCD, Femina Hip, Karibu Tanzania, Taasisi ya Mwalimu Julius Nyerere, IRCPT, OMZ, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (ORPP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UNWOMEN), na UNESCO. Washiriki katika makongamano yote mawili walitoa mchango mkubwa ambao umesaidia kujenga yaliyomo kwenye mwongozo huu. Tunawashukuru vilevile Bi. Sandra Bwire kwa kufanya kazi ya kupitia rasimu kadhaa za mwongozo huu kwa bidii chini ya ushauri wa kiufundi na usimamizi wa Bi. Léonie Abela.

Shukurani kubwa tunazipeleka kwa Wakala wa Ushirikiano na Utafiti wa Maendeleo kwa kuandaa mazingira wezeshi na msaada uliotolewa katika kutekeleza jukumu hili. Kabla ya kufika mwisho, shukurani za pekee zimfikie Bw. Luc Ansohi aliyehariri, na Bi. Léonie Abela aliyefanya uhakiki wa yaliyomo kwenye mwongozo huu.

Malengo na Matumizi ya Kitabu hiki cha Mwongozo

Lengo kuu la kitabu hiki cha mwongozo ni kuimarisha utamaduni wa Watanzania wa mazungumzo katika kuzuia migogoro na kujenga amani, hasa hasa katika ngazi ya jamii. Kwa ajili hii, mwongozo huu unapendekeza hatua muhimu zinazoweka muundo wa mazungumzo kuwa mchakato endelevu unaowaleta wadau pamoja, ili kubaini, kuchambua na kuelewa masuala muhimu yanayoathiri au yenye uwezekano wa kuvuruga mshikamano wa kijamii na hali ya kuishi pamoja kwa amani miongoni mwa wanajamii.

Jambo la kuelewa masuala yanayoathiri jamii kuishi pamoja kwa amani linaleta wazo la hatua ya pili ya kutafuta njia za muda mfupi na mrefu za kushughulikia masuala yaliyoainishwa yenye kuleta mashaka na kupata ufumbuzi uliopendekezwa katika mkataba wa kijamii uliopitishwa na kushuhudiwa na viongozi.

Kitabu hiki kimetumia mambo mengi kutoka katika mwongozo wa “*Ufufuaji Amani na Mapatano ya Jamii*” ulioandaliwa katika muktadha wa Kenya. Mwongozo unatoa zana nzuri kwa watendaji wote wanaoshughulika na kujenga amani katika ngazi ya jamii na vilevile waamuzi na watunga sera.

Mwongozo wa Mazungumzo ya Jamii kwa ajili ya Amani Endelevu umekusudiwa kwa ajili ya wote wanaopenda kuunga mkono na kuimarisha maisha ya pamoja ya amani na jitihada za maendeleo miongoni mwa jamii ya Watanzania. Zaidi ya hayo, mwongozo unaweza kutumiwa na mtu yeyote, wakala, taasisi za serikali ambazo zinataka kutumia modeli ya CDSP kadiri inavyofaa (katika Afrika na kwingineko).

¹ Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Wakala wa Ushirikiano na Utafiti katika Maendeleo (ACORD) & Kamati ya Taifa ya Uongozi katika Kujenga na Kusimamia Amani, Wizara ya Utawala wa Majimbo na Usalama wa Ndani, Ofisi ya Rais. (2011). *Community Peace Recovery & Reconciliation. A Handbook for Generating Leadership for Sustainable Peace and Recovery among Divided Communities.*

Dibaji.....	ii
Shukurani.....	iii
Malengo na Matumizi ya Kitabu hiki cha Mwongozo.....	4
Mtazamo wa Jumla ya Modeli ya Mazungumzo ya Jamii kwa ajili ya Amani Endelevu (CDSP).....	viii
Mchoro wa Muhtasari wa Modeli ya CDPS.....	ix

UTANGULIZI 1

1. USULI WA MUKTADHA WA TANZANIA 1

1.1. Hali ya Kijamii na Kiutamaduni	I
1.2. Hali ya Kiuchumi.....	I
1.3. Hali ya Kisiasa	I
1.4. Hali ya Kimazingira/Kiikolojia.....	I

2. MIGOGORO YA KIJAMII: UGUMU WAKE NA SABABU 3

2.1. Migogoro Inayotokana na Siasa: Tukio la Vurugu Unguja (Zanzibar) wakati wa vurugu za UAMSHO za 2012	3
2.2. Migogoro Unaotokana na Rasilimali: Vurugu za Gesi Mtwara (2014)	5

3. DHANA YA MAZUNGUMZO NA UMUHIMU WAKE KAMA NJIA NA MCHAKATO WA KUZUIA MACHAFUKO NA KUJENGA AMANI 6

3.1. Matumizi ya Mazungumzo Kama Zana ya Kuzuia Migogoro na Kuleta Mabadiliko.....	6
3.1.1. Kanuni kuu za Mazungumzo.....	6
3.1.2. Aina za Mazungumzo.....	7

4. AWAMU YA MAANDALIZI: MAZUNGUMZO YA JAMII NA AMANI ENDELEVU (CDSP)..... 9

HATUA YA 1: TATHAMINI YA JAMII NA UTAMBUZI WA MAKUNDI YANAYOLENGWA	9
HATUA YA 2: KUBAINI WASHIRIKA.....	9
HATUA YA 3: KUWASHIRIKISHA WADAU MBALIMBALI NA KUJENGA UWEZO WAWATENDAJI WA UTEKELEZAJI.....	10
Kuimarisha Uwezo wa Washirika Waliobainishwa	10
a. Mafunzo ya Washirika Waliobainishwa	10
b. Vifaa na Msaada wa Kifedha kwa ajili ya Jitihada za Kuleta Amani	11
c. Kupata Washirika na Wadau Wengine	11
HATUA YA 4: MIKUTANO YA UTAMBULISHO NA WADAU MUHIMU	12
a. Kuwaendea Wanajamii	12
b. Kuchagua Eneo na Tarehe ya Kipindi cha Mazungumzo	12
c. Kuchagua na Kujenga Uwezo wa Vinara wa Amani.....	13

5. AWAMU YA 1: KUPATA MKATABA WA KIJAMII WA WANANCHI	14
HATUA YA 5: UZINDUZI WA MAZUNGUMZO YA JAMII KWA AJILI YA AMANI ENDELEVU	14
HATUA YA 6: MAZUNGUMZO YA JAMII AU VIPINDI VYA MAZUNGUMZO	14
6.1. Kusimamia Hisia/Maoni	15
6.2. Kushughulika na Ukanushaji	16
6.3. Kushughulika na Tabia Zitokanazo na Haiba.....	16
6.4. Uchambuzi wa Tatizo	17
6.5. Hatua za Mgogoro.....	18
6.6. Zana za Kuchambualia Mgogoro	18
6.7. Kutengeneza Dira ya Jamii na Mapatano ya Amani.....	28
HATUA YA 7: MIKATABA YA KIJAMII NA YALIYOMO	29
7.1 Ufafanuzi wa Mikataba ya Kijamii na yaliyo Ndani yake.....	29
7.2 Kutiwa saina kwa mkataba ya kijamii kwa ajili ya kuishi pamoja kwa amani.....	30
7.3 Ahadi ya Kila Raia.....	30
7.4 Kuunda Kamati za Amani za Jamii	30
7.5 Mamlaka ya Kamati ya Amani.....	31
7.6 Mbinu za Jamii za Ufuatiliaji wa Mikataba ya Kijamii.....	31
6 AWAMU YA 2: UENDELEVU KUPITIA MIRADI YA AMANI	32
HATUA YA 8: MIRADI YA AMANI ENDELEVU.....	32
KIAMBATANISHO CHA 1: Kamati ya Uongozi ya Taifa juu ya Kujenga Amani na Kudhibiti Migogoro (NSC)	34
KIAMBATANISHO CHA 2: Hadidu za Rejea kwa Kamati za Amani za Wilaya (DPCs)	37
KIAMBATANISHO CHA 3: Mifano ya Mikataba ya Kijamii	39
Mfano wa 1: Mkataba wa Kuishi Pamoja kwa Amani (Mtaa wa Teza II, Kamenge), Burundi.....	39
Mfano wa 2: Mkataba wa Kijamii kati ya Jamii za Wakisii na Wakipsigis Wanaoishi katika mpaka wa Wilaya za Sotiki na Borabu, Kenya.....	40
KIAMBATISHO CHA 4: Zana ya Uchambuzi wa Mamlaka.....	43
KIAMBATISHOCHA 5: Uchambuzi wa Jinsia	47
Vipengele vya Hali ya Mgogoro na Wigo Unaowezekana wa Jinsia.....	47
Vipengele vya Uhusiano wa jinsia na wigo wa migogoro Zinazoweza kuwepo	48
Orodha ya Uchambuzi wa Jinsia	49
Jedwali la Uchambuzi wa Jinsia	50
MAREJEO	51

Ufafanuzi wa Vifupisho vya Majina na Taasisi zilizopo katika Mwongozo

ACORD	Wakala wa Ushirikiano na Utafiti wa Maendeleo
ANGOZA	Chama cha Asasi Zisizo za Kiserikali Zanzibar
CDSP Model	Modeli ya Mazungumzo ya Jamii kwa ajili ya Amani Endelevu
CPRR Model	Ufufuaji Amani na Maelewano ya Jamii
CSPM	Mpango wa Kudhibiti Madhara ya Migogoro
CYD	Kituo cha Vijana cha Mazungumzo
ILPI	Taasisi ya Kimataifa ya Sheria na Sera
INGO	Shirika la Kimataifa lisilo la Serikali
NGO	Shirika lisilo la Serikali
UNDP	Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
OMZ	Ofisi ya Mufti wa Zanzibar

Mtazamo wa Jumla ya Modeli ya Mazungumzo ya Jamii kwa ajili ya Amani Endelevu (CDSP)

Modeli ya CDSP ni mchakato wa mazungumzo yanayosukumwa na jamii kwa lengo la kuwaleta wanajamii waliobainishwa kuwa wako kwenye mgogoro mzito unaotishia kukua na kusababisha vurugu kubwa endapo hautapewa kipaumbele na kushughulikiwa kwa namna inayostahili. Mchakato huu huhusisha uelewa kamili wa muktadha unaobeba uchambuzi wa kina wa masuala mbalimbali, sura, upana, ngazi, vyanzo vya migogoro katika jamii, ambayo inatambuliwa ama kwa uhalisi wake au kwa kudhaniwa.

Modeli ya CDSP imeiga mambo mengi kutoka kwenye Ufufuaji Amani na Maelewano ya Jamii (CPRR) ambayo ni modeli ya mazungumzo yanayochochewa na jamii kwa lengo la kusaidia jamii kuchambua na kuelewa mizizi ya vyanzo vya mgogoro; kutambua ukiukwaji haki na jinai zilizofanywa na wanajamii dhidi ya wenzao; kuwezesha uponyaji, kuanzisha mapatano ili kupata ahadi rasmi kwa ajili ya maisha ya pamoja ya amani ya kudumu; na kufanyia kazi ufufuaji wa jamii.

Tofauti pekee kati ya modeli hizi mbili ni kwamba CDSP inashughulikia zaidi kuzuia wakati ambapo CPRR imejikita katika kutafuta suluhisho, ikibeba mitazamo ya kuzuia migogoro ya baadaye. CDSP inalenga kuzuia kutokea kwa migogoro wakati ambapo CPRR inawezesha ufufuaji na maelewano baada ya machafuko ya kikatili na kuchukua hatua zitakazozuia migogoro mingine ya baadaye. Ni muhimu kuzingatia kwamba ingawa modeli ya CDSP inalenga katika mbinu za kuzuia migogoro, kuna masuala ambayo yanaendana na CPRR ambayo ni hatua muhimu katika uchambuzi wa migogoro na kuelewa kwa kutumia zana mbalimbali za uchambuzi.

CPRR inahusu msingi wa kutafsiri viwango vya hatua za kuchukua zinazohitajika katika muktadha fulani. Kwa hiyo, vipengele muhimu vya modeli ya CDSP vinaelezwa kwa ufupi hapa chini:

❖ Uchambuzi wa Muktadha:

Jambo la kwanza la lazima ni kufanya tathmini ya jamii kwa kutumia zana yoyote ya kutambua na kuchambua eneo la mgogoro. Hatua hii husaidia kubaini vichochezi vya mgogoro, vijenga amani, wadau na nguvu za pamoja ambavyo vyote ni muhimu katika kujenga picha na ambavyo vinaweza kusaidia kubaini namna ya kuanzisha mjadala wa jamii na kuleta amani endelevu. Pasipo tathmini hii, mazungumzo ya jamii na hatua za kujenga amani hujiielekeza katika matatizo ya sasa, ambayo mara nyingi ni dalili za nje za matatizo ya ndani zaidi ambayo hayakushughulikiwa kwa muda mrefu na yana uwezekano wa kukua na hatimaye kuwa migogoro yenye ukatili mkubwa.

❖ Mazungumzo ya Jamii

Jamii zinaongozwa kushirikishana uzoefu wa mivutano iliyopo ambayo inaweza kusababisha migogoro na/au mapambano ya wazi na namna wanavyoweza kuiathiri au wanavyoathirika nayo. Hii husaidia katika kuandaa utoaji taarifa ya kijamii ya pamoja kuhusu sababu na asili ya vyanzo vya uwezekano wa kutokea migogoro na ile ambayo pengine imekwishatokea. Mchakato huu husababisha wanajamii kusikia maoni ya wengine miongoni mwao pamoja na kueleza mikakati bora ya kuzuia uwezekano wa mgogoro au kushughulikia masuala muhimu yaliyokwisha kubaliwa.

❖ Kutambua Haki na Masuala ya Kihistoria

Kipengele muhimu cha mazungumzo ya jamii ni kuanzishwa kwa mazingira salama ambapo wanajamii wanajisiikia huru kiasi cha kutosha kutambua na kuwajibika kwa vitendo vilivyotokea kabla vya ukiukwaji haki, na historia ambazo zinaweza kuwaumiza wanajamii. Katika nyakati

ambapo jamii zilikabiliwa na migogoro ya wazi, jamii inasaidiwa kutambua kwa pamoja maumivu, majeraha na mateso ambayo mtu mmoja mmoja na vikundi huenda walipitia kwa sababu ya migogoro, na hivyo kuandaa makubaliano ya kufanya kazi pamoja ili kuzuia kutokea tena kwa migogoro hiyo siku zijazo. Hiki ni kipengele muhimu cha mchakato unaowezesha wanajamii kutambua maumivu ambayo huenda waliyasababisha au kuyapata na kuendelea na kujishughulisha na kutafuta amani na kuishi pamoja katika jamii.

❖ **Mapatano ya Jamii Kuhusu Kujenga Hatma ya Pamoja**

Kwa kawaida wanajamii hujiona kuwa wanatoa kupita kiasi pale wanapopokea wajibu kuhusu uhusiano wa amani wakati masuala ya kimuundo yanabaki bila kutatuliwa. Kwa hiyo, njia pekee, ni kuwasaidia wanajamii kujihusisha na mchakato wa kutafuta dira. Kufanya hivi huwasaidia wanajamii kuunda dira ya siku zijazo na aina ya jamii ambamo wangependa kuishi. Kisha wanasaidiwa kufanya kazi kwa kurudi nyuma kutokana na dira hii ya siku zijazo, hadi kuufikia wakati uliopo. Lengo la zoezi la namna hiyo linapaswa kuwa kuwasaidia kukubaliana kuhusu dira ya pamoja.

Dira ya pamoja inawahakikishia kwamba masuala yao ya sasa huenda hayajatatuliwa au utatuzi si kamilifu, hatma inabeba ndani yake uwezekano wa mabadiliko ya kweli ya kijamii. Kisha inawezekana kufanya nao kazi ili kuandaa majukumu na wajibu wa kuhakikisha dira hiyo ya pamoja inakuwa kweli.

Mkataba wa Kijamii kwa Ajili ya Amani Ili kuweka ahadi ya dhati ya kuishi pamoja, jamii zinasaidiwa kukubaliana juu ya “*mikataba ya kijamii*”. Hii huwa ni mikataba inayofungwa kimaadili ambayo pande zote katika mazungumzo huchangia katika utamaduni wa amani na kujizuia kujiingiza katika tabia zisizofaa zilizobainishwa wakati wa majadiliano ya jamii. Mikataba hii ya kijamii inatiwa saini na wawakilishi kutoka katika makundi mbalimbali yanayoshiriki katika mazungumzo ya jamii na kushuhudiwa na viongozi.

❖ **Miradi ya Amani/Ufufuaji Iliyobuniwa na Kutekelezwa Pamoja**

Miradi ya amani/ufufuaji ibuniwe pamoja na pande zote zinazohusika katika mazungumzo ya jamii. Vipaumbele vinabainishwa na kutolewa kwa lengo la kuimarisha amani, na “*kuimarisha*” mikataba yao ya kijamii waliyokubaliana. Miradi hii hutumika kushughulikia vyanzo vya mivutano vinavyoonekana kuwepo katika jamii (*kwa kiasi ambacho hii inaingia ndani ya wigo wa ushawishi wa jamii na viongozi wa jamii*) na dalili zinazotokana nayo.

Pale ambapo shughuli za kiuchumi zinabainishwa kama miradi inayofaa ya amani na jamii, uamuzi juu ya vipaumbele hauna budi kutokana na matokeo ya uchambuzi wa orodha ya manufaa uliofanywa ili kubaini shughuli bora za kiuchumi ambazo zitatekelezwa na kundi pana la wanajamii.


Lengo hapa ni kuwavuta watu wengi zaidi, hasa vijana, ambao huenda wameegemea katika ukatili na migogoro kwa sababu ya umaskini, kukosa kazi au kujihushisha kwao na vitendo vya uhalifu.

Miundo ya Kijamii kwa Ajili ya Amani

Mifumo ya jamii inaundwa mara moja katika kila kitongoji ili kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kijamii katika jamii ile, na kuendelea kuwatia moyo watu kuendeleza ahadi zao za dhati katika kuishi pamoja kwa amani. Kwa kawaida mifumo hii iliyo katika muundo wa jamii au kamati za amani za jamii zinaundwa na wanajamii wanaojitolea muda wao kuhakikisha kwamba wanajamii wanatimiza ufumbuzi uliokubaliwa, na walio tayari kupatikana ili kushugulikia ukiukwaji wowote mpya au kutozingatiwa kwa mkataba wa kijamii katika namna isiyofaa.

Mchakato huu umethibitishwa kuweka msingi madhubuti kwa ajili ya amani na ufufuaji endelevu ili kuunda mazingira mwafaka kwa mfumo unaomilikiwa na jamii, wa haki na uwajibikaji, ambao hatimaye unachangia katika taifa kuwa na utulivu kwa ujumla.

Mazungumzo ya Jamii na Modeli ya Amani Endelevu



1. USULI WA MUKTADHA WA TANZANIA

1.1. Hali ya Kijamii na Kiutamaduni

Tanzania inakadiriwa kuwa na zaidi ya watu milioni 45². Imeundwa na watu wa asili mbalimbali ambapo kuna makabila zaidi ya 120. Imani kuu ni Ukristo na Uislamu. Dini hizi zina athari kubwa katika utamaduni na uwanda wa siasa.

Nchi hii ina sifa ya kuendeleza mfumo wa kisiasa na kijamii wa Ujamaa kwa takribani miongo miwili. Sera hiyo iliendeleza stadi za kusoma na kuhesabu, ilipunguza vifo vya watoto wachanga, na kuwaunganisha Watanzania kutoka katika asili za makabila chini ya “*Falsafa ya Ujamaa*”.

Katika miaka ya hivi karibuni, masuala kama ukabila, tofauti za kimaendeleo kati ya mkoa na mkoa, rushwa, kuongezeka kwa tofauti ya walio nacho na wasio nacho na dini, yote yanachochea kuvunjika kwa umoja nchini humo.

1.2. Hali ya Kiuchumi

Katika miaka yake ya mwanzo baada ya uhuru, Tanzania ilijiendesha kwa kutumia sera ya kijamii na kiuchumi ya ujamaa, ambayo ilikuwa na manufaa yake, lakini hatimaye Tanzania ilibaki kuwa moja ya nchi maskini kabisa duniani ikitegemea misaada ya kimataifa.

Tangu wakati huo, uchumi wa nchi umeimarika huku kasi ya ukuaji wake ikiwa wastani wa asilimia 6.7 tangu mwaka 2006, ikiwa ni moja ya kasi bora zaidi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hata hivyo, kiwango cha umaskini bado kiko juu huku takribani asilimia 34 ya Watanzania wakiishi katika umaskini³.

Zaidi ya hayo, ni muhimu kukumbuka kwamba viwango vya juu vya ukosefu wa ajira na ajira chini ya kiwango, hasa miongoni mwa vijana wa Tanzania, na hatari ya migogoro katika nchi za jirani kuenea hadi Tanzania, kwa mfano, mgogoro wa Burundi; kuibuka kwa siasa kali za kiimani, kwa kutaja tu masuala machache, yote ni changamoto kwa uchumi wa nchi.

1.3. Hali ya Kisiasa

Kwa kulinganisha na majirani zake, Tanzania imekuwa na utulivu wa kutosha. Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar umeendelea kudumu kwa zaidi ya miongo mitano ingawa mivutano ya hapa na pale haikukosekana. Zanzibar ina kiasi fulani cha mamlaka huku ikiwa na Baraza lake la Wawakilishi (Bunge) na Rais.

Tanzania inafuata demokrasia ya vyama vingi. Chama kinachotawala ni Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho kiliundwa mwaka 1977 kufuatia kuungana kwa TANU kutoka Tanganyika na Afro Shirazi Party (ASP) kutoka Zanzibar.

Kurudishwa kwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi mwaka 1992 kulisababisha kuibuka kwa mivutano iliyokuwa ya chini kwa chini. Hata hivyo, kumeendelea kufanyika jitihada za kumudu mivutano hii kupitia mifumo ya kijamii na kisheria.

1.4. Hali ya Kimazingira/Kiikolojia

Tanzania ni nchi iliyojaaliwa sana; licha ya utajiri katika kilimo, misitu na wanyama pori, taifa pia lina utajiri wa madini kama dhahabu, almasi, chuma, makaa ya mawe, nikeli, tanzanite, urani na gesi ya asili.

² Idara ya Taifa ya Takwimu ya Tanzania, 2012, <http://50.87.153.5/-eastc/sensa/index.php/home/BookOneDo>

³ Tanzania's country profile <http://www.bbc.com/news/world-africa-14095776>

Uchambuzi wa Mpango wa Kudhibiti Madhara ya Migogoro (Conflict Sensitive Program Management, kwa kifupi CSPM) uliofanyika mwaka 2014 ulionyesha kwamba; “Migogoro mingi inayotokana na rasilimali inazidi kuwa bayana nchini Tanzania.

Hii inaweza kutazamwa kama migogoro ya jamii dhidi ya wawekezaji (hasa kilimo cha

biashara na uchimbaji madini), migorogo ya ardhi kati ya jamii na jamii, hasa kati ya wafugaji na wakulima, kati ya wafugaji wenyewe wakigombea maji, malisho na ng’ombe (wizi wa mifugo), na migogoro kati ya jamii na Dola katika miradi ya hifadhi na maendeleo. Mara nyingi huwa kuna kiwango cha juu cha vitendo vya ukatili katika jamii za wachimbaji madini vinavyohusiana na haki za umiliki ardhi.”

2. MIGOGORO YA KIJAMII: UGUMU WAKE NA SABABU

Kule kutajwa rasmi kwa Tanzania kama “*kisiwa cha amani*” kunaonyesha kwa nini mara nyingi maofisa wa Tanzania huwa wagumu kujadili masuala yanayozungumzia migogoro na mivutano katika jamii (Bergmann, 2015 p.3). Bergmann katika ripoti yake ya “Actors Mapping of Peace Maintenance” anabainisha maeneo matano ambayo migogoro hutokea nchini Tanzania:

- Utawala na Usimamizi wa Siasa,
- Usimamizi wa Rasilimali za Asili,
- Masuala ya Kijamii na Kiuchumi,
- Uhusiano baina ya Dini mbalimbali, na
- Haki za Binadamu⁴

Uwezekano wa kutokea na kutokea kwa migogoro iliyoainishwa hapo juu inaonyesha umuhimu wa kuimarisha njia za kuboresha miundo ya amani kuanzia ngazi ya jamii hadi ya Taifa. Ni kutokana na usuli huu ndipo kitabu hiki cha mwongozo kinafafanua njia ambazo mazungumzo yamekuwa yakitumika, na bado zinaweza kutumika ili kuzuia, kutatua, kubadili migogoro hiyo hapo juu na vilevile kuleta amani endelevu nchini Tanzania.

Mifano miwili ya migogoro iliyotokea katika siku za karibuni imetajwa hapa chini kwa ufafanuzi zaidi. Kwa ajili ya kuthibitisha matumizi na umuhimu wa mazungumzo ya jamii, na zaidi sana umuhimu wa kitabu hiki cha mwongozo; ilionekana ni lazima kutazama aina mbili za migogoro iliyotokea Tanzania Bara na Zanzibar: mmoja wa kisiasa na mwingine unaohusu rasilimali.

2.1 Migogoro Inayotokana na Siasa: Tukio la Vurugu Unguja (Zanzibar) wakati wa vurugu za UAMSHO za 2012

Mwaka 2012 kulikuwa na ongezeko kubwa la harakati za wenye siasa kali hasa miongoni mwa vijana waliopambana na askari polisi na pia dhidi ya mifumo ya ulinzi wa jamii huko Zanzibar, hasa wilaya za Unguja Mjini na Magharibi. Harakati hizi ziliibuka kama sehemu ya vitendo vya UAMSHO dhidi ya polisi na kama sehemu ya kupinga Muungano wa Zanzibar na Tanganyika.

Matukio kadhaa ya kuashiria siasa kali yalitokea yakiwemo kuuwawa kwa askari kanzu huko Bububu, mashambulizi kutumia asidie dhidi ya Shekhe na Mapadre, na pia kuchomwa moto na kupigwa mabomu makanisa hasa yale ya madhehebu ya Katoliki kwa kuwa kikundi cha UAMSHO wayalikusisha na baadhi ya wanasiasa wa Tanzania. Kulikuwa na tuhuma kwamba Kanisa Katoliki lilikuwa na ushawishi mkubwa katika kuathiri na kuangamiza Visiwa vya Zanzibar chini ya mwamvuli wa Serikali ya Muungano ya Tanzania.

Uchambuzi wa haraka wa muktadha unaonyesha vigezo vifuatavyo katika mgogoro wa kisiasa wa 2012:

1. Kutoridhishwa na masuala ya Muungano wa Tanzania na wito wa Zanzibar kujitawala;
2. Ubaguzi wa kijamii na kisiasa (Wazanzibari walihisi kuwa walikuwa wakitengwa kiuchumi na kisiasa na Tanganyika kupitia Serikali ya Muungano);
3. Ukosefu wa ajira kwa vijana, matakwa ya vijana kutotimizwa, ahadi za Serikali zisizotimizwa na watendaji wake;
4. Ghadhabu, hasira na chuki za kisiasa za kihistoria;
5. Tuhuma za kuharibiwa kwa amali za utamaduni wa Zanzibar kwa sababu ya mila za Bara (masuala ya dini).

⁴ Kwa taarifa zaidi kuhusu aina zilizobainishwa za migogoro rejea ripoti kamili iliyoandikwa na Danja Bergmann (2015) kuhusu “Kubaini Wadau katika Kudumisha Amani”

Lengo la Kuingilia Kati

Mwaka 2013 ILPI ilipata ruzuku ya mwaka mmoja (Okt. 2013-Sept. 2014) kutoka katika Ubalozi wa Marekani jijini Dar es Salaam ili kutekeleza mradi uliojulikana kama “Kuto Fursa kwa Amani na Mazungumzo”, ambayo baadaye ilipewa jina la Kituo cha Vijana cha Mazungumzo. Mradi huu ulikuwa na malengo matatu:

- Kujenga imani kati ya polisi na vijana kupitia mazungumzo ili kuondoa pengo la mawasiliano na pia kukuza maelewano kati ya serikali na vijana na hata jamii kwa ujumla;
- Kutoa elimu kupitia mafunzo mbalimbali juu ya haki za binadamu, utawala bora, ujasiriamali, utawala wa sheria, utafutaji suluhu wa amani na kuzuia migogoro, ulinzi wa wanawake na watoto, uongozi, elimu ya uraia, mitandao ya kijamii, lugha ya Kiingereza, n.k.; na
- Kuongeza ushirikiano kati ya polisi na jamii katika kutoa taarifa na kukabili siasa kali.

Mafanikio ya Mradi ni Pamoja na:

- Kubadilika kwa mitazamo na kuongezeka kwa ushirikiano kati ya serikali (polisi) na jamii hasa vijana.
- Uendeleu wa shughuli za mradi, yaani, kuanzishwa kwa Kituo cha Malezi cha Serikali ya Zanzibar, kuongezeka kwa vijana wengi katika maktaba ya TAYI kuliko katika ile ya Taifa kwa siku.
- Kurekebisha mwenendo wa kundi moja lililojulikana kwa jina la *Ubaya Ubaya*⁵ ambao walibadili jina na kujiita *WemaWema*⁶. Kundi hili la WemaWema sasa wamejisajili kama asasi ya kiraia ambayo inalenga kujenga jamii bora kupitia shughuli kama vile kuendeleza ushirikiano unaokuza kiwango cha kuaminiana na kukubalika na polisi, serikali ya Zanzibar, na makundi mengine ya vijana wa Zanzibar.

Jitihada nyingine ni pamoja na ufanisi wa vijana na mazungumzo na polisi, haki za binadamu, ushirikiano wa dini mbalimbali, utawala bora, utawala wa sheria na mafunzo ya ujasiriamali. Wanachama wa makundi ya uhalifu walianza kuishi maisha ya kawaida kama wanajamii wengine baada ya kuwa sehemu ya mradi. Kwa mfano, waliokuwa wahuni wa kundi la UbayaUbaya sasa wanashirikiana kwa karibu zaidi na hucheza hata soka na askari polisi, jambo ambalo lisingeweza kufikiriwa kabisa hapo awali.

- Kupungua kwa vurugu na uhalifu kwa asilimia 19 katika mwaka 2013-2014⁷
- Kuimarika kwa kuvumiliana na maelewano katika jamii na pia na watu wa nje.
- Kuundwa na kuimarishwa kwa vituo vya vijana vya Shirika la Maendeleo Mji Mkongwe na TAYI, yaani, kupatiwa kompyuta, projekta, vitabu vya kiada, samani na hata huduma za intaneti.
- Polisi na wanajamii kushirikiana zaidi kupitia mitandao ya kijamii hasa kupitia ukurasa wa Polisi wa Facebook, ambao sasa una wafuasi 3,929.

Mafanikio ya mradi yalitokana hasa na mazungumzo ya wazi, ujuzi wa kijamii, kisheria na kiuchumi kuimarishwa kwa makundi ya kijamii na serikali, yaani, vijana walio hatarini, wanawake, mifumo ya ulinzi jamii, viongozi wa kisiasa na dini, wageni rasmi wa kijamii na kimataifa, polisi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na asasi za kijamii na kiraia.

Wakati wa Utekelezaji wa Mradi, baadhi ya Changamoto Zilibainika, zikiwemo:

- Msaada kidogo kutoka serikalini na mwanzo wa utekelezaji miradi, lakini hii imebadilika sana.
- Vijana walikuwa na fursa chache mbadala, yaani, shughuli za kuingiza kipato, ajira, mafunzo ya ufundi na ujasiriamali, n.k.

5 UbayaUbaya inaweza kufasiriwa kama 'jino kwa jino' au 'kulipiza ubaba kwa ubaya'

6 WemaWema kwa upande wake inaweza kutafsiriwa kama 'kutenda wema wakati wote'

7 Taarifa ya Kamanda wa Polisi wa Uguja Mjini Uguja wakati wa kufunga mradi wa CYD, Septemba 28, 2014



Picha inaonyesha askari polisi wakiwa na jezi za buluu bahari na wachezaji wa UbayaUbaya wakiwa na jezi za buluu nyeusi wakati wa mechi ya mashindano ya kujenga amani mwezi Januari, 2014, Unguja, Zanzibar.

- Hali isiyobashirika, mara nyingi ikiwa na mvutano mkali, ya Zanzibar na wasiwasi kwamba vijana wangeweza kutumiwa kwa malengo ya kisiasa.
- Kutokukiri kwamba kuna siasa kali Visiwani.

Mifano hiyo hapo juu inatoa fursa ambapo modeli ya CDSP ingeweza kutumika ili ama kuzuia kuenea kwa siasa kali pale ambapo ipo tayari, au pale inapatishia kusambaa na ikiwa na uwezekano wa kuchochea migogoro ya kijamii.

2.2 Mgogoro Unaotokana na Rasilimali: Vurugu za Gesi Mtwara (2014)

Mwezi Mei, 2013, mkoa wa Mtwara ambako Tanzania iligundua hifadhi kubwa ya gesi ya asili, kulishuhudiwa vurugu zilizosababisha umwagaji damu pale wenyeji walipopinga uamuzi wa serikali wa kujenga bomba la gesi kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya usafirishaji na kuuzwa, badala ya kujengwa kiwanda cha uchakataji huko Mtwara (*Gazeti la Mwananchi* 25.05.2013). Kwa mujibu wa Ndimbwa (2014): “Serikali imekwishatilia saina mkataba na mwekezaji katika gesi na mafuta pasipo kwanza kufanya mashauriano, bila kuwa na sera na hata kabla sheria mpya haijapitishwa.

Wakati wa mdahalo wadau waliyaona haya kama upungufu mkubwa uliochochea vurugu wakati wa mdahalo” (*Ndimbwa 2014:6*). Moja ya wasiwasi wa wanajamii mkoani Mtwara ilikuwa woga wa kunyimwa haki ya kupiga kura, kunyimwa stahiki yao katika manufaa yanayotarajiwa kutokana na kiwanda cha uchakataji na mashaka kuwa wataendelea kuishi katika umaskini mkali.

Hata hivyo, wachambuzi waliona kwamba vurugu zilikuwa na uhusiano na vitu kama maslahi ya kisiasa, hasa upande wa upinzani, masuala ya kijamii na kiimani⁸. Vurugu hizo zilisababisha vifo vya takribani watu 12, mali kuharibiwa, wengine kubakwa na kuteswa na kulikuwa na tuhuma za askari kushiriki katika kuiba mali za watu (*Daily News*, 29 Januari 2013). Pia kuna madai kuwa watu kadhaa walikimbia makazi yao, huku baadhi wakihamia Msumbiji.

Hali hiyo hapo juu inahitaji kuwepo kwa mazungumzo ya jamii ambapo pande zilizoumizwa zinaweza kueleza madukuduku yao kwa namna ya kujenga pasipo kuingia katika vurugu. Mwongozo huu unatoa muhtasari wa mchakato kama vile mazungumzo yanayohusiana na jamii yanayolenga kuleta maelewano katika mkataba wa kijamii kati ya pande zinazopingana wakitumia mazungumzo kama zana ya mapatano. Lakini kwanza, hebu tufafanue zaidi hii dhana ya mazungumzo.



Mkazi mmoja akizungumza katika mkutano wa hadhara wa chama cha upinzani Mtwara.

8 <http://www.thecitizen.co.tz/News/Why-Mtwara-violence-is-beyond-gas-pipeline/-/1840392/1861170/-/ctbqen/-/index.html>

3. DHANA YA MAZUNGUMZO NA UMUHIMU WAKE KAMA NJIA NA MCHAKATO WA KUZUIA MACHAFUKO NA KUJENGA AMANI

- Mazungumzo ni moja ya njia ambazo hutumiwa sana na ziko katika njia zote za kutafuta suluhu ya migogoro na mabadiliko. Mazungumzo ni njia ya pekee ya mawasiliano ambayo ndiyo kiini cha uhusiano (Bercovitch, 2008).
- Bercovitch anaeleza zaidi kwamba kutokana na tamaduni nyingi ambako mwingiliano wa kisiasa, kijamii na kiuchumi una tabia ya kuwa wa kukinzana na kuleta mgawanyiko, kutamani kuleta utamaduni wa mazungumzo - aina nyingine ya kuhusiana - itakuwa ni mchango muhimu katika kuondoa kwa njia za amani tofauti, kutengeneza maisha na kuleta utaratibu wa demokrasia.
- Kinyume na midahalo ambayo huwaweka watu katika makabiliano juu ya suala fulani na uhusiano wa kiuhasama, mazungumzo huandaliwa katika namna ya kujenga maelewano, ushirikiano na uhusiano chanya.
- Mazungumzo huelezwa pia kama majadiliano ambayo watu “wanazungumza waziwazi na kusikilizana kwa heshima na umakini. Majadiliano huondoa kushambuliana na kujitetea na hupusha matusi yanayohusiana na malengo, maana, au tabia ya wengine.
- Katika majadiliano, maswali hayana hila, yakichochea na udadisi na shauku. Lengo la mazungumzo ni kuimarisha maelewano baina ya pande mbili, kuongeza kuoneana huruma na kujenga uwezo wa kifikra lakini pia kuleta umakini, kujichunguza kwa makani, kujenga kuaminiana, na kufikia mtazamo usioegemea upande wowote juu ya suala linalogombaniwa na ulimwengu kwa ujumla. Kwa kuanzisha maelewano baina ya pande mbili, washiriki wanajifunza zaidi kuhusu wenzao wa kundi lingine, ikiwemo kujua tofauti zao.
- Ikumbukwe kwamba lengo la msingi la njia ya majadiliano si lazima kufikia makubaliano bali maelewano baina ya pande mbili. Kwa mfano, ni vigumu kufikia makubaliano katika mazungumzo yanayohusu mambo kama vile “kuunga au kupinga utoaji mimba; mahusiano jinsia moja; ukeketaji wanawake; wanawake kupewa daraja la upadre katika Kanisa Katoliki, miongoni mwa nyinginezo”. Katika hali ya namna hiyo, mazungumzo hutoa fursa ya pande hizo kujifunza kuhusu mitazamo ya upande wa pili, bila kutarajiwa kuondoa misimamo yao.

Mchakato wa mazungumzo ni matokeo ya maandalizi makini ili kufikia mazingira ya lazima kwa ajili ya mazungumzo yenye tija na uwanja wenye usawa, yaani, ili kuwaleta watu pamoja. Ni muhimu kuhakikisha kwamba watendaji wakuu na wadau wanakuwa tayari kwa moyo mmoja kujihusisha na mchakato huo.

3.1 Matumizi ya Mazungumzo Kama Zana ya Kuzuia Migogoro na Kuleta Mabadiliko

Sehemu hii inaonyesha baadhi ya kanuni muhimu za mazungumzo na aina tofauti za mazungumzo.

3.1.1 Kanuni kuu za Mazungumzo

Mchakato wa mazungumzo unaongozwa na kanuni zifuatazo:

Ujumuishi

Pengine hii ndio kanuni kuu kabisa ya utaratibu wa mazungumzo. Inaonyesha dhana ya msingi kwamba, kwa vile kila mmoja ambaye ni sehemu ya utatuzi wa tatizo anaweza kuhusishwa au kuwakilishwa katika mchakato wa mazungumzo,

washiriki kwa pamoja wana vipengele muhimu vya ‘ujuzi’ wanaouhitaji ili kushughulikia matatizo yao wenyewe, tofauti na kuwa wategemezi kabisa kwa watu wengine ili kupata ufumbuzi. Ujumishi/ushirikishwaji unafaa hasa palipo na muktadha wa mpangilio wa kihistoria wa ubaguzi ambao unajenga msingi wa matatizo ya jamii na ambao hauna budi kushughulikiwa. Ili mchakato wa mazungumzo uwe halali na wenye matokeo bora na imara, ni budi ujumuishi uzingatiwe.

Umiliki wa Pamoja

Ili kuleta mabadiliko endelevu, watu hawana budi kuanzisha ushiriki wa pamoja wa mchakato na kuwa wadau katika kubaini njia mpya na kushughulikia changamoto za pamoja. Mchakato wa mazungumzo haupaswi kuwa chombo cha upande (mtu) mmoja tu kuvuta muda au kukamilisha ajenda yake. Ikiwa wadau hawatajiskia kwamba huo mchakato ni wa kwao, mabadiliko yanabaki kuwa jambo la hadaa. Pale umiliki wa pamoja unapohakikishwa, watu wanasukuma mbele masuala yanahohusika kikamilifu, na hapo ndipo matokeo ya mazuri huonekana ikilinganishwa na nyakati nyinginezo.

Kujifunza

Mchakato si tu kuhusu kuketi mezani, bali huhusu kubadili namna watu wanavyozungumza, kufikiri na kuwasiliana miongoni mwao. Tofauti na aina nyingine ya majadiliano, mazungumzo huhitaji kuwepo kwa kujitafakari, kujitathmini ndani na kuwepo kwa mabadiliko ya mtu binafsi. Washiriki hawana budi kuwa tayari kushughulikia vyanzo vya mgogoro, na si dalili za juujuu tu.

Utu

Utu katika mchakato ya mazungumzo husaidia kuyatofautisha na aina nyingine za kushiriana.

Washiriki wanapaswa kuwa tayari kuonyesha kuwajali wenzao, kutambua tofauti na pia maeneo yanayowaunganisha, kuonyesha uwezo wa kubadilika. Ili kuendeleza aina hii ya mwingiliano wa kiutu, “fursa salama” yenye kuheshimu na isiyogemea upande wowote inapendekezwa. Pale watu wanapoanza kufanya jitihada za kuelewana, basi mbegu ya mazungumzo huwa imepandwa.

Mtazamo wa Muda Mrefu

Aina nyingine za mijadala huweka mkazo katika dalili badala ya vyanzo vya tatizo. Muda na ustahimilivu vinahitajika ili kupata suluhu endelevu. Mchakato unaweza kuwa wa polepole sana kiasi cha kuumiza lakini unaoongezeka taratibu, ambapo unaweza kudumu kati ya dakika kumi hadi miaka kumi - hatua ya uingiliaji kati mara moja mara nyingi haifanyi kazi katika kutatua chanzo ambacho ni cha kina kirefu cha mgogoro au kushughulika na masuala magumu sana.

3.1.2 Aina za Mazungumzo

Mazungumzo ya misimamo: haya ni mazungumzo yanayohusisha pande/jamii ambazo zinaendeleza uhasama na kubaguana, zinatupiana lawama na kubaki kushikilia misimamo yao. Katika aina hii ya mazungumzo, ni vigumu sana kupata mwafaka, maelewano na kuthaminiana.

Mazungumzo ya uhusiano wa kiutu: haya ni yale ambayo pande/jamii zinaketi na kubadilishana mitizamo, uzoefu na imani; wanakuwa tayari kusikiliza kwa uwazi na heshima; na pia kujifunza jinsi upande wa pili unavyotenda, na namna wanavyofanya; aina hii ya mazungumzo hutoa fursa za kukua kifikra, kujifunza na hata kubadili mitazamo yao. Inaweza kuleta uhusiano wenye kujenga mabadiliko chanya.

Mazungumzo ya kiuanaharakati: katika aina hii ya mazungumzo, lengo la jamii au pande zinazohusika ni kuleta ushawishi au utetezi wa ajenda au vuguvugu fulani. Yanaweza kuwa ya makabiliano wakati kila upande unataka kuhakikisha ajenda au vuguvugu lake ndiyo linapita bila kujali upande mahitaji/wasiwasi wa upande mwingine.

Mazungumzo ya kutatua tatizo: aina hii ya mazungumzo hulenga kupata uelewa wa pamoja wa masuala yanayozisibu pande zinazohusika; hufanyika katika mazingira ya warsha, mara nyingi huwezesha na wasomi na watendaji wasioegemea katika upande fulani. Huunganisha matokeo ya warsha na watu katika maisha ya kawaida na wadau wengine katika ngazi ya kitaifa.

Mazungumzo endelevu: huu ni mchakato wa mazungumzo unaolenga kubadili uhusiano unaosababisha matatizo au kuleta mgogoro na kuzuia mabadiliko. Mazungumzo Endelevu si warsha ya kutatua matatizo bali kuendeleza ushirikiano kati ya pande zinazohusika ambayo huanzishwa kutokana na mfululizo wa mikutano ya miezi au miaka.

Mazungumzo akisi: hii ni aina ya mazungumzo inayochochea udadisi katika nafsi ya mtu. Huhusisha usikilizaji wa msisitizo na kwa kawaida huzaa mazungumzo chanya; yanaweza kufanyika ndani ya mazungumzo mengine na kuchangia mijadala yenye tija miongoni mwa pande zinazohusika.

Mazungumzo yenye tija: Haya ni yale yanayohusu ushirikiano na hufungua milango kwa hatua zaidi kuchukuliwa, yakionyesha maarifa mapya ambayo si rahisi kuyapata mmojammoja.

Mzungumzo ya kidemokrasia: haya ni yale yanayoheshimu na kuimarisha taasisi za kidemokrasia, yakilenga kubadili uhusiano wenye uhasama ili kuzuia migogoro na vurugu na kwa hiyo kuchangia katika kuimarisha utawala wa kidemokrasia. Mazungumzo ya kidemokrasia ni mchakato wa ushirikiano na kufanya kazi pamoja, na yanaweza kuhusisha mkutano mmoja au kadhaa ya washiriki katika mazungumzo.

Kidokezo: Kuendesha mazungumzo yenye mafanikio ya jamii, mtu hana budi kuchukua vipengele chanya kutoka katika aina tofauti za mazungumzo

4. AWAMU YA MAANDALIZI: MAZUNGUMZO YA JAMII NA AMANI ENDELEU (CDSP)

Modeli ya CDSP inatekelezwa kupitia hatua tatu muhimu yaani, ile ya maandalizi, awamu ya 1 na awamu ya 2. Awamu zote tatu zinabeba hatua mbalimbali ambazo zimeunganishwa katika mchakato kama mabadiliko ya ukuaji kuliko matukio tofauti. Hatua muhimu katika awamu ya maandalizi, tathamini ya jamii na kubaini makundi yanayolengwa (hatua ya 1), kubaini washirika (hatua ya 2), kushirikisha wadau tofauti na kujenga uwezo wa washirika watakaotekeleza (hatua ya 3) na mikutano ya utambulisho na wadau (hatua ya nne).

HATUA YA 1: TATHAMINI YA JAMII NA UTAMBUZI WA MAKUNDI YANAYOLENGWA

Modeli ya CDSP inakusudiwa kutumiwa kwa jamii na makundi ndani ya jamii ambayo yanahitaji sana mazungumzo ya jamii, jambo ambalo ni kiungo kikuu katika kuzuia mgogoro, kujenga umoja na mshikamano katika jamii.

Kabla ya kuingia kwenye jitihada zozote, ni muhimu kufanya tathmini ya jamii. Hii hufanyika kwa kutumia mbinu zilizopo za uchambuzi wa mgogoro, uchambuzi wa jinsia na uchambuzi wa misukumo ya kimamlaka. Tathmini ni zana muhimu kwa ajili ya kuelewa sababu ambazo huenda zilikuwa chanzo cha mgogoro, mivutano, wadau na uwezo wa kuzuia mgogoro. Ili asasi inayoingilia kati kuelewa vizuri masuala ya kimuundo ambayo yanaweza kukua hadi kufikia mivutano halisi na hatimaye kulipuka na kuwa mgogoro kamili wenye kuleta athari.

Tathamini ya jamii husaidia kuzalisha vyanzo vya mvutano na uwezekano wa amani endelevu. Kwa kuongezea, tathamini huwezesha utambuzi wa makundi, miundo na asasi ndani ya jamii ambazo zitafaa wakati wa kushughulikia mivutano ili yaweze kutumika vema na kwa kipindi cha kutosha.

Modeli ya CDSP inatumiwa katika mazingira ya mgogoro unaoibuka kama hatua ya kuuzuia usitokee. Modeli inalenga jamii nzima kwa kuwa amani endelevu inaweza kupatikana tu kwa kuhusisha wanajamii wote. Hawa ni pamoja na viongozi wa dini, watu wenye ushawishi wa hoja, vijana, wanawake, na mamlaka za serikali kwa kutaja tu wachache.

HATUA YA 2: KUBAINI WASHIRIKA

Washirika wanaotekeleza modeli ya CDSP wanapaswa kutimiza wajibu wa uwezesaji katika mchakato wa mazungumzo ya jamii na katika mapatano ya mikataba ya kijamii kwa ajili ya kuishi pamoja kwa amani. Wajibu kama huo hauna budi kuhusisha uratibu, uongozaji, na kusaidia uundaji wa dhana ya miradi ya amani ya jamii inayolenga kuimarisha mshikamano na ushirikiano wa kijamii; kuzuia migogoro na kuleta mabadiliko.

Hii ni muhimu kwa sababu jamii inahitaji kundi huru ili kuanzisha na kuendeleza fursa za mazungumzo. Kundi huru, kwa hiyo, huwa kama wadhamini wa mazingira ya wazi na salama ndani ya jamii ambamo inaweza kushughulika na kujadili, na pia kusawiri uwezekano wa kufikia makubaliano ya pamoja.

Wajibu wa washirika kama hao, kwa hiyo, utajumuisha kuwaongoza viongozi wakuu katika mchakato huo wa jamii, kushirikishana uzoefu wao wa mahali pengine na kuhamasisha ushiriki motomoto na michango ya wanajamii katika mchakato huo.

Kidokezo: Tathamini ya jamii hasa ni kuhusu kuchambua na kuelewa muktadha ambamo kuna uwezekano wa mgogoro au mgogoro halisi wa jamii unatokea

Wajibu wao unaweza pia kuhusisha msaada wao wa kiuchambuzi na kiufundi ili kuimarisha ujuzi wa wanajamii katika kuzuia migogoro na kuleta mabadiliko. Upande huo huru, hata hivyo, haupaswi kunyakua uongozi na umiliki wa mchakato, ambavyo kimsingi havina budi kubaki ndani na kumilikiwa na wanajamii na taasisi zao.

Vigezo vya kuchagua washirika katika utekelezaji

Baadhi ya vipengele vya kuzingatia wakati wa kubaini na kuchagua washirika wa utekelezaji ni pamoja na (lakini hii si orodha kamili):

- Asasi/chama au mfumo wa uendeshaji jamii au aina ya ushirikiano ni unaotokana na jamii na uko tayari kuunganisha programu za uzuiaji migogoro na kuleta mabadiliko.
- Asasi/chama hakina budi kutunza maarifa na welewa wa jamii inayohusika, mazingira yao na vilevile taratibu za kijamii-kiutamaduni na imani.
- Asasi/chama na wanachama wake hawana budi kuwa na sifa njema, kuonekana kwamba ni huru, wasio na ubaguzi, waadilifu na wenye kujikita katika utamaduni wa amani (kuamua kupitia michakato ya mashauriano).
- Asasi/chama hakina budi kuwa na uwezo na ujuzi wa kushughulikia usimamizi wa migogoro ikiwemo mifumo ya utoaji tahadhari ya mapema na mwikitiko wa mapema.
- Dhima na dira ya asasi/chama ni mwafaka kwa kushughulika na kuzuia migogoro na kazi zinazohusiana na kuleta amani.
- Asasi haina budi kuwa makini na masuala ya jinsia na kutambua haki za makundi yanayobaguliwa.

HATUA YA 3: KUWASHIRIKISHA WADAU MBALIMBALI NA KUJENGA UWEZO WA WATENDAJI WA UTEKELEZAJI

Matumizi ya modeli ya CDSP si mepesi kama inavyoweza kudhaniwa kwa sababu mbalimbali ambazo hujitokeza wakati wa utekelezaji. Wakati wa kuchagua wadau wa utekelezaji – na kuunganisha na ulazima wa kufanyakazi kwa ushirikiano na mfumo wa jamii – mara nyingine inaweza kushindikana kupata kiwango kinachopendelewa ili kuchagua muundo wa kiungozi na ujuzi. Kwa hiyo, modeli ya CDSP inabeba mchakato wa kutekeleza kuwajengea uwezo washirika kabla ya kuanza kwa mchakato wa mazungumzo wa jamii.

Kuimarisha Uwezo wa Washirika Waliobainishwa

Kujenga uwezo kunaweza kuchukua sura ya kuimarisha ujuzi au mafunzo, kuimarisha mfumo, kuimarisha vifaa na msaada wa kifedha katika asasi/chama kinachoshughulika na mazungumzo ya jamii na jitihada za kuhamasisha amani.

Kabla ya kuendelea na kujenga uwezo, ni muhimu kutathmini uwezo wa washirika katika maana ya upungufu wa kiujuzi na kimaarifa kwa lengo la kutoa mafunzo sahihi na ya kutosha. Kipindi shirikishi cha kutathmini uwezo hakina budi kuandaliwa kwa ajili ya asasi/kundi/chama kilichochaguliwa ili kwa pamoja kutazama vipaumbele vyao kwa ajili ya kujenga uwezo na mafunzo.

a. Mafunzo ya Washirika Waliobainishwa

Miongoni mwa mambo mengine, wanaoweza kuwa washirika waliochaguliwa wanaweza kunufaika na kuimarishwa kwa ujuzi wa msingi katika maeneo mbalimbali ya kipaumbele kama inavyoelekezwa na tathmini ya upungufu wa ujuzi/maarifa iliyofanyika. Kudumu kwa mafunzo kunaweza kutofautiana, kutegemeana na kiwango cha

maarifa kilichopo miongoni mwa washiriki. Mifano ya maeneo/mada za kipaumbele katika mafunzo ni:

- Kuelewa dhana ya migogoro, machafuko na amani.
- Zana za uchambuzi wa migogoro.
- Mbinu za kuzuia migogoro.
- Mizunguko ya migogoro.
- Mazungumzo kama zana ya kuleta amani endelevu.
- Ujuzi na mbinu za mawasiliano (Kuelewa kanuni za msingi za mwafaka).
- Mapatano, Mashauriano, Kusimamia Maelewano, Kuwezesha, n.k.
- Ukweli, Haki, Msamaha na Mapatano.
- Kujenga, Kuaminiana na Imani.
- Uongozi wa Jamii.
- Mbinu kwa ajili ya uchambuzi wa ushirikishi na mipango ya jamii.
- Uhusiano wa jinsia, mienendo ya jinsia na uchambuzi wa jinsia.
- Usimamizi na tathmini shirikishi ya miradi ya amani.
- Vipengele vya uchambuzi wa orodha ya manufaa
- Taratibu za kidini na kiutamaduni.
- Mchakato wa tathmini shirikishi.
- Kuelewa sheria za msingi na miundo ya sheria iliyopo kuhusu kumaliza na kuzuia migogoro.

Angalizo: Hizo hapo juu ni baadhi tu ya mada zinazoweza kuandaliwa kwa ajili ya kuimarisha uwezo na ujuzi. Mada nyingine zinaweza kuandaliwa kwa kutegemea na tathmini ya upungufu wa ujuzi na maarifa iliyofanywa na washirika muhimu.

b. Vifaa na Msaada wa Kifedha kwa ajili ya Jitihada za Kuleta Amani

Licha ya kuimarisha ujuzi, vyama/asasi za jamii zinazoshughulikia amani zinaweza kuhitaji msaada wa vifaa wakati wanapobaini na kutumia fursa za amani za jamii zilizopo. Rasilimali vifaa na fedha zitawawezesha kuandaa michakato ya jamii kwa namna yenye tija (mawasiliano, maeneo ya mikutano, kutia saini mikataba ya kijamii, kuanzisha miradi ya pamoja ya amani, n.k.) na kutimiza wajibu wao katika kiu ya kuleta amani na ufufuaji wa kudumu wakati kila moja ikijitegemea katika kufanya kazi dhidi ya athari zinazoweza kukwamisha amani.

c. Kupata Washirika na Wadau Wengine⁹

Licha ya kundi linalolengwa (au makundi ya wanufaikaji), ambao modeli inataka kuwaleta pamoja, na asasi/vyama vya jamii vinavyowezesha mchakato huu, modeli ya CDSP inategemea ushirikishwaji wa viongozi wa kimila na dini, wenye ushawishi wa hoja, na mamlaka. Makundi haya yanahusishwa ili kuhakikisha udhati wao katika amani na mchakato wa ufufuaji, kwani uungaji wao mkono utafanya matokeo kuwa endelevu zaidi. Kwa hiyo, wao wanahimizwa kushiriki kikamilifu katika hatua zote za modeli ya CDSP.

Mwanzoni wanaalikwa kushiriki katika mikutano maalumu ambayo inaandaliwa ili kuwahamasisha juu ya mazungumzo ya jamii, yaliyomo na mchakato wa modeli ya CDSP, na namna gani wanaweza kuchangia katika utekelezaji wao mzuri kama wanajamii na viongozi wenye ushawishi katika jamii.

⁹ Kwa taarifa zaidi, tafadhali soma aya inayohusu uchambuzi wa wadau.

HATUA YA 4: MIKUTANO YA UTAMBULISHO NA WADAU MUHIMU

a. Kuwaendea Wanajamii

Kabla ya kuzindua mchakato wa CDSP, inafaa kuitisha mikutano ya utambulisho na jamii ambapo viongozi wa kimila, watu wenye ushawishi wa hoja, wawakilishi wa wanaume, wanawake na vijana na viongozi wa jamii na/au wilaya wanawakilishwa. Malengo ya mikutano hii ya utambulisho ni:

- Kushirikisha na kuweka muktadha wa dhana ya modeli ya CDSP, njia na matokeo yanayotarajiwa;
- Kusisitiza kuwa mchakato huo hauna upendeleo na unatafuta kupata uungwaji mkono na wadau wote katika ngazi ya jamii na mamlaka za serikali na kimila.

Mikutano ya utambulisho na umma mzima inaweza kufanyika popote pale ambapo mikutano ya wananchi hufanyika. Hata hivyo hapana budi kutambua, kwamba mkutano wa kwanza unaweza kuwa na mivutano, hasa katika maeneo ambako kuna mivutano inayojijenga miongoni wa wananchi. Ni muhimu kuwa waangalifu kwamba mikutano hii inafanyika katika namna yenye ustaarabu ili kujenga imani katika mchakato huo.

Mikutano ya utangulizi na wananchi wote kwa ujumla pia inaweza kushindwa kwa sababu ya kukanwa kwa tatizo lililopo katika jamii hiyo. Ikiwa mkutano kama huo hautawezekana, inashauriwa kufuta au kuahirisha na badala yake kuelekeza nguvu katika mikutano na vikundi maalumu na sekta kama vile wanawake, vijana, wenye ulemavu, walioathiriwa na migogoro n.k. ili kupata uungaji mkono wao kwanza. Ni baada tu ya kupata uelewa wa watu na ushirikiano katika mchakato ndipo jamii nzima inaweza kuletwa pamoja na kushiriki katika mkutano wa pamoja.

Zaidi ya hayo, itafaa kuendesha vikao tofauti na viongozi wa serikali ili kuwaingiza katika machakato wa kuleta amani na kubaini wajibu wao. Wao wanabaki kuwa na wajibu na dhima yao katika mchakato wa amani hauwezi kupuuzwa na ni lazima kwamba jamii na wadau wengine wawatazame kama wasioegemea upande wowote katika mchakato. Kinyume chake, pale ambako wanatazamwa kama waliohusika na sababu za kuwepo kwa tatizo, huenda ikawa vema kwamba waunge mkono mchakato wa amani kutokea nyuma ya pazia walau katika hatua za mwanzo hadi hapo kufikiriwa kwao huko kutakapokuwa kumemalizwa kabisa.

Licha ya kuanzisha modeli ya CDSP, mikutano hii na makundi na wadau wanaolengwa pia wanaweza kutumika kufikia mwafaka katika ajenda na njia za kuzindua uingiliaji kati wa CDSP, kukubaliana kuhusu mahali na tarehe za mikutano itakayofuatia baadae (majadiliano ya jamii), na kubaini na kuchagua watu kutoka katika jamii ambao wanafaa kuongoza mchakato kama *“mashujaa wa amani”*.

Kupitia mikutano hii, wanaoweza kuwa viongozi na waitishaji huenda wakatambuliwa. Kisha wataongoza mchakato mzima, wakiipa jamii umiliki na uhalali tangu mwanzo kabisa wa mchakato.

b. Kuchagua Eneo na Tarehe ya Kipindi cha Mazungumzo

Wakati wa kujadili maeneo yanayowezekana kwa ajili ya kuwezesha vipindi vya mazungumzo ya jamii, inashauriwa kufikiria maeneo yenye ishara za kujenga imani na hali ya usalama kwa wanajamii wote. Sharti ni kwamba eneo lililochaguliwa halina budi kuwa wazi, linalofikika na lililo salama kwa watu wengi.

Kuhusu kupanga tarehe na mikutano ya mazungumzo, inasaidia kuzingatia umuhimu wa tarehe za matukio ya kimila ya jamii (kama vile jando, harusi, unyago n.k.), kiuchumi (siku

za gulio/soko), kiutamaduni na kidini (siku za kuabudu) kwa jamii ili kuepuka migongano ya vipaumbele. Hata hivyo, tarehe hizo zingeweza kutoa fursa ya kuanzisha majadiliano kama hayo kwa kuwa jamii hujikusanya mahali pamoja na kwa hiyo zingeweza kulengwa kwa ajili hiyo.

Inapendekezwa kwamba uchaguzi wa tarehe kwa ajili ya mazungumzo ufanywe kwa namna ya kushauriana ili kukubaliana kuhusu tarehe zilizo mwafaka kwa mitazamo ya kijamii na kiutamaduni ya jamii inayohusika.

c. Kuchagua na Kujenga Uwezo wa Vinara wa Amani¹⁰

Katika maandalizi ya mazungumzo ya jamii, jamii inabaini na kutoa wawakilishi wake. Inashauriwa kuwaruhusu wanajamii wenyewe kubaini watu wanaoona wanafaa kwa ajili ya mchakato. Mikutano ya kikundi na wanajamii mbalimbali ingeweza kusaidia kwenye hili. Mara uungaji mkono unapokuwa umepatikana, na mchakato umekwishaelezewa kwa wanajamii, wanashauriwa kuchagua wawakilishi wao katika vipindi vya mazungumzo.

Ni muhimu kuhakikisha kwamba wakati wa mikutano ya kundi, sauti za wadau mbalimbali, kama vile wanawake, vijana na makundi ya wanaotengwa, zisikike. Katika mchakato huo wa kuchagua vinara/mashujaa, inasaidia kuzingatia kukubalika kimaadili, udhati kwenye mazungumzo na uwezo wa watu vinara waliopendekezwa ili kufikisha ujumbe kwa mdomo na/au kwa maandishi.

Vikundi vingi havitakuwa na uhakika kuhusu namna machakato utakavyokuwa. Katika hali ya

namna hiyo, wanaweza kutoa wenye siasa kali, wapandikizi wa chuki au wale wanaoamini kuwa watapigania vizuri zaidi maslahi yao kwenye mikutano hii. Kama hili litatokea, inashauriwa kutowakataa watu hawa. Hii ni kwa sababu wanaaminiwa na jamii zao, kuwakataa inatoa picha kwa jamii kwamba mchakato una ajenda zaidi ya vile ulivyoелеzewa.

Changamoto itakuwa kuwabadili hawa katika mitazamo yao na kuwafanya wawe watetezi wa amani. Mara wanapokuwa wamegeuzwa, huwezi kupata watu wenye udhati wa kutosha kuwazidi hawa katika kutetea amani.

Kundi hili la watu vinara litashiriki katika programu ya kujenga uwezo inayotolewa kwa washirika watekelezaji, ambapo italenga katika:

- Dhana ya Amani, Vurugu na Migogoro;
- Mbinu za kuzuia migogoro;
- Kubaini eneo la mgogoro;
- Kuchambua mgogoro;
- Ujuzi na mbinu za mawasiliano;
- Mazungumzo kama zana ya kuhamasisha amani endelevu;
- Kujenga kuaminiana na imani;
- Uongozi wa jamii;
- Viashiria vya mapema vya kuonya hatari.

Wajibu wa watu vinara wa amani ni kutetea utamaduni wa mazungumzo na kuibaini ndani ya jamii kwa utaratibu wa kila siku na kusaidia kuhamasisha jamii kushiriki katika vipindi vya mazungumzo.

¹⁰ Tazama hoja ya 3.2.

5. AWAMU YA 1: KUPATA MKATABA WA KIJAMII WA WANANCHI

Awamu yenye mafanikio ya maandalizi inafuatiwa na awamu ya kwanza (1) ya modeli ya CDSP. Lengo la jumla la awamu ya 1 ni kuzisaidia jamii kupata mkataba wa kijamii (au mkataba wa amani) kupitia hatua tatu zifuatazo: kuzinduliwa kwa modeli ya CDPS (Hatua ya 5), kuendesha majadiliano ya kijamii au vipindi vya mazungumzo (Hatua ya 6) na kupitishwa na kutiwa saina kwa mkataba wa kijamii (Hatua ya 7).

Mkataba wa kijamii wa jamii au makubaliano ya amani yanaeleweka kama ahadi rasmi ya jamii inayohusika kuishi pamoja kwa amani, kuzuia migogoro ya baadaye na kuchukua jitihada kwa ajili ya maendeleo ya jamii yao. Ahadi hii inapatikana baada ya mfululizo wa mazungumzo ya jamii kujadili kwa uwazi masuala yanayoihusu jamii yao na ambayo yana uwezekano wa kulipuka kuwa migogoro yenye machafuko na kwa pamoja kutafuta njia za kujenga za kushughulikia masuala hayo.

HATUA YA 5: UZINDUZI WA MAZUNGUMZO YA JAMII KWA AJILI YA AMANI ENDELEU

Uzinduzi ndio njia rasmi ya kutambulisha mchakato wa Mazungumzo ya Jamii na Amani Endelevu katika jamii pana zaidi. Ushiriki katika uzinduzi unajumuisha wadau mbalimbali (wazee wa jamii, wanaume, wanawake, wavulana na wasichana; viongozi wa jamii; viongozi wa dini na kimila n.k.) na pia vinara wa amani katika eneo, watendaji wengine wa maendeleo na kiutu wanaofanya kazi katika eneo linalohusika, kwa kutaja wachache tu.

Kimsingi, vipindi vya mazungumzo vinapaswa kuanza mara moja baada ya uzinduzi rasmi wa mpango.

Uzinduzi rasmi hutumika kutambulisha asasi/vyama vinavyotekeleza mchakato wa amani kwa jamii pana. Pia ni fursa ya kuangazia umuhimu wa mchakato wa majadiliano ambao utaanza kutekelezwa.

HATUA YA 6: MAZUNGUMZO YA JAMII AU VIPINDI VYA MAZUNGUMZO

- Modeli ya CDSP ni mchakato wenye mlengo wa kuzia migogoro ambao ulibuniwa ili kuanzisha vipindi vya majadiliano au mazungumzo yaliyokuwa yanalenga kushughulikia masuala ambayo yangeweza kusababisha migogoro.
- Ili kuanzisha majadiliano ya jamii, mwezesaji na wanajamii wanapata kipindi cha mwanzo ili kuweka miongozo ya mawasilinao (kuanzisha kanuni za ushirikiano na miongozo ili kuwa na majadiliano yanayojenga) na kushirikishana baadhi ya masuala nyeti na mihemko inayogusa suala linalojadiliwa.
- Kuelezwa huku kwa mihemko kunapaswa kusimamiwa kwa makini ili kwamba kusitawale mchakato na kuufanya mgumu katika kulinda uungwaji mkono ambao tayari ulikwishapatikana kutoka katika jamii. Mihemko mikali inaweza kuleta dhana potofu kwa washiriki, na isiposhughulikiwa sawasawa, inaweza kuwazuia kushiriki kikamlifu katika mchakato wa mazungumzo.
- Polepole, jukwaa linakuwa likiandaliwa ili kuandaa kwa pamoja tathmini ya muktadha: tatizo, chanzo chake, na kutambua wajibu uliotekelezwa na kila mwanajamii na ambao ulichangia katika kufika hali ya sasa.
- Kisha pande zinazohusika zinasaidiwa kushiriki katika mchakato wa dira ambayo inalenga katika aina ya jamii ambamo wangependa kuishi katika siku zijazo .
- Kutokana na dira hii, wanafanya kazi kurudi katika hali ya sasa, na kwa pamoja kuandaa

njia za kuzuia migogoro na kuendeleza jamii zenye amani katika muundo wa “mkataba wa jamii” ulioimarishwa katika “mkataba wa jamii”.

- Kisha mkataba wa jamii uliopatikana unaimarishwa kupitia ushirikishaji katika maendeleo ya jamii na miradi ya amani.

Kwa hiyo, majadiliano ya jamii au vipindi vya mazungumzo ya jamii vinaweza, kuwekwa katika muhtasari huu wa hatua tano za jumla, yaani:

- i. Kusimamia mihemko/mitazamo
- ii. Kushughulika na ukanushaji
- iii. Kuchambua tatizo
- iv. Kujenga mtazamo wa baadaye wa jamii wanayoitaka na kupatana kuhusu mkataba wa amani wa jamii
- v. Kuunda na kutekeleza maendeleo ya jamii na miradi ya amani

Angalizo:

Ingawa kitabu hiki cha mwongozo kinaelezea hatua hizi kama mchakato tofauti, kiuhalisia kuna uwezekano kwa mingine kuingiliana ana kubadilishana kulingana na mahitaji yajamii inayolengwa. Mchakato ni changamani. Lengo ni kwa jamii nzima kushiriki katika vipindi vya mazungumzo. Pale ambapo hili haliwezekani, ni muhimu kuwa makini katika kuhakikisha kuna uwakilishi kutoka katika matabaka yote ya jamii zinazolengwa, yaani, wanaume, wanawake, wazee, vijana, makundi ya wachache, n.k.

Mashujaa wa amani wana mchango muhimu wakati wa mchakato huu katika kuhakikisha ushiriki endelevu wa jamii zao au sehemu za jamii, na katika kumudu mivutano hii ambayo huenda ikaibuka. Kwa kawaida mikutano ya kijamii huwaleta karibu watu 200 kwa wakati. Ili kumpa kila mmoja fursa ya kujieleza, huenda itakuwa vema zaidi kuwagawa katika vikundi vidogovidogo vya watu 15. Hii ni muhimu hasa kwa uchambuzi wa matatizo.

Ugawanyaji huu unaweza kuchukua miundo tofauti (au muunganiko wa aina hiyo).

Kwa mfano, mtu angeweza kupanga washiriki kwa namna ambayo kila kundi dogo linajumuisha uwakilishi kutoka katika matabaka yote ya jamii, (kwa mfano, kila kundi dogo linapaswa kujumuisha wanaume, wanawake, wazee, vijana wa kiume kwa kike, na viongozi wa dini katika jamii). Tofauti na hayo, washiriki wangeweza kuwekwa katika makundi kwa kuzingatia matabaka yao (kwa mfano, wanawake wote pamoja, vijana wote pamoja, watu wa pembezoni wote, n.k.).

Baada ya hapo, kipindi cha mkutano wa pamoja ni muhimu kuhakikisha kwamba sauti ya kila mmoja inasikika. Hii ina maana kwamba makundi tofauti katika jamii yanashiriki katika mijadala ya vikundi.

Pale ambapo hili haliwezekani, kwa mfano, kwa sababu ya vikundi fulani vichache, au hofu ya kulipizwa kisasi ikiwa maoni yao yataelezwa wazi, asasi za kuingilia kati zinaweza kuhitaji kuanzisha vikundi tofauti vya mijadala na kuanzisha mfumo kwa kubadilishana mitazamo ya kundi, labda kupitia kundi la mashahidi wa amani. Kilicho muhimu ni kwamba masimulizi tofauti kuhusu suala hili yako mezani na kutambuliwa na makundi tofauti kama sehemu ya kitu kizima. Asasi inahitaji kutafuta njia za ubunifu ili kuhakikisha kwamba jambo hili linatokea.

Kwa ujumla, mijadala ya jamii ni changamani na inapitia hatua mbalimbali kutoka uchambuzi wa tatizo hadi kutia saini mkataba wa jamii. Muda halisi unaohitajika utategemea uzito wa suala linaloshughulikiwa na utayari wa wanajamii kushiriki katika mazungumzo. Ni afadhali kutenga muda kwa ajili ya mchakato huu, kwa kuwa unaunda msingi wa amani ya kudumu na endelevu katika jamii.

6.1 Kusimamia Hisia/Maoni

Hatua ya mwanzo ni sehemu muhimu ya mazungumzo na inalenga kupata wanajamii wa kueleza maoni yao na hisia zinazohusu suala litakalojadiliwa.

Washiriki pia wanahimizwa kukubaliana kuhusu kanuni ya mwenendo kupitia vipindi vyao. Hii inafanyika kupitia:

- Kuweka “Kanuni za Mazungumzo” kabla ya mazungumzo kuanza.
 - Mifano ni pamoja na (ingawa hizi si pekee):
 - Kila mwanachama atanufaika na mchakato wa mazungumzo, yaani, ni ushindi kwa kila mmoja.
 - Ni lazima kuwa na usikivu makini.
 - Watu wote wana haki ya kuzungumza na kusikilizwa, bila kujali jinsi, umri, dini, asili au msimamo wa kisiasa.
 - Hakuna mwenye haki ya kumkatisha mtu mwingine wakati wa kuzungumza.
 - Epuka kukashifiwa na kukatishwa na watu wa pande nyingine.
 - Mapendekezo yatakayotolewa hayawezi kufunguliwa mashtaka baada ya mapatano.
 - Kuweka mazingira yanayoruhusu mazungumzo yenye udhati wa kustawi
- Wanajamii wanachambua matatizo, matokeo na suluhu zinazowezeke kuwezesha amani endelevu.
- Washiriki kutoka katika makundi tofauti ya kijamii (makabila/koo tofauti, matabaka ya kijamii, wanaume, wanawake, vijana) yanaalikwa kutoa uzoefu wao ambao utatumika kama msingi wa mabadilishano miongoni mwa makundi tofauti yaliyowakilishwa.

Vipindi havina budi kuwa vya kirafiki na shirikishi kadiri inavyowezeke.

Kidokezo: Inashauriwa kuwa na wawezeshaji wanaojua vema masharti ya namna ya kusimamia mihemko au hisia na hofu zinazoweza kutokea wakati wa vipindi vya mazungumzo

6.2 Kushughulika na Ukanushaji¹¹

Moja ya vikwazo vikuu katika kutafuta ufumbuzi wa migogoro ni kukana – wakati watu wanapokana kwamba hakuna mgogoro, iwe kwao wenyewe au mtu mwingine.

Kukana huku kunaweza kutokana na sababu nyingi, kama vile:

- Hofu kwamba kukubali kuwepo kwa mgogoro kutafichua uhusiano.
- Kuamini kwamba kukiri kuwepo kwa mgogoro ni kukiri kushindwa kwa upande wako.
- Kuhofia mgogoro wenyewe na kujihofia (hii ni kweli hasa kama umekulia katika mazingira ya mgogoro) na,
- Hofu ya kwamba kukiri kuwepo kwa mgogoro kunaweza kusababisha – vurugu, kwa mfano.

Kukana kunaweza kuonekana kwa kuficha, ambapo mtu anaamua kukataa kukubali kwamba mgogoro upo, au kwa kujitoa (ambapo mtu fulani anaondoka moja kwa moja au kwa muda). Katika mazingira yote mawili ‘mkanushaji’ hatakuwa na mchango katika kupata ufumbuzi na hakuna uwezekano mkubwa wa suluhu kamili kupatikana, kwa sababu hakuna anayejua kile ambacho ‘mkanushaji’ anahitaji.

Kimsingi, haiwezekani kupata ufumbuzi wa mgogoro ambao haujatambuliwa. Kwa hiyo, ni wajibu wa mwezeshaji katika mchakato kutumia ujuzi na mbinu mwafaka ili kuifanya jamii ielewe na kutambua jambo lililo hatarini. Kwa hiyo, uchambuzi mzuri wa mgogoro na stadi za mawasiliano zinahitajika katika hali hii.

6.3 Kushughulika na Tabia Zitokanazo na Haiba

Jinsi watu wanavyopokea migogoro hutofautiana na huathiriwa sana na mahitaji, nafasi zao na namna maslahi yao yanavyoguswa¹². Kwa hiyo, hakuna budi kuwa tayari kukutana na haiba tofauti wakati wa kushughulikia mgogoro. Kwa

¹² Tazama zana za uchambuzi wa migogoro

sababu hii, lazima utarajie kukutana na watu wanaotoa ushirikiano bila shida, kupokea na kuwa tayari kuridhia suluhisho wakati wengine wataleta ubishi, kutokuwa tayari kuridhia suluhisho au kuwapokea wengine.

Kwa ujumla, kuna njia kuu tatu ambazo watu huitikia wengine katika nyakati za migogoro: wapo wanaoitikia kimyakimya, wengine wana vurugu na wapo ambao huwa na mtazamo chanya. Upokeaji wa kimyakimya huchukua tabia ya unyonge, ambapo mgogoro huepukwa lakini ni jambo ambalo hufanya ukue zaidi, hasa kwa sababu kuna mambo ambayo hayakushughulikiwa. Watu wanaopokea kimyakimya huelezea chuki zao kwa wengine, na hujaribu kutafuta uungwaji mkono wa wengine.

Wale wanaopokea kwa vurugu nyingi njia yao inaweza kufanyakazi kwa muda mfupi, maana watu wanaweza kulazimishwa kupokea matokeo. Ni mara chache sana kwamba njia hii ya vurugu inaweza kuleta suluhu ya muda mrefu, kwani wale ambao wamelazimishwa kupokea wanaweza kubaki na chuki kwenye nafsi zao.

Njia ya kupokea kwa mtazamo chanya ndiyo ambayo ina uwezekano wa kuleta suluhu ya kudumu, kwani hii ndiyo njia ambayo kuna mazungumzo ya wazi kati ya pande zinazohusika na nia ya kufanikisha upatikanaji wa mahitaji ya pande zote. Kuna kukiri kwa dhati juu ya kile ambacho kila mmoja anahitaji na mkazo huwa katika matokeo ya haki.¹³

6.4 Uchambuzi wa Tatizo

Modeli ya CDSP imejikita katika kuwaleta wanajumuiya pamoja ili kufanya mazungumzo/ majadiliano ya kina na hivyo kuwaongoza kuchambua matatizo fulani yaliyobainishwa au masuala yanayowaathiri au yanayoweza kuvuruga kuishi kwao pamoja kwa amani.

Mchakato wa mazungumzo au majadiliano huchukuliwa kwa mtazamo wa kutafuta chanzo cha masuala yaliyobainishwa na kuibuka na njia/ namna ya kuzuia au kuyabadili au kuwa kwenye njia ya kuelekea katika kupata amani endelevu. Mtu anaweza asifikiri sana kwa nini uchambuzi wa kina wa masuala yanayotishia kuishi pamoja kwa amani na kuathiri wanajumuiya kwa namna hasi ni jambo muhimu katika kupata suluhu ya kufaa kwa uwezekano wa mgogoro au sababu halisi za mgogoro zilizobainishwa.

Uchambuzi wa mgogoro unahitajika ili kusaidia jamii kubaini na kushughulikia masuala na watu sahihi, mikakati ya kuingilia kati, na rasilimali za kushughulikia hali hizo.

Zaidi ya hayo, uchambuzi bora wa mgogoro pia unahitaji kuelewa hatua au ngazi mbalimbali ambazo mgogoro hupitia. Kabla ya kuelekea njia tofauti ambazo zinaweza kutumika kuchambua mgogoro, ni muhimu kwa jamii zinazotumia modeli ya CDPS kutambua hatua mbalimbali za mgogoro kama zinavyoonyeshwa hapa chini.


Daima wakati wa kutafuta amani endelevu katika jamii, ni muhimu kutambua na kuelewa haiba za watu na kujiandaa kwa ujuzi unaostahili wa namna ya kushughulika nao wakati wa kutatua migogoro katika jamii.

¹³ https://crana.org.au/uploads/pdfs/Other_44.pdf, imesomwa mnamo tarehe 24 Machi, 2016

6.5 Hatua za Mgogoro

Migogoro hutokea hatua kwa hatua kwa vile huanzia mahali fulani na kuendelea hadi kumalizika. Modeli ya wimbi ni kielelezo cha hatua za mgogoro. Husaidia kubaini hatua ambapo vita vimefikia na inaweza kufaa katika kuelewa mgogoro na vyanzo vyake.

Hatua za mgogoro au amani



6.6 Zana za Kuchambualia Mgogoro

Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, uchambuzi wa mgogoro ni utafiti wa kitaalamu wa sura, vyanzo, wahusika, mivutano na hatua za mgogoro; husaidia jamii zinazotumia modeli ya CPDS kupata uelewa bora zaidi wa mgogoro wanaotaka kuutatua kupitia mazungumzo. Ili kuelewa mgogoro wao, jamii zinaweza kutumia zana tofauti zikiwemo hizi:

- i. Uchambuzi wa mti wa tatizo;
- ii. Kujenga taswira ya mgogoro;
- iii. Modeli ya kitunguu;
- iv. Modeli ya mlima wa barafu;
- v. Pambetatu za mgogoro;
- vi. Muda wa mgogoro kutokea;
- vii. Zana ya Pande 4;
- viii. Uchambuzi wa nguvu za eneo. .

Maelezo ya kina zaidi juu ya zana hizo hapo juu yanafuata hapa chini:

Zana ya 1: Uchambuzi wa Mti wa Tatizo

Uchambuzi wa Mti wa Tatizo (unaojulikana pia kama Uchambuzi wa Hali au Uchambuzi wa Tatizo) husaidia kubaini suluhu kwa kutengeneza ramani ya mwonekano wa sababu na matokeo kushusiana na suala hilo. Mifano ya maswali ya kutumia kwenye majadiliano katika kundi dogo ni:

- i. Je, unafikiri chanzo cha mvutano au mgogoro huu ni nini?
- ii. Je, mvutano au mgogoro huu unaweza kuleta matokeo gani?
- iii. Je, unapendekeza suluhu zipi zifanyike katika ngazi za jamii na mkoa/taifa?

Njia hii hutoa manufaa mbalimbali, kama vile:

- Tatizo linaweza kugawanywa katika vipande vidogo ambavyo ni rahisi kuvimudu. Hii huwezesha utoaji kipaumbele kufanyika kwa ubayana zaidi.
- Hii hutoa welewa mzuri zaidi wa tatizo, ni changamani na pia hutoa vyanzo vinavyokinzana. Hii kwa kawaida huwa ni hatua ya kwanza katika kutoa suluhisho la kufaa.
- Hii hubainisha masuala na hoja zinazoundwa, na inaweza kusaidia kutambua wanaohusika na michakato katika kila hatua.
- Inaweza kusaidia kubainisha iwapo taarifa zaidi, ushahidi au rasilimali zinahitajika.
- Masuala ya sasa, badala ya masuala dhahiri, yajayo au yaliyopita, yanashughulikwa na kubainishwa.
- Mchakato wa uchambuzi mara nyingi husaidia kujenga uelewa, malengo na utekelezaji wa pamoja.

Uchambuzi wa Mti wa Tatizo hutumika vizuri zaidi katika kundi dogo la majadiliano linalotumia karatasi za kubandika. Hatua ya kwanza ni kujadili na kukubaliana juu ya tatizo au suala litakalochambuliwa; tatizo huitwa “tatizo la kujadili”. Usihofu endapo itaonekana kwamba mada ni pana kwa sababu Mti wa Tatizo utasaidia kuligawanya katika sehemu ndogondogo.

Tatizo au suala linaandikwa (na/au kuchorwa) katikati kwenye karatasi iliyoandikwa kwenye ubao maalumu na linafanywa kuwa “shina” la Mti wa Tatizo. Maneno si lazima yawe sahihi kabisa kwani mizizi na matawi yatafafanua zaidi, lakini ni lazima lieleze tatizo la kweli ambalo kila mmoja anaona kweli lipo.

Baada ya kundi hili kubaini vyanzo vya tatizo kiini; vyanzo hivi vinakuwa “mizizi” ya Mti wa Tatizo. Matokeo yake, mjadala unahamia kwenye kubaini matokeo, ambayo yanakuwa “matawi” ya Mti wa Tatizo.

Lengo la zoezi hili ni kujadili na kuzungumzia vipengele vya mjadala wa Mti wa tatizo, na kuwaruhusu washiriki kupangilia au kuuvunja katika vipande vidogovidogo, na inawezekana kuvunja zaidi mizizi na matawi ili kueleza vyanzo na matokeo ya mvutano uliopo kwa undani.

Waruhusu watu kutumia muda wa kutosha kueleza hisia na fikra zao na weka rekodi ya mawazo au fikra zinazoonekana katika karatasi tofauti chini ya vichwa vya habari kama vile suluhu, wasiwasi na uamuzi. Maswali ya majadiliano yanaweza kuwa:

- Je, Mti huu wa Tatizo unawakilisha hali halisi? Je, hali za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni za tatizo zimeakisiwa ipasavyo?
- Je, kuna matokeo gani mabaya kabisa ya mvutano? Je, ni yapi yanaleta wasiwasi zaidi? Ni vigezo gani ni muhimu kwetu katika kufikiri kuhusu mwelekeo wa baadaye?
- Je, ni vyanzo na matokeo yapi yanapata unafuu, ni yapi yanazidi kuwa mabaya na ni yapi hayabadiliki?
- Je, ni vyanzo vipi ni rahisi kuvishughulikia? Je, ni vipi ni vigumu kuvishughulikia? Je, kuna matokeo gani au njia gani mbadala?
- Je, ni ufumbuzi upi unaweza kushughulikiwa katika ngazi ya jamii? Je, upi unahitaji hatua katika ngazi nyingine? Na nani atashughulikia?
- Je, tunaweza kupata mahitimisho gani?

Mwongozo wa Kina wa Uchambuzi wa Mti wa Tatizo

Mti wa Tatizo ni uwakilishi kwa kielelezo cha “mzizi” wa tatizo, na athari za tatizo ni “matawi”. Mchakato huu unachochea na kupanua fikra kuhusu uwezekano au vyanzo halisi vya mgogoro na husaidia kubaini sababu za tatizo.

Kwa upana zaidi, njia hii huwasaidia wadau kushughulikia vyanzo vya matatizo kwa mipango halisi inayoeleweka.

Vifaa vinavyohitajika

- i. Kadi za faharisi Karatasi za kubandika
- ii. Kalamu na daftari
- iii. Mawe, kokoto, punje za maharage/mahindi
- iv. Karatasi za kufundishia za kufunua

Uchambuzi wa Tatizo katika Hatua Nne Kuu Zifuatazo:

- i. Mkubaliane kuhusu tatizo au hitaji linalotakiwa kuchambuliwa;
- ii. Mbaini ‘kiini cha tatizo’, yaani, tatizo au hitaji ambalo kundi linalolengwa linachukulia kuwa ndiyo changamoto kuu;
- iii. Mbaini matatizo mengine yote yanayohusiana na kiini cha tatizo;
- iv. Andaeni Mti wa Tatizo ili kuonyesha mfuatano wa matatizo yote kwa maana ya uhusiano wa chanzo na athari.

Mti wa Tatizo hauna budi kuandaliwa kama kazi shirikishi ya kikundi (kikundi cha watu 6 hadi 8 ndiyo kipimo kizuri: kama kuna watu wengi zaidi wanataka kushiriki, basi tumia vikundi vingi).

Ni muhimu kuhakikisha kwamba vikundi vimeundwa kwa namna inayowezesha mitazamo fulani, hasa ile ambayo haina nguvu sana, kuelezwa. Kwa mfano, mara nyingi wanawake wana mtazamo tofauti sana juu ya matatizo ya jamii kuliko wanaume.

Kuandaa Mti wa Tatizo (Hatua 5):

Hatua tano zifuatazo zinaweza kusaidia kuandaa mti wa tatizo:

- i. Vipindi vya bunguabongo ili kubaini kiini cha tatizo; liandike kwenye kadi au “karatasi za kubandika”;
- ii. Bunguabongo ifanyike katika matatizo yote yanayohusiana na kiini cha tatizo na kila tatizo liandikwe katika kadi tofauti (au “karatasi za kubandika”);
- iii. Tayarisha mfuatano wa vyanzo na athari – matatizo ambayo yanasababisha moja kwa moja kiini cha tatizo yawekwe chini yake, na matatizo ambayo yanaathiri kiini cha tatizo yawekwe juu;
- iv. Kwa kila tatizo uliza “Nini kinasababisha tatizo hili?” Andika sababu katika kadi tofauti na iweke chini ya tatizo ambalo inasababisha. Endapo kuna sababu mbili au zaidi za tatizo, na moja ni chanzo cha nyingine basi ziweke katika ngazi moja;
- v. Pitia mti wa matatizo ili kuukamilisha na kuleta usahihi na unganisha matatizo na mishale/mistari ya vyanzo na athari ili kuonyesha uhusiano (tazama mfano hapa chini).

Mambo ya kukumbuka:

Ubora wa mti utategemea kuhusishwa kwa watu sahihi.

- i. Huenda ikawa vema sana kuendesha warsha tofauti ya uchambuzi wa tatizo na makundi ya wadau tofauti;
- ii. Mchakato ni muhimu kama yalivyo matokeo na itazamwe kama uzoefu wa kujifunza na kujenga uhusiano;
- iii. Mti wa tatizo unapaswa kuwa sahihi lakini ni kiwakilishi rahisi cha hali hasi ya sasa;
- iv. Usijaribu kushughulikia kila chanzo cha kila tatizo lililobainishwa—weka mkazo katika yaliyo muhimu zaidi.

Mchakato

Hatua ya 1 – Andaa kiini cha tatizo

- i. Kikundi kitapaswa kukutana kwa takribani saa moja hadi dakika 90.
- ii. Mwezeshaji ataanza kwa kuweka kadi ya faharisi – huku tatizo limeandikwa au kuchorwa kwenye kadi – katika eneo la katikati la nafasi iliyo wazi.
- iii. Kadi ya tatizo haina budi kujumuisha maneno na mchoro ili kueleza hali hasi iliyopo;
- iv. Epuka kuelezea tatizo kama kutokuwepo kwa suluhisho au kuonyesha chanzo au athari ya tatizo.

Hatua ya 2 –Baini vyanzo vikuu

- i. Waombe washiriki, kwa kutumia mwafaka wa kikundi, kubaini vyanzo/matukio makuu yaliyosababisha tatizo. Zingatia: vyanzo vya kufaa huakisi hali hasi iliyopo.
- ii. Waelekeze washiriki kuweka alama (kipande cha jiwe au kijiti) kuwakilisha kila sababu katika mstari kwa upande mmoja (kwa kawaida huwa chini) ya kadi ya faharisi/alama inayowakilisha tatizo.
- iii. Kisha mwezeshaji anaandika jina la kila chanzo kwenye kadi ya faharisi na kuiweka kadi hiyo chini ya alama inayowakilisha chanzo.
- iv. Mwezeshaji anauliza kuhusu kila chanzo, “Je, ni kwa vipi chanzo hicho kimesababisha kipaumbele cha suala/tatizo?”
- v. Andika maelezo yanayotolewa na watoa majibu.

Hatua ya 3 –Baini viini vya vyanzo

Kubaini viini vya vyanzo vya mgogoro/tatizo kunaweza kuhusisha mchakato ufuatao:

- i. Mwezeshaji awaombe washiriki kuonyesha orodha ya matukio yaliyosababisha vyanzo vikuu/matukio ya tatizo;

- ii. Kanuni iliyozeleka ni kuuliza mara tano “Nini kinasababisha...?” kwa kila chanzo/tukio kuu ambalo husababisha tatizo au hadi hapo washiriki wawe hawana tena cha kufikiri;
- iii. Kwa mfano, kila chanzo/sababu kuu (X) uliza, “Ni mambo gani (Y) ambayo husababisha X?” na kisha “Nini husababisha Y ambayo nayo husababisha X?” na kisha “Nini husababisha hilo?” n.k.
- iv. Endelea na mtiririko huu wa maswali kwa kila chanzo/tukio kuu lililosababisha tatizo;
- v. Waombe washiriki, kwa kuzingatia mwafaka, kuonyesha kwa mchoro mfuatano wa matukio uliosababisha tatizo kwa kuweka alama ardhini na kuchora mistari kati ya alama kwa namna ambayo inaunganisha matukio katika mpangilio uliotajwa;

Tunauliza maswali haya ili kulitazama tatizo kwa kina na kujaribu kuelewa vyanzo vya ndani. Hii ni ili kwamba tuweze kushughulikia tatizo kwa kupata suluhu zitakazoshughulikia viini vya tatizo badala ya ishara ambazo ni za bandia.

Hatua ya 4 –Baini viini vya chanzo “vilivyo muhimu zaidi”

- i. Mara baada ya kukamilisha Mti wa Tatizo, basi kikundi kichague, kutoka miongoni mwa viini vya vyanzo vilivyobainisha, vile ambavyo wanafikiri ndio vyanzo vikuu vya tatizo.
- ii. Wahimize washiriki kupanga miongoni mwa vile vyanzo kile kilicho mbali zaidi na “mzizi” wa mti wa tatizo.
- iii. Kwa mfano kwa njia shirikishi: Kama kuna viini vya vyanzo vipatavyo kumi na mbili, waombe wanakiundi kuchagua vile sita vya muhimu kabisa (nusu ya jumla). Kama kundi – kwa kutumia mwafaka pale inapowezekana, kwa kupigia kura ikishindikana – ziweweke punje sita (6) za mahindi karibu na alama ya chanzo cha tatizo ambalo wanafikiri linachangia zaidi kwenye tatizo. Kisha, waweke punje tano (5) karibu na alama ya chanzo ambacho kinachangia kwa kufuatia kile cha kwanza, nne (4) kwa chanzo

kinachoshika nafasi ya tatu katika kuchangia, tatu (3) kile kinachofuatia, na kuendelea.

- iv. Omba upewe maelezo – ya kwa nini baadhi ya viini vya tatizo vinapewa nafasi ya juu sana ya umuhimu na yaandike maelezo hayo.

Hatua ya 5 –Baini viini vya vyanzo ambavyo vyote ni muhimu na vinavyoweza kubadilishwa.

- i. Hakikisha kwamba kuna kadi au alama kwa ajili ya viini vya vyanzo vilivyobainishwa kama “vya muhimu zaidi” katika zoezi hilo hapo juu.
- ii. Waombe washiriki kupanga upya alama kwa ajili ya viini vya vyanzo “vilivyo muhimu zaidi” kwa utaratibu wa “kubadilishika” kutoka vinavyoweza kubadilishika zaidi hadi ambavyo ni vigumu kubadilishika.
- iii. Gawa viini vya vyanzo hivyo katika nusu na makundi mawili: vinavyobadilishika zaidi na vilivyo vigumu kubadilishika.
- iv. Pendekeza kwamba vile vya kundi la “vinavyobadilishika zaidi” viwe ndiyo kiini cha uchukuaji hatua.

Kielelezo cha Mti wa Tatizo

Matawi: Matokeo



Shina: Kiini cha tatizo

Mizizi: Vyanzo

Zana ya 2: Kuelewa Mapana ya Mgogoro

Huu ni mchakato wa kimpangilio ambao mgogoro unachambuliwa kwa kina ili kuwasaidia wasuluhishi na wanaohusika na mgogoro kuelewa vyanzo vyake na kusaidia uwezekano wa kuupunguza, usimamizi au kupata suluhisho. Ramani ya mgogoro inaweka mkazo katika wanaohusika na mwingiliano wao wa kiuhusiano. Ni zana muhimu katika kuchambua mgogoro.

Sura ya mgogoro ni sawasawa na ramani ya kijiografia ambayo inarahisisha mtiririko wa sura ya nchi kiasi cha kuweza kuwekwa kwa muhtasari katika ukurasa mmoja; ramani ya mgogoro huweka mgogoro katika namna inayoeleweka kwa urahisi, na kusaidia kupata picha yake:

- Wanaohusika na “nguvu” yao, ushawishi wao katika mgogoro,
- Uhusiano wao wenyewe kwa wenyewe, na
- Ujumbe au masuala yaliyo katika mgogoro huo.

Ramani ya mgogoro inawakilisha mitazamo maalumu (ya mtu au ya ramani ya kundi), hali fulani maalumu (haipaswi kuwa ngumu sana!), katika wakati fulani maalumu, sawa sawa na picha.

Maelekezo ya Hatua kwa Hatua:

- i. Amua juu ya mgogoro unaotaka kuchambua; weka mipaka ya mfumo wa mgogoro.
- ii. Unda vikundi vya watu wawili au zaidi. Mtu anaweza kutengeneza ramani yake ya mgogoro wake mwenyewe, lakini ni vema iwe kwenye vikundi. Kama kuna watu katika kundi ambao hawajui chochote kuhusu mgogoro, wanaweza kusaidia kwa kuuliza maswali ya ufafanuzi, mtu anayehusika na mgogoro anaweza kuzungumza nao na kujaribu mawazo yaliyopo.
- iii. Chukua kipande kikubwa cha karatasi na wachore wanaohusika katika maduara kwenye karatasi hiyo, au kwenye kadi ambazo zinaweza kubandikwa kwenye karatasi, ukubwa wa duara unawakilisha ‘nguvu’ ya wanaohusika.

- iv. Usisahau kujiweka kama mmoja wa wanaohusika katika ukurasa huo, endapo wewe au taasisi yako inahusika. Onyesha watu wa pande nyingine kama nusu duara.
- v. Chora mistari (*tazama alama hapo chini*) kati ya maduara yanayowakilisha uhusiano kati ya wanaohusika.
- vi. Katika miraba, au juu ya ramani, orodhesha ujumbe mkuu. Kwa taarifa za ndani zaidi kwa kila anayehusika, tumia Zana ya Ramani ya Mahitaji-Mashaka.
- vii. Usisahau kuongeza kichwa cha habari na tarehe kwenye ramani hiyo ya mgogoro, na kama sio siri, basi pia jina au taasisi ya mtu anayetengeneza ramani hiyo.

Alama Zinazoweza Kutumika katika Kutengeneza Ramani ya Mgogoro

- Duara: pande zinazohusika katika mgogoro. Ukubwa wa duara unaonyesha nguvu ya upande fulani wa mgogoro katika mgogoro. Jina linaweza kuandikwa ndani ya duara.
- Mstari wa ulionyooka: uhusiano wa karibu
- == Mistari miwili: Uhusiano mzuri sana, ushirika
- Mstari wa nukta: uhusiano dhaifu, usio rasmi au wa kuja na kuondoka.
- Mshale = Mwelekeo wa kudumu wa nguvu ya kuathiri au shughuli.
- ≈ Mstari uliopindapinda mgongano, mgogoro. Alama za radi zinaweza kuongezwa ili kuonyesha matukio motomoto.

Zana ya 3: Modeli ya Kitunguu

Modeli ya kitunguu imejengwa kwenye dhana kuwa matabaka ya mgogoro yako kama ya kitunguu: kuna masuala mengi ya kuzingatia, lakini yale tu yaliyo juu ndiyo yanayoonekana, ni mpaka tuanze kumenya matabaka hayo ndipo tutaona kilicho ndani. Modeli inaruhusu *welewa mzuri wa misimamo ya pande zilizo kwenye mgogoro, maslahi na mahitaji yao ya dhati.*

Inatusaidia kutofautisha yale ambayo pande mbalimbali zinasema ndivyo wanavyovitaka, vile ambavyo kweli wanavitaka na kile wanachokitaka.


Modeli ya kitunguu inaweza kutumika kama sehemu ya uchambuzi ili kuelewa yaliyomo kwenye hali ya mgogoro, lakini pia katika kuandaa uwezeshaji wa mazungumzo kati ya makundi yaliyo katika mgogoro, kama sehemu ya mapatano au mchakato wenyewe wa upatanishi – hata baada ya mchakato wa ujenzi upya wa jamii baada ya mgogoro.

Inaweza kusaidia kwa wale wanaohusika katika mazungumzo, ili kupata mapatano ya mafanikio, kuelewa kikamilifu mahitaji ya kila upande. Kabla ya kuingia kwenye mapatano, inafaa si tu kuelewa maslahi ya wengine vizuri, misimamo na mahitaji yao, bali pia kufafanua yale ya kwetu na kuyatilia maanani katika kipindi chote cha mchakato. Lengo ni kuchukua uchambuzi wa kitunguu kwa kila upande unaohusika, ukiwemo ule wa kwako.

Modeli ya kitunguu pia inaweza kuleta ung'amuzi katika migogoro ya muda mrefu; kiasi cha kuleta matumaini mapya, kwani aina hizi za migogoro mara nyingi huonekana kutokana na kufichwa au kupotoshwa kwa mahitaji ya kweli na kufanya iwe vigumu kuufuatilia mgogoro. Mahitaji haya yanaweza kubainishwa zaidi kwa kumenya matabaka ya juu ya mgogoro.

{Position = msimamo, interest = maslahi, needs = mahitaji}

MSIMAMO:	<i>Kile tunachosema kuwa ndicho tukitakacho</i>
MASLAHI:	<i>Kile ambacho ndiyo kweli tunataka</i>
MAHITAJI:	<i>Kile ambacho ni lazima tukipate</i>



Modeli ya kitunguu inawakilisha matabaka kwenye kitunguu. Tabaka la nje la kitunguu linawakilisha misimamo ambayo inaonekana kwa kila mmoja. Chini ya misimamo hii kuna maslahi (yale tuyatakayo) ambayo yanawakilisha wanayotaka watu kupata katika hali ya mgogoro.

Katika kiini cha kitunguu kuna mahitaji (yale ambayo ni lazima kupata), ambayo yanaweza kukamilishwa ili kwamba pande zilizo katika mgogoro ziridhishwe na matokeo. Wakati kunaweza kufanyika mapatano kuhusu maslahi, hili haliwezekani katika mahitaji. Ingawa inaweza kuwa vigumu kuweka misukumo mingine kando, ni muhimu kwa pande zilizo katika mgogoro kuelewa mahitaji yao na ya upande mwingine ili kupata matokeo yanayojenga na yanayoridhisha.

Vifaa Vinavyohitajika

- i. Karatasi
- ii. Penseli za rangi

Masuala ya Kukumbuka:

Wakati wa kuchambua maslahi, ni muhimu tukumbuke kwamba:

- i. Watu wote waliopo wana maslahi na mahitaji ambayo ni muhimu na sahihi kwao.
- ii. Suluhu kwa tatizo haina budi kukidhi maslahi ya wengi zaidi miongoni mwa waliopo.
- iii. Daima kuna zaidi ya suluhu moja inayoweza kukubalika katika tatizo hilo.
- iv. Mgogoro wowote unahusisha maslahi yanayoshindana, na hata yanayogongana.

Mchakato

Kundi litakutana kwa muda wa dakika 40 (kutegemeana na urefu wa majadiliano)

Hatua za Kufuata:

- i. Kwa msaada wa mwezeshaji, kundi liorodheshe wahusika wanaofaa ambao wanaweza, kwa kiasi kikubwa kuleta ushawishi katika mgogoro, au walio katika hatari zaidi katika mgogoro. (Orodha ya wanaohusika itofautishe kati ya ngazi ya jamii,

mkoa na taifa, na izingatie makundi mengine, ambayo yana ushirika na pande au ambayo yanaweza kuwaathiri).

- ii. Kisha mwezeshaji anawagawa washiriki katika makundi na kuomba kila kikundi kuchaugua msimamo.
- iii. Mwezeshaji anakiomba kila kikundi kuchora Modeli yao ya Kitunguu na kukiandikia misimamo, maslahi na mahitaji yao (kwa mitazamo yao).
- iv. Kila kikundi kionyeshe modeli zao na kuwashirikisha wengine matokeo yao. Kwa msaada wa mwezeshaji, jaribu kubaini kipengele chochote ambacho kinaweza kuonekana katika makundi tofauti, na vilevile kipengele ambacho kinaweza kufanyiwa mapatano.
- v. Baada ya hapo, zoezi la kutoa mrejesho litalenga kupata kiini cha tatizo ambacho kimo ndani ya maslahi yanayoonekana kutoendana na mahitaji kuliko misimamo kama ilivyo.

Kwa mfano

Migogoro mingi ya kijamii inayoonekana kama kwamba ni ya kikabila mara nyingi ni migogoro kuhusu rasilimali, kama vile migogoro ya ardhi.

Pande zinazohusika na mgogoro wa aina hii kwa kawaida huonyesha misimamo yao kama wamiliki wa ardhi katika mgogoro. Hata hivyo, endapo pande zitabaini maslahi na mahitaji yao zaidi ya misimamo waliyoeleza, kuna uwezekano wakuweza kugundua kwamba katika kiini cha tatizo, pande zote zinashiriki maslahi ya pamoja ya ardhi, na njia za kupatanisha maslahi zinaweza kufanyiwa mapatano.

Moja ya maslahi yaliyojificha yanaweza kuwa mahitaji ya kupata na kutumia ardhi kwa ajili ya manufaa ya jamii pana zaidi. Zingatia kwamba si rahisi daima kutofautisha kati ya maslahi na mahitaji. Mara nyingine ni kitu kilekile.

Zana ya 4: Modeli ya Mlima wa Barafu

Mlima wa Barafu ni zana ya kielelezo ambacho kinatofautisha misimamo ambayo kwa juu (kile tunachokiona) kama kila upande katika mgogoro unavyodai dhidi ya maslahi na mahitaji yaliyoko (yaliyojificha).

Mara nyingi ni rahisi kupatana kuhusu maslahi kuliko misimamo halisi, kwani haya mara nyingi kuna namna mbalimbali za kuyakidhi. Modeli hii inaweza kutumiwa ili kuchambua pande za tatizo zisizoonekana - na uhusiano wao na pande zinazoonekana.

Mlima wa Barafu unaowakilisha vyanzo vya nje (vinavyoonekana) na vile vya ndani (visivyooonekana) katika mgogoro. Kama ilivyo kwa mlima barafu, vyanzo vile vya kina na hatari zaidi huenda vikawa havionekani. Ili kupunguza mgogoro, ni muhimu kuelewa mipangilio na vyanzo vilivyo chini kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo hiki hapa chini.



{Position= msimamo, interest= maslahi, needs = mahitaji}

Modeli ya mlima wa barafu inatumika kuonyesha kwamba huenda ni sehemu ndogo tu ya mgogoro ndiyo inayoonekana kwa juu. Sita ya saba ya mlima wa barafu huwa chini ya maji na haionekani – wakati wa kuchunguza ukubwa na tabia ya mlima huo wa barafu kwa wakati mmoja.

Mara nyingi modeli hii hutumika kuonyesha kwamba ni sehemu tu ya matukio na misukumo ndiyo huonekana. Upane mwingine pia unahitaji kushughulikiwa.

Mara nyingi migogoro hutokea katika ngazi mbili kwa wakati mmoja: katika ngazi ya kuonekana na ile ya kisaikolojia. Kutambua ngazi zote mbili, kujua nguvu yao ya kubadilishana na kujenga uwezo wa kuzichunguza kila moja peke yake ni muhimu.

Ngazi ya kuonekana (*Misimamo*): 'lengo' la ncha ya mlima barafu limeundwa na mada maalumu, tabia zinazoweza kuchunguzwa na taarifa za kweli.

Ngazi ya kisaikolojia (*Maslaha na mahitaji*): hofu, ukosefu wa usalama, matamano, hisia, miiko na mengine hayawezi kuonekana mara moja, lakini yapo kwa msingi wa upana wake. Mara nyingi huwa hayazungumzwi na huwa na athari zilizojificha.

Ngazi ya kisaikolojia mara nyingi hutawala matukio. Kadiri mgogoro unayoongezeka makali, ndivyo ngazi hiyo inavyozidi kuonekana ya muhimu. Kwa hiyo, kutambua na kuelewa misukumo ya ndani ya ngazi ya chini/kisaikolojia inawakilisha hatua muhimu katika kuelewa mgogoro kiukamilifu. Kuinua ngazi ya kisaikolojia hadi katika ngazi ya ufahamu na kuondoa misukumo kuna maana ya kuweka lengo halisi la mgogoro katika uwanda wa kuchunguzwa na kulifanya liweze kuzungumzika.

Zana ya 5: Pembetatu za Mgogoro

Pembe tatu za mgogoro huchambua vipengele vya msingi vya hali ya mgogoro kwa kuviweka katika uhusiano wa pembetatu, ambapo kila kipengele kinaathiri na kuathiriwa na vingine. Inasaidia kuchambua vigezo vinavyohusiana na mitizamo, tabia na muktadha kwa kila moja ya pande zinazohusika.


Modeli hii inaeleza kwamba migogoro ina vijenzi vya kimuundo vitatu (3), vyenye uhusiano wa ndani kwa pamoja kwa namna isiyoelezeka kirahisi. Vijenzi hivyo ni:

1. Mitazamo na dhana za pande zilizo katika mgogoro.
2. Tabia za wale wanaohusika na mgogoro huo.
3. Hali ya mgogoro au muktadha.

Kwa hiyo, mgogoro unaweza kutazamwa kama pembetatu yenye mitazamo (A), tabia/mwenendo (B) na muktadha (C), katika mihimili yake.

Pembetatu za Mgogoro zinaweza kutumika kama zana ya kuchambua mgogoro na mchakato wa misukumo ambamo kwamo miundo/muktadha, mitazamo na tabia hubadilika mara nyingi na kuathiriana. Zaidi ya hayo, kwa kuwa Mgogoro wa Pande Tatu unalenga katika dhana za kila upande peke yake, ni zana inayopendekezwa sana katika kuchambua migogoro inayohusisha pande nyingi.

Pembetatu ya mgogoro ni zana inayochambua vipengele vya msingi vya hali ya mgogoro kwa kuviweka katika uhusiano wa kipembetatu, ambapo kila kipengele kinaathiri na kuathiriwa na vinginevyo. Kinawakilishwa katika muundo wa pembetatu. Ni kama inavyoonyeshwa hapa chini: (*Behavior* = Tabia; *Attitudes* = Mitizamo; *Context* = Muktadha)



Mitizamo ina maana ya hali ya kisaikolojia ya watu wanaohusika katika hali ya mgogoro. Hii ni pamoja na dhana za pande na kukosa kuona mitizamo ya pande nyingine na hata miongoni mwao, ambavyo huenda vikawa hasi, kwani pande zinazopingana huwa na kawaida ya kujenga dhana potofu dhidi ya wenzao. Hizi ni pamoja na hisia na imani, na ambazo mara nyingi zinaathiriwa na mihemko kama vile woga, kutoaminiana, kutojali, hasira na chuki.

Mara nyingine, mitazamo inaweza kuchukuliwa kama chanzo cha mgogoro, au kichochezi cha hali za mgogoro na tabia ya mgogoro. Hofu, kupitisha hukumu au kudhania kunaweza kusababisha vuguru au tabia nyingine ya kimgogoro kama mwitikio.

Tabia/mwenendo ina maana ya tabia halisi ya pande zinazopingana kutokana na malengo yao (ya kweli au ya kufikirika) yasiyoendana, na mara nyingi kutoka katika jitihada zao za kufikia malengo hayo. Haya ni matendo yanayofanywa na upande mmoja kwa lengo la kuathiri upande unaopingana nao, kwa dhamira ya kuushinikiza upande huo kuacha au kurekebisha malengo yao. Kimsingi hii inaweza kutokea katika miundo mikuu miwili: vurugu, kama vile uharibifu wa vitu, vitisho, kulazimisha na maangamizo; au pasipo vurugu, kama vile kwa njia ya ushawishi.

Muktadha una maana ya msingi wa hali ya mgogoro, ikiwemo “malengo yasiyoendana” ya kweli au ya kudhania kati ya pande zilizo katika mgogoro. Hii inaweza kutokana na “mingongano” inayofanuliwa na pande zinazohusika, maslahi yao, au moja kwa moja kutoka katika muundo wa jamii yenyewe – kisiasa, kiuchumi au mfumo wa kijamii, michakato na taasisi.

Pembetatu ya mgogoro inaweza kutumika:

- i. Mwanzoni katika mchakato, kupata ung’amuzi juu ya yale yanayozichochea pande tofauti.

- ii. Baadaye, kubaini ni masuala yapi yanaweza kushughulikiwa kupitia uingiliaji kati.
- iii. Wakati wowote, kuonyesha namna mabadiliko katika suala moja yanavyoathiri jingine.

Zana ya 6: Zana ya Pande 4


Zana ya pande 4- ni toleo lililorahisishwa la Zana ya Pande 10 - ya uchambuzi wa mgogoro. Ili kuchambua hali ya mgogoro, zana ya pande nne ni duara lililogawanywa katika sehemu nne. Linatumika kutoka kushoto kwenda kulia, sawasawa na mishale ya saa inavyotembea. Upande (robo) wa kwanza unabaini tatizo.

Upande wa pili unaakisi vihamasishi au vyanzo, wa tatu ni kuhusu suluhisho na wa nne ni hatua madhubuti. Malengo ya matumizi ya dhana hii ni kufikia uchambuzi kamili wa mgogoro na kupata suluhisho sahihi, na pia kuleta mpango wa hatua za kuchukua ili kusimamia amani katika mgogoro kama inavyoonyeshwa chini.

Zana ya 7: Uchambuzi wa Nguvu ya Uwandani

Uchambuzi wa nguvu ya uwandani ni mbinu inayoweza kusaidia jamii kuelewa na kimsingi kubaini nguvu mbalimbali zinazojenga mgogoro au kuzuia ufikiwaji wa amani endelevu kwa upande mmoja na nguvu zinazofanya kazi ili kufikia amani endelevu kwa upande mwingine katika muktadha unaohusika.

Inaonyesha nguvu zote mbili za kukubali na kupinga, na kufanya kazi kwa dhana ya kwamba mgogoro unaweza kutokana na nguvu za kupinga, na kwamba unaweza kutumia baadhi ya nguvu za kukubali ili kuleta amani endelevu. Mbinu hii inaweza kutumiwa na mtu mmoja tu,



lakini ina ufanisi zaidi pale inapotumika na wale walio katika pande zenye mgogoro ambao wana malengo bayana na njia za kuikamilisha.

Hatua zifuatazo zinaweza kusaidia kwa kutumia uchambuzi wa nguvu:

- i. Anza kwa kuchora mishale iliyolala ikilenga mraba (unapofanyia kazi kuleta amani endelevu);
- ii. Andika muhtasari mfupi juu ya malengo ya kazi yako katika mraba huu. Hii itatoa kiini cha kubaini nguvu zinazounga mkono na za ukinzani.
- iii. Chora mraba mwingine juu ya mshale wa katikati. Orodhesha nguvu zote zinazoweza ambazo pengine zinakuzuia kufikia malengo yako ya kazi hapa.

- iv. Chora mraba kama huo ukibeba nguvu zote zinazoweza kuunga mkono, chini ya mshale. Chora mraba wa nguvu wa mwisho.

Zana ya 8: Mstari wa Muda

Mgogoro wowote una mtiririko wa matukio. Haya ni matukio yanayosababisha mivutano na dhana potofu, na hatimaye kusababisha mgogoro wenye vurugu. Ni lazima kuchambua matukio yote haya katika mpangilio wa yalitokea ili kuwezesha pande zinazohusika kuelezea namna wanavyoelewa/wanavyoishi. Huu ni uwasilishaji wa matukio kwa mfuatano jambo linalofanya iwezekane kuelewa mitazamo ya watu wanaohusika kama inavyoonyeshwa hapa chini:



MANUFAA YA ZANA HII:

- Ni zana rahisi.
- Inafikisha katika uchambuzi wa kina wa mgogoro/tatizo.
- Inaruhusu kubaini kwa vyanzo vinavyoweza vya tatizo.
- Inatoa uwezekano mbalimbali wa kupata suluhu inayopokelewa vema.
- Inawezesha kuanzishwa kwa Mpango wa Kuchukua Hatua wenye hatua. maalumu za kuingilia kati ili kutekeleza suluhu kwa vitendo.

UDHAIFU WA ZANA:

- Mchakato unahitaji muda wa kutosha.
- Kama kuna kosa katika kubaini tatizo au chanzo, basi ni rahisi kupata mpango kazi usio sahihi.
- Kwa migogoro mikubwa huenda itafaa zaidi kutumia Zana ya pande 10 badala ya Zana iliyorahisishwa ya pande 4.

Zana ya 8: Mstari wa Muda



Mchoro/Kielelezo—katika mtindo wa mfuatano wa matukio—matukio yaliyosababisha kulimbikizwa kwa mivutano kadiri muda unavyopita.

(Source Conflict=chanzo cha mgogoro; Event1=Tukio la 1; Etc=N.k.; Trigger = Kisababishi; Conflict = Mgogoro; Present = Muda uliopo)

MAMBO CHANYA YA ZANA:

- Husaidia kuelewa mitazamo ya pande zinazohusika:
 1. Matukio tofauti yanayokumbukwa na kila kundi ni muhimu katika kupata uelewa kamili wa mgogoro
 2. Husaidia kujua mitazamo ya upande mwingine.
 3. Huunda na kuimarisha welewa wa pamoja wa muhtadha.
- Inaruhusu pande zinazohusika na wapatanishi kuelewa historia ya mgogoro.

UDHAIFU WA ZANA:

- Taarifa zinabaki katika ngazi ya mitazamo ya pande zinazohusika.
- Haitoi vyanzo au suluhu (ni mitazamo tu).
- Haina budi kuunganishwa na matumizi ya zana nyingine.

6.7 Kutengeneza Dira ya Jamii na Mapatano ya Amani

- i. Mara tatizo linapokuwa limeshachambuliwa kikamilifu (kwa kutumia zana yoyote ya uchambuzi wa migogoro) ni rahisi kuanza kubaini suluhisho la kiini cha tatizo kilichobainishwa kupitia mikutano ya mapatano.
- ii. Mikutano hiyo inakusudiwa kuwasaidia wanajamii kuibua mwafaka katika dira ya pamoja wanayoitaka au wanayolenga kuifikia ya “jamii yenye amani” na namna gani kwa pamoja wanachangia katika kuijenga jamii hiyo wanayotamani kuifikia.
- iii. Vipengele vya dira hii ya pamoja havina budi kunyumbulishwa. Mifano inaweza kuwa pamoja na: ulinzi wa jamii, ushiriki motomoto katika uamuzi wa jamii kitaifa ambao unaihusu jamii; kupata shughuli zinazozalisha mali, ajira kwa vijana, kugawa upya ardhi na rasilimali, usalama na ulinzi wa wanajamii, kwa kutaja michache tu.
- iv. Hatua inayofuata ni kufanya kazi kwa kurudi nyuma kutokea kwenye dira hii hadi wakati uliopo. Je, wanajamii wanapaswa kufanya nini ili kuhakikisha vipengele vya dira hii vinafikiwa? Wanajamii wanaweza kuandaa majibu yao mbalimbali kwa baadhi ya masuala yanayochukuliwa kuwa ya ngazi ya kitaifa yanayoathiri jamii. Kwa mfano, wanaweza kubaini ukosefu wa usawa katika kupata ardhi kama suala la kitaifa ambalo linaweza kushughulikiwa kupitia miundo ya ngazi ya jamii. Wao, wanajamii na mamlaka wanaweza kukubaliana namna ya kupata ardhi huku ugawaji wake ukisimamiwa kwa kuzingatia usawa.
- v. Kujenga taswira ya baadaye kwa kutumia dira ya jamii ili kupata ahadi wazi na wajibu kwa upande wa makundi tofauti yanayowajibika katika kufikia dira hiyo ya pamoja.
- vi. Njia kama hiyo inaweza kuwawezesha wanajamii kushughulika na mambo halisi magumu ambayo hawako tayari kuyakabili kwa kupendelea zaidi hatima ambayo wanaweza kuchangia ili kuiunda na kwa hiyo

kupokea hali halisi ya mivutano inayoibuka. Itambuliwe kwamba huenda baadhi ya wanajamii wasiwe tayari kuweka ahadi kwa sasa ikwa hawana uhakika kwamba wanajamii wengine watakuwa tayari kuweka ahadi kama hiyo. Mwezeshaji anapaswa kutambua hisia zilizopo na anashauriwa kutafuta mikutano binafsi ya ndani pamoja na vikundi ikiwa njia hii itasaidia wanajamii kujisikia huru kueleza hisia zao. Mara baada ya mwafaka kupatikana wakati wa mikutano hiyo ya ndani, mwezeshaji anapaswa kulileta kundi zima pamoja katika kikao cha hadhara ili kuthibitisha mwafaka huo uliokwishapatikana katika vikao tofauti vya ndani.

Zingatia: Mapatano ya amani ni mchakato changamani, ambao unategemea sana njia zisizo za kutumia nguvu na zilizo jumuishi. Wazungumzaji wakuu hawana budi kutambua umuhimu wa kutafuta suluhu isiyo ya kutumia nguvu katika hali ya mivutano.

Kupendeleza Suluhu katika Masuala/Kiini cha Mgogoro Kilichobainishwa

- i. Hatua hii, washiriki katika mchakato wa mazungumzo ya amani wanatoa mapendekezo ili kushughulikia masuala yaliyobainishwa au kiini cha tatizo kinachoathiri jamii. Kila upande unaandaa mapendekezo ya suluhisho kupitia vikundi vikundi.
- ii. Baadaye, kikao cha pamoja kinaitishwa ambapo kila kikundi kinawasilisha pendekezo lao la suluhu. Masuluhisho ambayo yanaonekana kukubaliwa na pande zote katika mazungumzo ya amani ndiyo yanapitishwa. Masuluhisho yasiyoafikiwa yanarudishwa katika meza ya majadiliano, au vikundi vidogo vyenye wanajamii kutoka pande zote katika mazungumzo vijaribu kutafuta maelewano au mapendekezo ya pamoja yasuluhu.
- iii. Kwa suluhu zilizokubalika, kila kikundi kinapendelea ahadi zake ili baada ya hapo kichangie katika utekelezaji kwa vitendo. Kwa

mara nyingine, ahadi hizi zinajadiliwa kati ya pande ambazo pamoja zitafanya tathmini ya kufaa kwake ili kuhaikisha masuluhisho ni yenye kuleta mwafaka. Baadhi ya masuluhisho ya mwafaka, kuna yale ambayo yanafikiwa kwa urahisi na mengine ambayo ni vigumu kuyafikia lakini ni muhimu kwa amani.

- iv. Baada ya mwafaka katika masuluhisho, ni muhimu kwa jamii kuamua muundo utakaochukuliwa na matokeo ya mazungumzo. Matokeo ya mazungumzo yanaweza kuchukua miundo tofauti kutegemeana na muktadha wa kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni na tatizo lililopo. Katika mazingira ya kiutamaduni, kwa mfano, ahadi ya kila upande katika mazungumzo ya suluhisho zinaweza kutolewa kwa mdomo wakati katika mengine, kutekeleza mila fulani huenda kukahitajika ili kuonyesha ahadi ya pande zilizokubaliana. Kwa mfano jamii zinaweza kubadilishana madume ya ng'ombe ili kumaanisha mwisho wa mgogoro na kumbukumbu ya daima ya yale yaliyokubaliwa.
- v. Kwa tukio la vurugu za Unguja (Zanzibar) wakati wa Machafuko ya UAMSHO mwaka 2012 kati ya vijana na polisi¹⁵ kama ilivyoelezwa pale mwanzoni, matokeo ya mazungumzo ya wazi na harakati nyingine yalileta kubadilika kwa mitizamo na kuongezeka kwa ushirikiano na kuaminiana kati ya serikali (polisi) na jamii, hasa vijana, ushirikiano na uhusiano huu uliimarika kati ya Polisi na Wanajamii. Hii haikuandikwa popote au katika mkataba wa kijamii unaofunga pande zinazohusika.
- vi. Hata hivyo, wasiwasi mkubwa ni kuhusu uhalali wa ahadi yoyote ya mdomo, ambayo inaweza kukanwa wakati wowote. Ndio maana mara nyingi, ni muhimu kwa pande zinazohusika kuwekeana saina makubalino kupitia wawakilishi wa wadau wote, jambo ambalo CDPS inalielezea kama mkataba wa jamii; kuonyesha ahadi kwa matokeo ya makubaliano.

HATUA YA 7: MIKATABA YA KIJAMII NA YALIYOMO

Sehemu ifuatayo inatoa miongozo ya jinsi ya kufafanua yaliyomo katika mkataba wa kijamii (7.1), utiwaji saina wake na wadau wote (7.2) ili kuonyesha utayari wao wa kuutii (7.3) ikiwemo kuanzishwa kwa kamati za amani (7.4) na mifumo mingine kwa ufuatiliaji bora zaidi (7.5).

7.1 Ufafanuzi wa Mikataba ya Kijamii na yaliyo Ndani yake

- i. Kutokana na mazungumzo ya jamii, mikataba ya kijamii inatungwa ili kuhakikisha kwamba mtu mmojammoja wanaweka ahadi ya kuendeleza mazungumzo ili kuzuia migogoro na kuleta mabadiliko, mshikamano na ushirikiano wa kijamii.
- ii. Mikataba ya kijamii huandaliwa kwa msingi wa matatizo makuu yaliyobainishwa na suluhu wakati wa mikutano ya mazungumzo ya jamii. Mikataba ya jamii inatungwa katika muundo wa ahadi na makundi mbalimbali ya kijamii miongoni mwa pande zinazohusika katika mazungumzo ya amani.
- iii. Kwa mikataba hii maalumu, wanaweka ahadi ya kusahau kumbukumbu na vitendo vyote vya kuumiza vilivyopita na kukubali kuishi pamoja kwa amani. Wanaweka ahadi ya kumaliza kutoaminiana na chuki na kuzuia vishawishi vya watu wa nje katika kutengeneza migawanyiko miongoni mwa wanajamii wa jumuiya inayohusika.
- iv. Ahadi hizi zinaunda msingi wa kuanzisha upya jitihada za kutafuta riziki na miradi ya uzalishaji, kujenga upya makazi na miundombinu, kurekebisha uhusiano wa kijamii, na pale inapowezekana kufungua njia ya kuleta amani na uwajibikaji.

¹⁵ Tazama kipengele cha 2.1

7.2 Kutiwa saine kwa mkataba ya kijamii kwa ajili ya kuishi pamoja kwa amani

- i. Kutiwa saine kwa mkataba wa kijamii ili kuishi pamoja kwa amani kunafanyika kwa kuheshimu wanajamii ambao ndio viongozi na wenye ushawishi katika uwanja wa amani. Hawa wanaweza kuwa viongozi wa kimila au wa dini. Lililo muhimu ni kwamba, wanapaswa kuwa watu waliochaguliwa na jamii zao.
- ii. Mchakato wa kutia saine kwa ujumla hufanyika mbele ya washiriki wote katika mazungumzo ya amani na kushuhudiwa na viongozi wa kiserikali. Pale inapofaa, mchakato unaweza kuambatana na sherehe maridadi na yenye shamrashamra nyingi na kuelezea umoja, furaha na amani. Mifumo ya sherehe maalumu inaweza kupata msingi wake katika muktadha wa kijamii na kiutamaduni. Msisitizo unapaswa kuwekwa katika vielelezo vya pamoja na nia thabiti katika amani ya kijamii.
- iii. Wanajamii wenyewe wanapaswa kutayarisha maandalizi ya tukio hilo, kwa kutumia miongozo na msaada wa amani katika watu vinara na wakala za utekelezaji.

7.3 Ahadi ya Kila Raia

Watu wote waliopo wanahimizwa kuweka ahadi zao za kuheshimu masuluhisho yaliyofikiwa katika mkataba uliotiwa saine wa kijamii. Kila raia/mtu anaweza ahadi ya kuwa mtu wa amani akichukulia kwa uzito mahitaji na masibu ya raia wenzake, na kutenda kile ambacho yeye anaweza kuhakikisha kuwa hakuna madhara na amani inadumishwa. Pande zinazohusika kwa pamoja zinaanzisha miradi kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi zilizowekwa kadiri ya mkataba wa amani uliotiwa saine.

7.4 Kuunda Kamati za Amani za Jamii

- i. Kamati za amani zenye wajumbe mchanganyiko katika jamii zinaundwa kidemokrasia na wajumbe wenye sifa katika jamii. Kamati zina nafasi kama kichocheo cha amani na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kijamii ili kuishi pamoja kwa amani na kwa miradi itakayofuatia ya amani.
- ii. Kwa msingi huu, wanachama wa kamati za amani wanatarajiwa kupitia mafunzo ya uongozi wa jamii ili kuimarisha uwezo wao kama wahamasishaji na watetezi wa jamii.
- iii. Kamati ya amani inapaswa kuwa na uwakilishi wa kila kundi la kijamii (wanaume, wanawake, vijana, wahamiaji, waliorejea katika jamii, walio wachache, n.k.).
- iv. Kila kamati inapaswa kuwa na walau watu 6 au zaidi, au idadi itakayokubaliwa na wote.
- v. Wajumbe wa jamii waeleze utaratibu wa uchaguzi wa wawakilishi wao katika kamati kwa namna inayokubalika kwa wote.
- vi. Wajumbe wa kamati wanachaguliwa na washiriki katika mapatano ya amani ya jamii. Sifa kuu ya kuchaguliwa ni utayari na udhati wa ujenzi wa amani na kuzuia migogoro katika jamii.
- vii. Kwa kawaida, watu wenye sifa hizo hufahamika vema katika jamii. Mara nyingi watu huwafahamu wachochezi miongoni mwao, na pia wanaume/wanawake wenye mapenzi mema na wanaohamasisha matumizi ya hoja na kulinda amani miongoni mwao.
- viii. Taasisi wezeshi inaweza kuongozwa na Hadidu za Rejea za Kamati ya Amani zilizotayarishwa na Kamati ya Uongozi ya Taifa na kurekebisha hayo ili washiriki waone inafaa kuakisi muktadha wa mahali. Hadidu za Rejea ziko katika Kiambatanishi cha 1 cha kitabu hiki cha mwongozo huu.

7.5 *Mamlaka ya Kamati ya Amani*

- i. Kamati ya amani yenye wajumbe mchanganyiko katika jamii inaweza kuwa na mamlaka haya:
- ii. Kufuatilia mkataba wa amani wa kuishi pamoja kijamii uliotiwa saini na wanajamii;
- iii. Kueneza ujumbe uliomo katika mikataba ya kijamii kwa jamii nzima;
- iv. Kusaidia kuwezesha mazingira ya kuishi pamoja kwa amani;
- v. Kuzuia au kusimamia migogoro katika ngazi ya jamii;
- vi. Kuwezesha mikutano ya kuimarisha au kurejesha amani pale inapobidi; na
- vii. Kuongoza mchakato wa uhamasihaji jamii ili kuleta utambuzi wa dira ya pamoja ya jamii yenye amani.

Kwa kutambua kwamba kuanzishwa kwa kamati ya amani ni mchakato unaosukumwa na jamii, jumuiya inaweza kutamani kuingiza masuala mengine katika majukumu ya kamati. Majukumu yaliyokubaliwa yanaingizwa katika mkataba wa amani wa kijamii.

7.6 *Mbinu za Jamii za Ufuatiliaji wa Mikataba ya Kijamii*

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba ya kijamii hufanyika kupitia wawakilishi wa pande zilizo

katika mazungumzo ya amani pamoja na wajumbe waliochaguliwa wa kamati za amani. Katika suala hili ufuatiliaji huwa na pande mbili: Usimamizi, utetezi na uchukuaji hatua katika kujenga amani kunakofanywa na kamati za amani na urudufishaji wa mapatano hayo ya amani katika ngazi ya chini.

Kamati za amani zinatarajiwa kila mara kusimamia uzingatiwaji wa mikataba ya kijamii, kushiriki katika utoaji tahadhari ya mapema, na kwa lengo hili, kufanya kazi kwa karibu na mamlaka za kiserikali ili kuzuia vurugu zozote, na kuhakikisha utekelezaji wa haki na ushirikiano wa miradi ya amani.

Kwa upande wa migogoro katika ngazi ya chini (kama vile ndani ya kaya au miongoni mwa majirani) wajumbe wa kamati za amani waandae mikutano ya mapatano ya amani katika vikundi vidogovidogo wanamoishi pamoja katika mtaa/kijiji/uwanja. Wanaweza kuchagua zaidi matukio ya migogoro ya kati ya mtu na mtu, kama vile matukio ya matumizi mabaya ya nguvu kati ya wanandoa, migogoro kati ya ndugu, n.k.

Kushughulika na vyanzo na matokeo ya migogoro na kuhamasisha ari ya ushirikiano na mshikamano kupitia miradi ya pamoja ya amani kwa lengo la kuimarisha mshikamano miongoni mwa wajumbe.

Wajumbe waliochaguliwa wa kamati za amani wanahitajika kufanya kazi kwa karibu na viongozi wanaowakilisha jamii zao mbalimbali na pia utawala wa jamii.

6. AWAMU YA 2: UENDELEWU KUPITIA MIRADI YA AMANI

Awamu hii inahusu uendeleu wa mkataba wa amani. Mwisho wa mchakato wenye mafanikio wa mazungumzo, modeli ya CDPS inapendekeza kuweka sawa hatua na mbinu zitakazoendeleza kuishi pamoja kwa amani katika jamii hasa kupitia kubuni na kutekeleza miradi ya amani kunakofanywa na jamii.

HATUA YA 8: MIRADI YA AMANI ENDELEWU

Awamu hii inahusisha kuandaa miradi ya amani ya jamii yenye lengo la kuimarisha mshikamano na ushirikiano wa kijamii; kuzuia migogoro na kuleta mabadiliko. Msingi wa kubuni na kutekeleza miradi ya amani ya jamii ni kuendelea kuhusisha katika kuimarisha mchakato wa amani kupitia miradi yenye tija kwa jamii na kuendelea kuchangia katika mshikamano wa kijamii miongoni mwa wanajamii.

Miradi ya amani inabainishwa na kufafanuliwa katika utaratibu uleule shirikishi ambao umekuwa ukitumiwa katika mikutano ya mazungumzo ya jamii. Kufuatia kuelewa kiini cha vyanzo vikuu vya mivutano na masuluhisho yaliyopendekezwa na jamii na wadau wengine wa jamii, mkutano wa jamii unaitishwa na washiriki wanagawanywa katika vikundi vidogo vidogo – vikiwemo vya wanawake na vijana na wale wanye mahitaji maalumu – kujadili maeneo yanayofaa ya utekelezaji wa baadhi ya masuluhisho yaliyopendekezwa katika muundo wa miradi ya amani endelevu.

Ili kuibuka na miradi ya amani maalumu, vyama, watu vinara katika amani wanaitwa katika mkutano na jamii ili kupitia upya vyanzo vya migogoro na masuluhisho ambayo wamependekeza wenyewe. Wakati wa kuwasaidia, wajumbe wa kamati wanapaswa kujiunga kwa pamoja ili kuweka vipaumbele vya hatua za uingiliaji kati, ambavyo vitachangia katika kuendeleza kuishi kwa pamoja. Pengine njia sahihi ingeweza kuwa:

- i. Mapitio ya pamoja ya yatokanayo na uchambuzi wa kitisho/mgogoro katika awamu zilizotangulia za Modeli ya CDSP. (Kwa hiyo, inasaidia kutunza makabrasha ya mijadala, michoro n.k. ambao ilitumika katika kila hatua ya Modeli, ili kwamba sasa haya yatumike kujikumbusha uchambuzi wa pamoja uliofanyika). Waelekeze wanajamii kugawanyika katika makundi madogo madogo – waombe kila mmoja alete suluhisho linaloweza kufanya kazi dhidi ya matatizo yaliyobainishwa. Wanavikundi wanapaswa kuwa tayari kwa mabadiliko ili kuchukua au kuonyesha mienendo mipya ya mgogoro, kama itakuwepo, na kupendekeza njia inayostahili.

Mapendekezo ya makundi tofauti yanawasilishwa katika mkutano wa pamoja na pale ambapo mwafaka umefikiwa, mapendekezo yanachukuliwa.

- ii. Baada ya kurudi katika mkutano wa pamoja, waelekeze kuwasilisha mapendekezo ya masuluhisho ya vikundi vyao na fikra za miradi.
- iii. Ili kuwezesha uwekaji vipaumbele vya miradi katika jamii, mtu anaweza kufanya yafuatayo:
 - Kama kuna miradi ishirini iliyopendekezwa, waombe wajumbe wa vikundi kuchagua walau kumi iliyo muhimu zaidi (Asilimia 50 ya jumla)
 - Kundi—kwa kutumia mwafaka—liweke kokoto kumi (10) jiriani na alama inayofuatia ya mradi ambao wanafikiri unachangia zaidi katika kutatua tatizo lililobainishwa. Kisha, weka kokoto (9) jiriani na alama ya mradi ambao unaweza kuwa wa pili katika uchangia kutatua tatizo lililobainishwa, iendelee hivyo hadi mradi ambao una sifa chache utakapofikiwa (waweke rekodi) kwa nini baadhi ya miradi imepewa nafasi ya juu kabisa na nyingine hapana. Kutakuwa na madaraja na utoaji sababu za kuchagua mradi fulani kwa makundi tofautitofauti ndani ya jamii.

Ni wajibu wa wakala wa utekelezaji kushauri wanajamii juu ya utengemao wa kiufundi na kifedha kwa miradi yao.

Wanajamii pia watafafanua njia za jamii za kutekeleza miradi ya amani, hasa ile iliyobainishwa kwa upana wa uwezo wao.

Bila kujali miradi ina ukubwa gani, bado inapaswa kuendeshwa na jamii, inapangwa, kutengenezwa na kutekelezwa katika jamii, kwa msaada wa wadau na wakala.

Miradi ya amani inaweza kuhusu elimu ya amani, mshikamano wa kisheria na hata urekebishaji wa miundo ya kijamii, harakati za kuongeza kipato, kuzuia migogoro na zile za kuleta mageuzi. Mifano hii haionyeshi miradi yote na inategemea muktadha, ni juu ya jamii kuamua kuhusu aina za miradi iliyo endelevu katika kuifikia mahitaji yao ya kuendeleza na kuimarisha kuishi kwao kwa amani.

Baada ya kuanzishwa kwa mpango kazi kwa ajili ya amani endelevu, wakala anayetekeleza anaweza kuhitaji kutoa msaada kwa makundi ya jamii na vyama kuchangisha fedha kwa ajili ya jitihada zao (pale inapokuwa lazima), au kupatana na mamlaka zinazohusika za serikali katika wizara zinazohusika au wafadhili, sekta binafsi ili kusaidia miradi ya amani ya jamii.

Kwa kutumia majukwaa yaliyopo kama vile mikusanyiko ya makanisani na misikitini, mikutano ya viongozi wa maeneo, sherehe za kimila na utamaduni (kwa kutaja tu mifano michache) ili kusambaza ujumbe wa amani hakuhitaji msaada wa kifedha bali utayari madhubuti wa mtu mwenyewe ili kuhamasiha amani na mshikamano wa kijamii katika jamii inayohusika.

Ikumbukwe kwamba wanajamii wanapaswa kutiwa moyo ili kutafuta msaada ndani ya jamii zao na kusawiri rasilimali zinazoweza kupatikana katika jamii kwa matumizi hayo. Si jitihada zote zinahitaji msaada wa kifedha ili kutekelezwa.

KIAMBATANISHO CHA 1: Hadidu za Rejea kwa Kamati za Amani za Wilaya (DPCs)

Kamati ya Uongozi ya Taifa juu ya Kujenga Amani na Kudhibiti Migogoro (NSC)

Dira

Kupata amani endelevu nchini Kenya.

Dhima

Kuanzisha uratibu, ushirikiano na uunganishaji kati ya Serikali, vyama vya kiraia na washirika wa maendeleo, kwa lengo la kupatanisha, kuimarisha na kuanzisha taasisi kwa ajili ya ujenzi wa taifa wa amani wenye tija na mikakati na mifumo ya kudhibiti migogoro, zikiwemo ushirikiano wa kikanda.

Hadidu za Rejea

- i. Kuwezesha uunganishwaji miongoni mwa wadau katika ngazi zote;
- ii. Kuimarisha uratibu kati ya Serikali, wahisani na wakala za utekelezaji katika kujenga amani, kudhibiti migogoro na jitihada za kudhibiti silaha haramu ndogondogo;
- iii. Kuhamasisha upatanishi wa njia za kujenga amani, kudhibiti migogoro na silaha haramu ndogondogo na nyepesi nchini;
- iv. Kuwa chanzo cha rejea kwa ajili ya taarifa juu ya kujenga amani, kudhibiti migogoro na shughuli za silaha ndogondogo haramu na asasi;
- v. Kubaini na kuhamasisha rasilimali za kujenga amani, kudhibiti migogoro na jitihada za kudhibiti siala ndogondogo na nyepesi haramu;
- vi. Kuhamasisha na kufanya utetezi wa amani nchini kupitia juhudi zinazotokana na jamii, ikiwemo ulinzi shirikishi wa jamii;
- vii. Kuwezesha kuanzishwa kwa mifumo ya utambuzi wa mapema wa ishara za migogoro;
- viii. Kuwezesha mazungumzo na wadau ili kuanzisha sera kamalifu ya taifa juu ya amani, kudhibiti migogoro na kujenga taifa; na
- ix. Kuanzisha kamati ndogondogo zenye wajibu maalumu. (Hadi sasa, kuna Kamati Ndogondogo tatu, yaani, Ufundi, Vyombo vya Habari na Uchambuzi wa Mgogoro).

Matokeo Yanayotarajiwa:

- i. Kusimamia na kupitia upya jitihada za kujenga amani katika ngazi zote;
- ii. Kubaini maeneo yenye uwezekano wa migogoro;
- iii. Ubainishaji wanakopatikana wadau;
- iv. Kusaidia shughuli zinazokazia masuluhisho na njia za kuzuia migogoro;
- v. Kuhamasisha vikao vya ushauri vya ngazi ya Wilaya na Mkoa (Jimbo);
- vi. Kuanzisha Muundo wa Kitaifa wa Ujenzi wa Amani;
- vii. Kujenga uwezo wa wadau wote kupitia ulinzi, ushauri na mafunzo;
- viii. Kuongoza katika uhamasishaji rasilimali kwa ajili ya amani;
- ix. Kupigania ushirikiano katika kujenga amani na kudhibiti migogoro ili iingizwe katika programu za maendeleo.

Kamati ya Amani ya Wilaya (DPC)

Wajumbe:

Wawakilishi wa jamii, DSICs, CSOs, Mamlaka za Mahali, wanawake, vijana, wenye ulemavu, sekta binafsi – wakitoka katika eneo lote la utawala la Wilaya.

Dhima na Wajibu

- i. Kuratibu, kuoanisha na kuwezesha programu za ujenzi wa amani na taifa katika Wilaya;
- ii. Kuhamasisha elimu, utamaduni wa amani na kutokuwepo na vurugu;
- iii. Kuunganisha na majukwaa/kamati na asasi nyingine za amani ili kukuza uhusiano mwema;
- iv. Kusimamia utekelezaji wa makubaliano na maazimio ya amani;
- v. Kuhamasisha mawazo ya walio wengi kwa njia makini katika kubaini migogoro katika mipango ya maendeleo ya Wilaya;
- vi. Kuunga mkono jitihada za kukomesha silaha haramu, na usalama na ulinzi (ulinzi shirikishi) katika Wilaya;
- vii. Kuhamasisha ukusanyaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa programu/shughuli mbalimbali;
- viii. Kuwezesha mafunzo na mazungumzo katika jamii;
- ix. Kuimarisha mifumo ya utambuzi wa mapema wa migogoro na namna ya kuitika;
- x. Kuhakikisha utawala wenye hekima na kuweka uwajibikaji kwa rasilimali zilizotengwa kwa ajili yake;
- xi. Kutunza kumbukumbu na taarifa za michakato ya amani na hatua za uingiliaji kati;
- xii. Kusimamia, kutathmini na kutoa taarifa za amani na programu za ujenzi wa taifa;
- xiii. Kutekeleza majukumu mengine yoyote ya lazima ili kufikia malengo ya Sera ya Taifa ya Ujenzi wa Amani na Kudhibiti Migogoro.

Jukwaa la Viongozi/Wadau wa Amani wa Jimbo/Mkoa

Wajumbe:

Linajumuisha Wakuu wa Idara, Wabunge, Wajenga Hoja, Wawakilishi wa Kamati za Amani za Wilaya, Asasi za Kidini, Vyama vya Kiraia, Asasi za Sekta Binafsi, vyama vya wafanyakazi, asasi za

vyombo vya habari, Wawakilishi wa Mamlaka za Mitaa na wakuu wa mashirika ya umma.

Dhima na Wajibu

- i. Kuwezesha na kuratibu utekelezaji wa programu za amani na ujenzi wa taifa na mikakati katika Jimbo/Mkoa;
- ii. Kusanifu na kuthibitisha mipango ya jimbo/mkoa kuhusu ujenzi wa amani na taifa;
- iii. Kuhamasisha rasilimali kwa ajili ya programu za utekelezaji;
- iv. Kuendesha usimamizi na tathmini za programu za ujenzi wa amani na taifa;
- v. Kutoa taarifa juu ya maendeleo ya programu za amani;
- vi. Kuwa jukwaa la kutoa mrejesho wa matokeo katika jimbo/mkoa.

Jukwaa la Viongozi wa Amani wa Wilaya/ Jimbo la Uchaguzi

Wajumbe:

Wakuu wa Idara, Wabunge, Wawakilishi wa DPCs, Asasi za Kidini, Vyama vya Kiraia vya Kitaifa, Asasi za Sekta Binafsi, Asasi za Vyombo vya Habari, Wawakilishi wa Serikali za Mitaa, Wakuu wa Mashirika ya Umma.

Dhima na Wajibu

- i. Kuwezesha na kuratibu utekelezaji wa programu za ujenzi wa amani na taifa na mikakati katika Wilaya/Jimbo la Uchaguzi;
- ii. Kusanifu na kuthibitisha mipango ya Wilaya/ Jimbo la Uchaguzi juu ya ujenzi wa amani na taifa;
- iii. Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa programu;
- iv. Kuendesha usimamizi, tathmini na utoaji taarifa juu ya programu za ujenzi wa amani na taifa;
- v. Kutoa taarifa ya maendeleo ya programu za amani kwa Jukwaa la Viongozi wa Jimbo/ Mkoa;
- vi. Kutumika kutoa mrejesho wa matokeo katika Wilaya/Jimbo la Uchaguzi.

Ngazi Nyingine za Chini za Miundo ya Ujenzi wa Amani na Kudhibiti Migogoro

Wajumbe:

Wajenga Hoja, Asasi za Kidini, Viongozi wa Jamii (Wanawake, Wanaume na Vijana)

Dhima na Wajibu:

- i. Kubaini na kuweka vipaumbele vya maeneo maalumu ya kufanyiwa mazungumzo;
- ii. Kubaini malengo ya mazungumzo ya kiraia;
- iii. Kuandaa muundo na programu ya mazungumzo;
- iv. Kuratibu mazungumzo ya raia;
- v. Kutoa taarifa kwa DPC juu ya programu;
- vi. Mifumo ya Kusimamia, Kutathmini na kutoa taarifa;
- vii. Kuweka kumbukumbu ya mafunzo yaliyopatikana na njia bora zilizogunduliwa;
- viii. Kuleta uongozi mkuu wa tunu na maadili.

Uundaji

Kamati za Amani ni taasisi mchanganyiko ambazo zinaunganisha nguvu ya pamoja kati ya mifumo ya kimapokeo na rasmi ya utafutaji

suluhu ya migogoro. Uundwaji wake hauna budi kujumuisha wawakilishi wa jamii wakiwemo DSICs, CSOs, Mamlaka za Jamii, wanawake, vijana, wenye ulemavu, na sekta binafsi ambao wana jukumu la kuamua vigezo vya majukumu katika wilaya. Wawakilishi wa jamii wanapaswa kuchukuliwa kutoka katika maeneo yote ya utawala katika Wilaya.

Kanuni za Uendeshaji

Ufanisi wa Kamati za Amani utahitaji kuwepo kwa kanuni fulani. Kanuni kuu ni:

- i. Kujitoa kwa ajili ya amani, kutetea kutokuwepo kwa vurugu, njia za amani za kushughulikia migogoro;
- ii. Kuheshimu utu na utakatifu wa uhai;
- iii. Kuheshimu haki za binadamu;
- iv. Kusimamia haki;
- v. Uvumilivu;
- vi. Uaminifu na uadilifu;
- vii. Usawa wenye haki kijinsia;
- viii. Ujumuishi;
- ix. Uwazi na mawasiliano yenye ufanisi;
- x. Umiliki wa jamii.

KIAMBATANISHO CHA 2: Muundo was Kamati za Dini Katika Ngazi Mbalimbali

Kamati

2.1 MUUNDO WA KAMATI ZA DINI KATIKA NGAZI MBALIMBALI

Muundo wa kamati utazingatia uwepo wa viongozi wa dini katika maeneo husika. Viongozi hawa watachaguliwa kutokana na kada na nafasi zao kulingana na eneo lengwa. Muundo huu utakuwa kama unavyoonekana hapa chilli

- Taifa
- Mkoa
- Wilaya
- Tarafa
- Kata
- Kijiji
- Mgawanyo wa majukumu utategemea ngazi husika

2.2 SIFA ZA MWANAKAMATI

- Awe ni mkazi au anahudumu katika eneo husika
- Awe ameteuliwa na ameridhiwa na viongozi wa taasisi
- mwanachama
- Awe mwenye kujua kusoma na kuandika
- Awe mpenda na mshiriki katika mambo ya mahusiano ya kidini
- Awe mfano wa kuigwa katika jarnii
- Awe mchamungu, mwenye roho ya maridhiano na maadili mema.
- Ikiwa mwanachama atapoteza moja ya sifa tajwa, taasisi mwanachama
- itawajibika kubadilisha kwa kuturna rnbadala.

2.3 UPATIKANAJI WA WANAKAMATI

Ukiachia mbali ngazi ya taifa, uwakilishi katika ngazi mbalimbali utakuwa kwa mujibu wa uanachama wa IRCPT. ill kuweza kuleta uwiano wa namba kila mwanachama atatakiwa kuleta idadi sawa. Wanachama wa IRCPT watateua

watu wawili katika ngazi husika. Namba ya juu ya jumla ya wanakamati wote itakuwa ishirini (20) na idadi ya chini itakuwa kumi. Ikiwa idadi ya wanachama wa IRCPT katika ngazi husika ni chini ya watano (5), wanachama waliopo watateua wajumbe kwa idadi sawa ambao jumla yao si chini ya watu kumi (10) na haitazidi watu ishirini (20) Mwanachama wa IRCPT anaweza kufanya mabadiliko ya mwakilishi wake katika kamati akiona ni muhimu kufanya hivyo.

2.3.1 Uundaji wa mitandao ya akinamama na vijana katika ngazi mbalimbali.

Kutakuwa na mitandao ya vijana na akina mama katika ngazi mbalimbali watakaoteuliwa na taasisi mwanachama katika eneo husika. Katika kila mtandao mwenyekiti na katibu watakuwa wawakilishi katika kamati za viongozi wa dini kwenye ngazi husika. Katika uteuzi wa viongozi wa mitandao Jili kila mtandao utatakiwa kuhakikisha kwamba nafasi za uongozi zinawakilisha dini mbalimbali.

2.4 KAZI ZA KAMATI ZA DINI KATIKA NGAZI MBALIMBALI

- Kujadili kwa kina vyanzo mbalimbali vinavyoweza kuchochea vurugu na uvunjifu wa amani katika eneo lao na kukubaliana njia bora ya utatuzi.
- Kuwa jukwaa la kuzungumzia na kujadili mambo yenye maslahi na uhusiano wa pamoja kwa ajili ya ujenzi wa amani na ustawi wa jamii.
- Kuwa mshauri na mtetezi wa wananchi juu ya masuala mtambuka yanayohusu ustawi wao na pale inapobidi kutoa matamko ya pamoja.
- Kushauri, kupanga na kutekeleza programu mbalimbali za pamoja zenye lengo la kttleta maendeleo na uwajibikaji kwa jamii.
- Kuhimiza kutambua, kuheshimu na kuvumilia dini ya kila mmoja.

- Kupinga na kupiga vita vitendo vya kikatili, unyanyasaji, unyonyaji, ubaguzi na utesaji katika jamii yetu.
- Kuhimiza, kuendeleza na kusimamia maadili mema ya kitanzania na ktnva mfano mwema wa kuigwa katika jamii yetu.
- Kuendeleza, kusaidia na kutetea ustawi wa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi katika jamii yetu.
- Kuhimiza na kusaidia walioa.thirika na majanga.
- Kushirikiana na taasisi mbalimbali za kijamii na za serikali katika kutatua matatizo yanayoikumba jamii.
- Kuendeleza tabia njema ya viongozi wa dini mbalimbali ya kutembeleana.
- Kusimamia uundwaji na utendaji wa mitandao ya vijana na wanawake wa dini mbalimbali katika ngazi hiyo.
- Pale itakapoonekana ni muhimu Kamati itasimamia uundwaji na utendaji wa kamati ndogondogo ktilingana na mallitaji.
- Kuunga mkono na kusaidia jitihada zenye lengo la kuendeleza amani, utulivu, umoja na kuishi pamoja kwa amani nchini Tanzania na jumuiya za kimataifa.
- Kuanzisha na kuendesha miradi inayoweza kuendeshwa pamoja na isiyokuwa na masharti yanayokwaza imani za wanachama wengine bila kujali idadi yao katika eneo husika. Miradi hiyo inaweza kuwa ya kilimo, ufugaji, biashara, kuweka na kukopa n.k
- Kamati itakuwa na uwezo wa kutafuta fedha na rasilimali nyingine kutoka vyanzo mbalimbali vya halali ill kuendesha shughuli za kamati kama itakavyokubaliwa na kamati katika ngazi husika.
- Kamati inaweza kutafuta na au kuteua mratibu kwa ajili ya shughuli katika ngazi husika. Mratibu huyo atapangiwa majukumu na kuwajibika moja kwa moja kwa kamati iliyomteua na kutoa taarifa kama

atakavyoelekezwa na kamati.

- Kufanya jambo lolote ambalo litasaidia kufikia lengo kuu la kujenga amani, mahusiano, ushirikiano na maendeleo.
-

2.5 TUNU, MILKO NA MIPAKA.

2.5.1 Tunu

- Kutambua na kuheshimu imani ya kila mwanachama wa IRCPT
- Kufanya kazi kwa uwazi, kuaminiana na kuheshimiana
- Kutambua na kuthamini jitihada na michango ya wadau wengine wenye lengo la kuimarisha amani, maendeleo na ustawi wa jamii
- Kutambua na kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo serikali katika jitihada hizo za kuimarisha amani, kuleta maendeleo na kukuza ustawi wa jamii.

2.5.2 Milko Na Mipaka

- Kamati haitajihusisha na shughuli ya kuimarisha chama chochote cha siasa.
- Kamati haitojihusisha na jambo lolote ambalo linakwaza imani ya dini yoyote.
- Kamati haitakuwa na mamlaka ya kuingilia kwa namna yoyote ile mambo yanayomhusu mwanachama wa IRCPT binafsi.
- Kamati itajihusisha na kazi au wajibu wake kama ilivyoelezwa katika mwongozo huu.
- Kamati itajihusisha na masuala yanayochochea amani na yale yenye maslahi kwa jamii
- Kamati itafanya kazi kwa kuheshimu utu na katu haitojihusisha na jambo lolote linalochochea ubaguzi wa aina yoyote katika jamii.
- Kamati itahakikisha maamuzi yake hayafanywi na dini moja tu bali yanahakikisha ushiriki wa kila mmoja kadri inavyowezekana.

KIAMBATANISHO CHA 3: Mifano ya Mikataba ya Kijamii

Unaposoma mifano hii ya mikataba ya kijamii, tafadhali zingatia kwamba mikataba ya kijamii inaandaliwa na kukubaliwa na wanajamii wenyewe; mikataba hii ya muundo wa kujiamulia na kuimiliki ni sehemu ya umadhubuti wa ahadi. Hii pia inaeleza ni kwa nini mikataba yote haina muundo unaofanana ingawa yote inaandaliwa kwa lengo moja. Kwa hiyo, mitazamo na maoni yanayoelezwa katika mifano hii ni ile ya jamii na isitafsiriwe kuwa ni maoni ya ACORD.

Mfano wa 1: Mkataba wa Kuishi Pamoja kwa Amani (Mtaa wa Teza II, Kamenge), Burundi.

Sisi, wakazi wa Kamenge, Mtaa wa Teza II, Wahutu na Watutsi, watu waliokimbia makwao, waliorejea na jamii ya wenyeji wanaoishi katika mtaa huu:

- Kwa kuzingatia kwamba Burundi imekuwa kwenye vita kwa zaidi ya miaka kumi
- Wakati vita imeharibu sana Kamenge, ambapo Watutsi walifukuzwa kutoka kwenye makazi yao, na baadaye Wahutu walifukuzwa kutoka kwenye makazi yao, ambapo jamii zimekuwa waathirika wa uporaji, mauaji, ubakaji na aina nyingine za uhalifu wa kivita;

Tunathibitisha kwamba:

- Kwa pamoja maisha yetu hapa katika Mtaa wa Teza II yameharibiwa na watu wa nje, wawe wanasiasa, wanajeshi au wahalifu.
- Wakati wa vita, Watutsi walikimbia makazi yao na kuwa wakimbizi, wakikimbia kwa kuhofia maisha yao.
- Vilevile Wahutu walifukuzwa na kuteswa kwa kiasi kiubwa kiasi kwamba wengine wamejikuta pamoja na Watutsi katika kambi za hifadhi za waliokimbia makwao au kwingineko.

Kama msemo wa Kirundi usemavyo: “*Nta mwonga ubura isato iba idahizwe*” (*hakuna damu pasipo na mwiba*), wakosaji miongoni mwa vijana walitenda uhalifu dhidi ya wale waliokuwa wa

makabila mengine, wamewatesa, wameiba mali zao na hata kuwaua.

Sisi Wahutu tunathibitisha kwamba:

- Sisi, ambao tayari tumerudi nyumbani, tunatumaini kwamba majirani zetu nao watarudi nyumbani ili tuishi tena pamoja;
- Tunajiandaa kuwapokea kwa moyo mkunjufu kabisa. Ni lazima warudi katika ardhi waliyoimiliki hapo kabla;
- Tutawasaidia kujenga upya nyumba zao, na wao pia watusaidia kujenga zetu;
- Tutapambana pamoja dhidi ya wahalifu au maadui wanaotaka kuharibu mtaa wetu.

Sisi Watutsi tunathibitisha kwamba:

- Tunafurahi kuwaona majirani zetu tena. Sisi sote tunataka kurudi kwenye nyumba zetu tena na kuungana na majirani zetu waliokwisharejea tayari. Tunajua kwamba kwa sehemu kubwa yale yaliyotokea katika nchi yetu ni matokeo ya siasa mbaya za nchi, ambazo zinatumiya ujinga wa watu wachache, ambazo ziliturubuni na kusababisha maelfu ya vifo.
- Hata kama baadhi yetu bado wana woga, tunatamani sana kama kungalikuwa na mikutano mingi na kutembelewa zaidi ili kurejesha imani kati yetu.

Sisi sote, Wahutu na Watutsi, tukitambua kwamba kuna uhalifu wa hali ya juu sana uliofanywa na watu wa hapa mtaani kwetu, kuanzia sasa tunajizua kunyoosheana vidole vya lawama ili kuepuka hatari ya kurudi katika mgogoro.

Hata hivyo, ni matumaini yetu kwamba wale wenye hatia wataomba msamaha na msamaha tayari umekwishatolewa.

Hata hivyo, kama kuna sababu za mtu kumkosoa jirani yake, mtu anaweza kutumia kamati iliyochaguliwa hapa ili kusaidia kutatua suala hilo.

Sisi Wahutu na Watutsi, tunakubaliana mambo yafuatayo:

- Hakuna Mhutu atakayemwua au kumtesa Mtutsi kwa sababu ya kabila, siasa au nyingineyo.
- Hakuna Mtutsi atakayemtesa au kumwua Mhutu kwa sababu za kabila, siasa au nyingineyo.
- Daima tutabaki tumeungana ili kuhimili mikikimikiki yoyote ya kisiasa au mingineyo.

Tunaweka nia ya dhati kutekeleza yafuatayo:

- Kuishi pamoja kwa amani;
- Kusameheana kwa dhati;
- Kuanza upya maisha pasipo kutoaminiana, hila, na chuki;
- Kuunda umoja wa viongozi huku tukiungana mkono;
- Kubomoa ujumbe wote wenye uharibifu, uwe wa kisiasa au mwingineo;
- Tutasaidiana kujenga upya nyumba zilizoharibiwa;
- Kuishi kwa pamoja kwa amani pasipo ukiukwaji wa haki; na
- Kurejesha imani miongoni mwetu kwa sisi kushiriki mikutano au kutembeleana.

Ili kuhakikisha kuwa nia yetu hii inadumu, tumechagua kamati, ambayo itakuwa na wajibu wa kuisimamia. Kamati hi inaundwa na watu sita:

1. **Wawakilishi wawili wa vijana:** 1 akiishi katika mtaa wetu; mwingine aliyekimbia makazi
2. **Wawakilishi wawili wa wanaume:** 1 akiishi mtaani; mwingine aliyekimbia makazi;
3. **Wawakilishi wawili wa wanawake:** 1 akiishi mtaani; mwingine aliyekimbia makazi.

Kwa niaba ya wakazi wa Teza II, Kamati iliyochaguliwa:

Mwakilishi wa vijana anayeishi Kamenge:

[Jina& Saini]

Mwakilishi wa vijana aliyekimbia makazi:

[Jina& Saini]

Mwakilishi wa wanaume anayeishi Kamenge:

[Jina& Saini]

Mwakilishi wa wanaume aliyekimbia makazi:

[Jina& Saini]

Mwakilishi wa wanawake anayeishi Kamenge:

[Jina& Saini]

Mwakilishi wa wanawake aliyekimbia makazi:

[Jina& Saini]

Tunatoa wito kwa ACORD, CADEKA na wahisani wengine kutusaidia katika yafuatayo:

1. Kudumisha mikutano na kazi nyingine za pamoja ili kuimarisha kuaminiana kwetu.
2. Kujenga upya na hasa kutusaidia mabati.
3. Kuandaa mikutano ya vijana ili waweze kufikia ahadi hizi kwa sababu wao ndiyo kundi linaloweza kurubuniwa kwa urahisi.

Ahadi hizi zimepitishwa na watu 150 wanaoishi katika Mtaa wa Teza II, wakiwakilisha makundi ya jumuiya nzima.

Yametiwa saina katika Mtaa wa Teza II, katika makazi ya Askofu Dacillia Joseph, anayejulikana pia kama Buyengero, mnamo tarehe 30/06/04.

Mfano wa 2: Mkataba wa Kijamii kati ya Jamii za Wakisii na Wakipsigis Wanaoishi katika mpaka wa Wilaya za Sotiki na Borabu, Kenya

Utangulizi

Mpaka wa Sotiki na Borabu umekuwa na sifa ya mapigano ya mara kwa mara kati ya jamii hizi mbili, Wakisii na Wakipsigis kwa sababu ya matukio ya wizi wa ng'ombe unaofanywa na magenge ya wahalifu. Ingawa hutokea mara nyingi, matukio haya yalishughulikiwa vizuri na jumuiya zote mbili wakisaidiwa na Kitengo cha Kuzuia Wizi wa Mifugo katika maeneo tofauti.

Hata hivyo, machafuko ya baada ya uchaguzi, tatizo la ukosefu wa usalama katika mpaka lilikuwa kubwa. Sisi, wanajumuia, tulipambana wenyewe kwa wenyewe na kutenda maovu kama vile: kuchoma nyumba moto, kuuana, kuporana mali, kubaka wasichana na wanawake, na chuki ya kikabila iliongezeka sana.

Kupitia mikutano ya amani iliyowezeshwa na Wakala wa Ushirikiano na Utafiti wa Maendeleo (ACORD) na Chama cha Wakulima wa Nafaka (CGA), tumepata fursa ya kuwa na mazungumzo na kutafakari masuala yanayoathiri jamii zetu mbili. Tumetia saina makubaliano yafuatayo kama masuala makubwa yanayochangia katika mgogoro kati ya jamii zetu mbili:

VIGEZO VIKUU VINAVYOSABABISHA MATATIZO HAYA

- i. Wizi wa kila mara wa ng'ombe;
- ii. Ukabila;
- iii. Siasa mbaya/propaganda/taarifa potofu;
- iv. Migogoro ya kihistoria ya ardhi;
- v. Umaskini/Kukosa ajira/Uvivu/Matumizi ya dawa za kulevyu/Ulevi

MAAZIMIO

Sisi Wakisii na Wakipsigis tunaoishi katika mpaka kati ya Wilaya za Sotiki na Borabu ambao tumehangaishwa sana na madhara ya migogoro kati yetu, tunaweka nia ya dhati ya kuishi pamoja kwa amani pasipo kuingia katika machafuko na tumekubaliana zaidi juu ya masuluhisho yafuatayo kwa matatizo yetu haya ambayo yatachangia katika kuishi kwa pamoja kwa amani. Kwa hiyo, tumeazimia kukomesha matatizo haya yafuatayo:

Matukio ya kila mara ya Wizi wa Mifugo

Kuhusiana na hili la wizi wa mifugo, tuta:

1. Shirikiana na kufanya kazi pamoja ili kufuatilia ng'ombe walioibwa kupitia kamati ya pamoja ya ulinzi na ulinzi jamii;
2. Kuweka mapatano na Kitengo cha Kudhibiti Wizi wa Mifugo na uongozi wa mkoa pale inapotokea wizi wa mifugo badala ya kujichukulia sheria mikononi;

3. Kutoa taarifa ya wizi wowote wa mifugo kupitia kwa Chifu Mkubwa;
4. Kuhakikisha usalama na kinga ya wale wanaotoa taarifa za watuhumiwa wa wizi wa mifugo.

Ukabila

- i. Kuhusu hili la ukabila, tumekubaliana:
- ii. Kuvumiliana;
- iii. Kuhimiza uchangamani huru kati ya jamii zetu mbili kupitia shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi; na
- iv. Kuwafundisha watoto wetu uzalendo na kuheshimu watu wa makabila mengine.

Siasa Mbovu

Kuhusu hili la siasa mbovu, tumekubaliana kuwa:

- i. Tutawaalika Tume ya Uchaguzi ya Kenya na wawezeshaji wengine ili kutoa elimu yauraiia katika jamii yetu;
- ii. Kuwahimiza wanajamii wetu kuwashirikisha vijana katika shughuli zote za kijamii kama vile michezo (soka), michezo mingine na hatimaye shughuli za kiuchumi;
- iii. Kujizuia kushiriki siasa na propaganda zinazogawa watu;
- iv. Kuthibitisha uhalisia na kutafuta taarifa kutoka kwa mamlaka zinazohusika kabla ya kufanyia kazi taarifa hiyo; na
- v. Kujifunza na kuitumia stadi ya kumudu hasira.

Migogoro ya Ardhi ya Kihistoria

Tunatambua kwamba masuala hayo hapo juu ni magumu, yanabeba tatizo la kitaifa na ni kiini cha Ajenda 4 (masuala na masuluhisho ya muda mrefu) za Mazungumzo ya Taifa na Mapatano kuhusu suluhu ya mgogoro wa kisiasa na vyanzo vyake.

Kwa hiyo, tutaheshimu mipaka iliyopo na mali za watu ndani ya mipaka hiyo;

- i. Tunatambua unyeti wa masuala ya ardhi na yenye kuunganishwa na urithi katika ngazi ya familia.

- ii. Tutatoa wito kwa watu wazima pamoja na watoto wao wa kiume na wa kike kutafuta suluhu kwa njia mazungumzo.

Umaskini/Ukosefu wa Ajira/Uvivu

Tunatambua kuwa idadi kubwa ya vijana hawana kipato, bila kuwa na kazi wala ardhi ya kulima. Kwa hiyo ni rahisi kwao kuvutwa katika tabia zisizofaa kama matumizi mabaya ya pombe, dawa za kulevya, uhalifu na shughuli kama vile wizi wa ng'ombe, wizi, ubakaji, n.k.

Tutaanzisha vyama vya wanafunzi ambavyo vitasimamia mapatano kati ya Wizara ya Vijana na kuwashughulisha katika kazi zenye tija kama vile shughuli za kuingiza kipato karibu na mipaka yetu. Tunaamini kwamba fursa za kiuchumi zitasaidia kuimarisha vijana ili washiriki katika mambo yasiyofaa.

HITIMISHO

Ili kusimamia utekelezaji wa mkataba wa kijamii, Kamati ya Uangalizi wa Jamii yenye wawakilishi 6 kutoka katika kila eneo imekwishaanzishwa:

wanaume 2, wanawake 2 na vijana 2.

Kamati itatekeleza majukumu yafuatayo:

- i. Kuendesha vikao vya kila mwezi ili kutathmini hali;
- ii. Kufanya mazungumzo na viongozi wa Jimbo/ Mkoa kuhusu masuala yanayotishia amani ya jamii;
- iii. Kusimamia utekelezaji wa mkataba wa kijamii uliotiwa saina;
- iv. Kusambaza mkataba uliotiwa saina miongoni mwa jamii za jirani;
- v. Kushiriki kaitka kutafuta mwafaka wa migogoro katika jamii;
- vi. Kuendesha vipindi vya ujenzi wa amani ya jamii na kuimarishwa kwake;
- vii. Kuwasilisha ripoti kwa ACORD na CGA.

Kwa niaba ya watu wa Kamukunji/Gelegele, Riontony/Tembwo na Memisi/Cheplelwa, viongozi wawili wa jamii watatia saina mkataba wa kijamii wakishuhudiwa na wawakilishi kutoka katika kamati ya uangalizi wa jamii.

VIONGOZI WA JAMII: MEMISI/CHEPLELWAL

Majina	Mahali	Saini
1) [Jina]		
2) [Jina]		

WAJUMBE WA KAMATI YA UANGALIZI YA JAMII

Majina	Mahali	Saini
1) [Jina]		
2) [Jina]		
3) [Jina]		
4) [Jina]		
5) [Jina]		
6) [Jina]		

Imetiwa saina mnamo tarehe 21 Novemba, 2008, Borderline Academy, katika mpaka kati ya Wilaya za Sotik na Borabu, Kenya.

Mfano wa 3: Makubaliano ya Amani ya Mabanga (MPA) yakihusisha Bukusu, Teso na Saboat katika Kaunti za Bungoma na Trans-Nzoia nchini Kenya.

KIAMBATISHO CHA 4: Zana ya Uchambuzi wa Mamlaka

Wakati wa kupitia vipengele vya uchambuzi wa mamlaka, itaonekana wazi kwamba inaunda sehemu yenye nasaba ya karibu sana na Uchambuzi wa Utengaji/Ubaguzi wa Kijamii. Tafsiri na njia zilizo nyingi zinazofafanuliwa hapa chini zitawasaidia watendaji na wawezeshaji kuongoza jamii zinazonufaika kuhusu namna ya kufanya Uchambuzi wa Ubaguzi wa Kijamii kama sehemu ya uchambuzi wa tatizo lao.

1. Muundo wa Uchambuzi wa Zana za Mamlaka¹⁶

Uchambuzi wa mamlaka ni muhimu katika kuelewa muktadha ambamo tunataka kuleta tofauti; kwa mantiki hii, ni muhimu kushikilia njia za kutumia haki. Mamlaka—inafasiriwa hapa kama uwezo wa kutenda kazi pamoja au kila mmoja kivyake, kwa kutumia ushawishi wa ndani, kwa kutumia au kutotumia msaada wa nje—hii ni sehemu yenye nasaba ya karibu katika kila uhusiano na inaweza kuwa na madhara chanya au hasi, inategemeana na hali ya mambo ilivyo kati ya wadau. Uchambuzi wa mamlaka wa kiusiano unatoa ung'amuzi kuhusu mambo yaliyopo na taathira zake.

Mashirika mengi hutambua aina tatu tofauti za miundo ya mamlaka lakini zinazokamilishana ambazo zinaweza kusaidia kuchambua mienendo ya mamlaka, yaani:

- i. Sura mbadala za mamlaka (aina za mamlaka)
- ii. Sura za mamlaka, na
- iii. Muundo wa mamlaka

Ni juu ya wawezeshaji kupima ni muundo-mbinu upi wa uchambuzi wa mamlaka unafaa katika muktadha ambamo kwamo wanafanya kazi, na aina ya taarifa wanazotaka kukusanya.

i. Sura mbalimbali za Mamlaka

Muundo wa sura mbalimbali za mamlaka unatoa mwonekano wa mamlaka kama nguvu chanya kwa ajili ya mabadiliko na haiitazami nguvu kama rasilimali yenye kikomo. Inapendekeza njia tatu tofauti za kuyatazama mamlaka kama kitu ambacho watu wanatumia katika kuhusiana wao kwa wao:

Aina za mamlaka/	Sifa
Mamlaka pamoja na	Kutafuta eneo la pamoja linalounganisha maslahi tofauti na kujenga nguvu ya pamoja. Nguvu ya utendaji wa pamoja.
Mamlaka kwa	Nguvu ya pekee ya kila mwanamke au msichana ya kujitengeneza maisha na ulimwengu wake. Hii inatokana na imani ya msingi kwamba kila mtu ana nguvu ya kuleta tofauti duniani.
Mamlaka ndani ya	Mtu mmojammoja au pamoja na wengine kujithamini, kujitambua na kuwa na utu. Hii inajumuisha uwezo wa kutambua tofauti za mtu mmojammoja na wakati huohuo kuheshimu wengine.
Mamlaka juu ya	Mamlaka chanya au hasi inayotumiwa dhidi ya wengine (wanaume, wanawake, wavulana, wasichana, makundi, n.k.)

¹⁶ Sehemu hii imechukuliwa kutoka: Guijt, I, Seeboldt, S, *Power relations in context: the power of understanding power*, http://www.capacity.org/en/journal/tools_and_methods/the_power_of_understanding_power.

Muundo huu ni muhimu katika kubaini maeneo dhaifu katika makundi, uhusiano, asasi na mtu mmojammoja—na kujua namna ya kuweka mikakati kwa kuwatumia. Wakala inaweza kuweka mkazo kwenye kuimarisha kujiamini kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI (“Nguvu ya ndani”) kama sehemu ya mchakato mkubwa zaidi wa wao kutoa changamoto dhidi ya unyanyapaa na ubaguzi.

ii. Sura tatu za mamlaka

Sura hizi tatu za mamlaka zinaunda moja ya wigo wa mamlaka iliyoelezwa hapa chini. Wazo la “sura” liliibuka kutoka katika midahalo juu ya namna ya kidemokrasia “demokrasia” kwa hakika inavyofanyiwa ghiliba nyuma ya pazia, na matumizi ya vikwazo na itikadi kwa kujua au kutojua ambavyo huwakatisha tamaa watu ili wasishiriki michakato inayomilikiwa na kundi la wachache. “Sura za mamlaka” zinasaidia kuona nini kingine kinatokea ndani ya uhusiano fulani au mwingiliano ambao unaamua matokeo. Kwa mfano, agizo rasmi la serikali linaweza kuipa mamlaka tume ya uchaguzi kuchunguza ufiisadi wakati wa uchaguzi wa hivi karibuni, hata hivyo, endapo kamati hatimaye inapewa muda kidogo sana kufanya uchunguzi wao na kuandaa maoni basi “mamlaka yaliyojificha” yanatumiwa kuwafanya washindwe kuathiri uamuzi.

Sura tatu hizi ni:

Sura za mamlaka	Tabia
Mamlaka inayoonekana	Utoaji uamuzi rasmi na unaoonekana, siasa za vyama vingi ambayo ina “mamlaka juu ya” yanayoonekana.
Mamlaka iliyojificha	Kutengeneza ajenda nyuma ya pazia, kuhamasisha chuki na maslahi, kubagua watu na mada kutoka katika mjadala.
Mamlaka isiyoonekana	Uambukizaji kijamii, kiitikadi na kuongoza maoni ya umma na mahitaji yao; mara nyingi yanaingizwa ndani ya nafsi (inahusiana na “mamlaka ya ndani”).

iii. Muundo wa Mamlaka

Muundo wa mamlaka, ulioandaliwa na John Gaventa wa Taasisi ya Mafunzo ya Maendeleo huko Sussex (Uingereza), ina wigo wa aina tatu, yaani:

- i. Nafasi
- ii. Mahali, na
- iii. Sura (zilizotajwa hapo juu)

Muundo wa mamlaka unaonyesha njia ya kutathmini hatua ya kushiriki katika maendeleo na mabadiliko katika uhusiano wa kimamlaka na na/au kwa niaba ya watu maskini na wanaotengwa. Inafanya hivyo kwa kutofautisha hatua za ushiriki kama ifuatavyo:

Wigo wa Mamlaka	Tabia
Mahali	Katika ngazi tatu (au “mahali”): ya ulimwengu mzima, kitaifa na ngazi ya jamii ambayo huenda itatumika.)
Nafasi	Katika aina tatu za “nafasi” ya (kisiasa). Iliyofungwa, kualikwa na kuundwa (au nyingine ambazo zinaweza kufaa.)
Sura	Miongoni mwa “sura tatu za mamlaka” zilizopo ndani ya ngazi na nafasi: mamlaka inayoonekana na ile isiyoonekana.

Wazo la “nafasi” ni muhimu. Kwa mujibu wa Gaventa, hizi ni “fursa, nyakati na njia ambamo raia wanaweza kuchukua hatua kiasi cha kuweza kuleta mabadiliko katika sera, mijadala, uamuzi na uhusiano unaoathiri maisha na maslahi yao”. Muundounatazama mamlaka kwa kuyahusianisha na namna nafasi za kushirikiana zinavyotengenezwa, ngazi za mamlaka (kutoka jamii hadi ulimwenguni), na pia aina tofauti za mamlaka zilizoenea kote.

Kwa kutazama hatua zinazochukuliwa na raia kupitia mtazamo huu, kwa mfano, kunawezesha tathmini ya kimkakati ya uwezekano wa hatua inayoleta mabadiliko kwa raia, na namna ya kuifanya iwe na matokeo bora.

Uchambuzi wa mamlaka si tu kukagua orodha ya kuangalizia. Dhana zinaweza kusaidia watendaji kuelewa njia mbalimbali ambazo mamlaka zipo na zinavyofanya kazi. Inahitaji ukuzaji wa mtazamo ambao unamsababisha mtu kuuliza maswali machache, kuwasikiliza watu na kuchambua hali halisi kwa njia tofauti.

2. Mwonekano wa Jedwali maalumu kwa wanawake (mfano)

Hapa chini kuna mfano wa namna jedwali la Mwonekano na Sura za mamlaka zinavyoweza kutumika kuchambua hali fulani halisi ambazo kundi dogo katika jamii linakabiliana nazo. Jedwali hili linakazia upande wa wanawake pamoja na uhusiano wa jinsia, lakini hii inaweza kuchukuliwa kwa matumizi ya kuchambua muktadha wa kundi lingine.

Aina za Mamlaka	Maana	Mikakati
Mamlaka pamoja na	Kutafuta msimamo wa pamoja miongoni mwa maslahi tofauti na kujenga nguvu ya pamoja. Mamlaka kutokana na wingi.	Kuunga mkono uanzishwaji na uimarishwaji wa asasi na mavuguvugu ya wanawake. Unga mkono mshikamano kati ya mavuguvugu ya wanawake na yale ya wapigania haki wengine. Toa changamoto kwa uhusiano wa mamlaka na unga mkono ajenda za kuimarisha uongozi wa wanawake.
Mamlaka	Kipawa cha kipekee cha kila mwanamke au msichna kujitengezea maisha yake na yale ya ulimwengu. Hii ina msingi wake katika imani ya msingi kwamba kila mtu ana mamlaka ya kuleta tofauti duniani.	Kujenga mamlaka ya wanawake kutoa uamuzi na kufanya uchaguzi. Unga mkono utetezi wa elimu ya wasichana. Imarisha uwezesaji wanawake kiuchumi na kupitia programu za kiuchumi.
Mamlaka kutokea ndani	Yaani, kujenga uwezo wa wanawake kujitambua na kujijua, hii inajumuisha uwezo wa kutambua tofauti za watu na kuheshimu kila mmoja.	Hamasisha na wezesha programu kuhusu kujenga kujiamini, kujitambua na kujithamini. Jenga uelewa wa haki na uwakala binafsi.
Mamlaka kwa	Kipawa cha pekee cha kila mwanamke au msichana kutengeneza maisha yake na ya ulimwengu. Hii inatokana na imani yetu ya msingi kwamba kila mtu ana mamlaka ya kuleta tofauti ulimwenguni.	Kujenga uwezo wa wanawake wa kutoa uamuzi na kufanya uchaguzi. Unga mkono na tetea elimu ya wasichana. Imarisha programu za uwezesaji wanawake kiuchumi na kisiasa.
Mamlaka kutokea ndani	Yaani, kujenga uelewa wa wanawake na wasichana wa kujithamini na kujitambua; hii inajumuisha kutambua tofauti kati ya mtu na mtu na kuheshimu wengine.	Hamasisha na wezesha programu za kujenga kujiamini, kujitambua na kujithamini. Kujenga uelewa wa haki na uwakala binafsi.
Mamlaka juu ya	Namna mamlaka yanavyotumika inamaanisha kwamba wanawake na wasichana wana mamlaka kidogo sana juu ya mambo mengi yanayohusu maisha yao na nafasi katika jamii. Pia ina maana kwamba wanaume, wavulana na taasisi mara nyingi wanatumia MAMLAKA HASI JUU yao.	Kukuza uelewa miongoni mwa jinsi. Kukuza kujitambua miongoni mwa wasichana na wanawake. Kusisitiza thamani chanya na kutumia mamlaka katika utawala na uongozi.

Sura za Mamlaka:

Sura	Maana
Inayoonekana waziwazi	Utoaji uamuzi unaoonekana. Hii ina maana ya kanuni, sheria, mifumo, mamlaka, taasisi na hatua rasmi za utoaji uamuzi. Mageuzi mengi ya serikali na mikakati ya utetezi hushughulika na mamlaka haya yanayoonekana, yanayoweza kufafanuliwa kwa kushughulika na upendeleo, michakato iliyofungwa na sheria za kibaguzi za taasisi.
Iliyojificha	Kuandaa Ajenda ya Kisiasa Mamlaka yaliyojificha hayafanyi kazi waziwazi na kwa hiyo, ni vigumu kushughulika nayo. Kutokana na maslahi yanayolengwa, huwa na kawaida ya kufanya kazi nyuma ya pazia ili kudumisha ushawishi wao kwa kudhibiti; ambao hufikia meza ya utoaji uamuzi na nini kinaingia katika ajenda ya umma. Misukumo hii hubagua na kuondoa thamani ya wasiwasi na uwakilishi wa makundi yasiyo na nguvu sana, kama yale ya maskini na wanawake.
Isiyoonekana	Mamlaka isiyoonekana ndiyo wigo wa kisiri zaidi kwa sababu huathiri thamani, imani na kujitambua kwa mwanamke. Ushirikiano wa kijamii, utamaduni na itikadi huendeleza ubaguzi na kukosekana kwa usawa kwa kufafanua nini ni "kawada", au kinachokubalika. Aina hii ya mamlaka ndiyo ambayo mara nyingi huwafanya wanawake na wasichana kujiona wao ndio wa kulaumiwa kwa matatizo na huwazuia kudai haki zao.

KIAMBATISHOCHA 5: Uchambuzi wa Jinsia

1. Vipengele vya Hali ya Mgogoro na Wigo Unaowezekana wa Jinsia¹⁷

Vipengele vya Hali ya Mgogoro	Wigo Unaowezekana wa Kijinsia
Hali kabla ya mgogoro	
Kuongezeka kwa vikosi vya askari mitaani.	Kuongezeka kwa biashara ya ngono (ikiwemo ngono na watoto) karibu na kambi za jeshi.
Propaganda za utafa, ukabila au aina nyingineyo inayotumiwa kuunga mkono harakati za kijeshi.	Fikra potofu kuhusu jinsia na ufafanuzi wa aina fulani wa hali ya kiume na kike mara nyingi hupigiwa chapuo. Huenda kukawa na ongezeko la msukumo kwa wanaume na wavulana la “kutetea taifa/kabila”.
Kujikusanya kwa wanaharakati wa amani na taasisi zao.	Wanawake wamekuwa mstari wa mbele katika vuguvugu la amani – kwa ujumla wake na kupitia asasi maalumu za wanawake. Mara nyingi wanawake wamepata ridhaa kutokana na wajibu wao kama akina mama, lakini pia wameweza kujiweka kando na wajibu huo wa kimapokeo nyakati za migogoro, wakichukua wajibu mwingine katika umma katika asasi za misaada na siasa.
Kuongezeka kwa vitendo vya ukiukwaji haki za binadamu	Si mara zote haki za wanawake zinatambuliwa kama haki za binadamu. Vitendo vya ukatili kwa msingi wa jinsia huenda vikaongezeka.
Wakati wa mgogoro	
Maumivu ya kisaikolojia, ukatili wa kimwili, majeruhi na kifo	Wanaume na wavulana huwa askari/wapiganaji wa mwanzo. Hata hivyo, katika migogoro mbalimbali, wanawake pia hufanya idadi kubwa ya wapiganaji. Wanawake na wasichana mara nyingi huwa waathirika wa ukatili wa kingono (ikiwemo ubakaji, uumizaji kingono, udhalilishaji kingono, ukahaba wa kulazimishwa na ulazimishaji mimba) wakati wa mgogoro wa kivita.
Mitandao ya kijamii hutibuliwa na kuharibiwa – mabadiliko katika muundo na uundwaji wa familia	Uhusiano wa kijinsia unaweza kubadilishwa. Mgawanyo wa kimapokeo wa kazi ndani ya familia unaweza kushinikizwa. Mikakati ya kujinusu mara nyingi hulazimisha mabadiliko katika migawanyo ya kazi kwa jinsia. Wanawake wanaweza kuwajibika kwa kuongezeka kwa idadi ya wategemezi.
Ukusanyaji watu wakati wa mgogoro. Mtiririko wa maisha wa kila siku na kazi huvurugwa.	Mgawanyiko wa kazi kwa jinsia katika mahali pa kazi huenda ukabadilika. Kutokana na ukusanywaji wanaume kwa ajili ya kupigana vita, wanawake mara nyingi huishia kuchukua kazi na majukumu ambayo kimapokeo huwa ni ya wanaume. Wanawake wameleta changamoto katika fikra potofu za kimila za jinsia na kuchukua wajibu wa kuwa wapiganaji na kuchukua majukumu mengine yasiyo ya kimapokeo.
Upungufu wa mahitaji (upungufu wa chakula, matunzo ya afya, maji, mafuta, n.k.)	Wajibu wa wanawake kama watafuta riziki za kila siku katika familia kunaweza kumaanisha ongezeko la shinikizo na kazi zaidi kwani mahitaji ya lazima huwa ni vigumu kuyapata. Wasichana pia wanaweza kujikuta wakipata majukumu zaidi. Wanaume wasio wapiganaji hupata shinikizo kwa majukumu yao ya jinsia nyumbani ikwia wanatarajiwa, lakini hawawezi, kutafuta riziki kwa familia zao.

¹⁷ Imechukuliwa katika muundo uliotayarishwa na Woronjuk katika: *Woroniuk B. Gender Equality & Peace-building Operations: An Operational framework*, CIDA, Canada, 2000

Kusababisha wakimbizi na watu wanaokimbia makazi yao	Uwezo wa watu kuitikia katika hali ya dharura inatokana na ikiwa wao ni wanaume au wanawake. Wanawake na wanaume wakimbizi (na pia wavulana na wasichana) mara nyingi wana mahitaji na vipaumbele tofauti.
Mazungumzo na mapatano ya amani	Mara nyingi wanawake wanabaguliwa katika majadiliano yoyote rasmi kwa sababu ya kutoshiriki kwao na kutofikiwa na asasi na taasisi za kutoa uamuzi kabla ya mgogoro.
Wakati wa ujenzi na urekebishaji	
Mapatano ya kisiasa na mipango ya kutekeleza makubaliano ya amani	Ushiriki wa wanaume na wanawake katika mchakato huu kwa kawaida hutofautiana, ambapo wanawake mara nyingi huwa kundi dogo katika mapatano rasmi na utungaji sera.
Vyombo vya habari vinavyotumika kutoa taarifa	Utumiaji vyombo vya habari kwa wanawake huwa hakuna usawa, jambo linaloweza kuashiria kwamba maslahi, mahitaji na mitazamo yao hayawakilishwi na kujadiliwa.
Kutumia wachunguzi, walinda amani wa nje n.k.	Kwa ujumla maofisa hawafundishwi katika masuala ya usawa wa kijinsia (haki za wanawake kama haki za binadamu, jinsi ya kutambua na kushughulika na ukatili kwa msingi wa kijinsia). Wanawake na wasichana wamenyanyaswa na kudhulumiwa kingono na walinda amani.
Kuendeshwa kwa uchaguzi	Wanawake hukabiliwa na vikwazo maalumu katika kupiga kura, wanapogombea katika uchaguzi na katika kuhakikisha masuala ya usawa wa jinsia yanajadiliwa kama masuala ya uchaguzi.

Vipengele vya hali ya mgogoro	Wigo unaowezekana wa jinsia
Uwekezaji wa ndani katika utengenezaji ajira, afya, matunzo n.k.	Programu za ujenzi huenda zisitambue au kutoa kipaumbele katika kuunga mkono mahitaji ya kiafya ya wanawake na wasichana, wajibu wa nyumbani au mahitaji yao ya mafunzo ya stadi na mikopo.
Kuvunjwa kwa vikosi vya wapiganaji	Mara nyingi wapiganaji huchukuliwa kuwa ni wanaume. Ikiwa kipaumbele kitatolewa kwa vijana wanaume, wanawake hawanufaiki katika ugawaji ardhi, mipango ya mikopo n.k.
Hatua za kuongeza uwezo na kujiamini katika jamii ya kiraia	Kwa ujumla hakuna uwiano katika ushiriki wa wanawake katika asasi za kijamii na AZISE. Asasi hizi mara nyingi hukosa uwezo na shauku ya kutoa kipaumbele katika masuala ya jinsia.

2. Vipengele vya Uhusiano wa jinsia na wigo wa migogoro zinazoweza kuwepo

Vipengele vya uhusiano wa jinsia	Ufafanuzi	Zinavyobadilika kutokana na migogoro	Matokeo yake
Wajibu wa jinsia	Shughuli za kila siku za wanawake na wanaume: mgawanyo wa majukumu	Wanawake wanawajibika zaidi katika kutafuta riziki ya familia; kazi ya wanaume ni kidogo.	Wanawake wanajenga kujiamini katika uwezo wao wa kuwajibika wakati wanaume wanajihisi “kupotea” ikiwa uanaume wao unapunguzwa
Ubainisho wa jinsia	Tabia zinazotarajiwa za wanaume na wanawake (“uanaume” na “uanamke”)	Mikakati ya kujinusuru au kujiweka bayana kwa njia mpya za maisha kunaweza kubadili thamani.	Pengo kati ya tabia zinazotarajiwa na uwezo wa kufikia matarajio.
Taasisi za jinsia	Taasisi (kaya, jamii, dola, n.k.) ambazo zinazalisha mitazamo na tabia na ambazo zinatawala rasilimali.	Wanawake wanapata nguvu mpya ya kutoa uamuzi katika kaya ikiwa ni matokeo ya kuongezeka kwa wajibu wa kiuchumi, lakini miundo katika jamii, serikali za mitaa na ngazi ya taifa zinabaki kumilikiwa na wanaume.	Wanawake wana majukumu lakini wana mamlaka iliyodhibitiwa. Ujuzi wao unaweza kuwawezesha kujipangia majukumu na kuanzisha haki zao
Itikadi za jinsia	Mitazamo na amali zinazotokana na utamaduni (zikiwemo zile zilizojionyesha kupitia dini, lugha na vyombo vya habari) na zilizoanzishwa katika kipindi kirefu na kushonwa katika muundo wa jamii, ambavyo vinatoa ushahidi wa wajibu wa jinsia, ubainisho na miundo inayotawala.	Mitazamo na amali hubadilika polepole sana. Katika nyakati nyingine, wanaweza kuwa zaidi vichwa vya habari kuliko na kuegemea zaidi upande wa utawala wenye msimamo mkali unaoelekea katika udhibiti wa wanaume dhidi ya wanawake.	Ubishi wa itikadi za mfumo dume unaweza kusababisha tija inayoletwa na wanawake kuachwa baada ya vita kumalizika. Mara nyingine huenda kutakuwa na “adhabu” dhidi ya uwezeshaji mwanamke, na kusababisha kuongezeka kwa hatari ya kuangamizwa.

¹⁸ Orodha hii ya kuangalizia imetokana na orodha iliyotolewa katika mwongozo wa UNDP kuhusu Njia za Kushughulikia Jinsia katika Hali za Migogoro na Baada ya Migogoro, UNDP Bureau for Crisis Prevention and Recovery (BCPR), New York, 2002.

3. Orodha ya Uchambuzi wa Jinsia¹⁸

Ifuatayo ni orodha ya maswali yanayoweza kuongoza uchambuzi wa ubaguzi/ushirikishwaji wa wanaume na wanawake.

1. Uchambuzi mfupi wa muktadha wa kijamii na kiutamaduni, ukiwemo:

- Wajibu uliopo wa jinsia (nani anafanya nini)
- Nani mwenye mamlaka ya kuamua ndani ya familia, jamii au taasisi?
- Miundo ya kaya za jamii
- Nani ana kauli ya mwisho juu ya rasilimali/mahitaji katika kaya?
- Rasilimali zimegawanyika vipi katika kaya?
- Wajibu wa wanaume na wanawake katika maisha ya kiroho/kiimani
- Taratibu za kimila/kiutamaduni zinazokwamisha haki za wanawake

2. Uchambuzi mfupi wa muktadha wa kisiasa, ikiwemo:

- Kiwango cha ushiriki wa wanawake katika vuguvugu la kisisasa, mamlaka za kijamii, utoaji uamuzi katika ngazi ya jamii.
- Jinsi wanawake wanavyojiandikisha kwa ajili ya upigaji kura na namna ya kushiriki katika kura (ikiwa inafaa).
- Ikiwa wavulana na wasichana wana fursa sawa za kupata elimu.
- Ikiwa wasichana wanakatisha masomo, na kama ni ndiyo, katika ngazi ipi?

3. Uchambuzi mfupi wa muktadha wa kiuchumi, ikiwemo:

- Ni aina gani ya shughuli/wajibu/kazi zinakatazwa kwa wanawake au wanaume kwa mujibu wa mila za jamii?
- Je, nani ndiye mtafuta riziki mkuu katika familia?

- Je, wanaume na wanawake wanashiriki katika sekta rasmi? Kama ndivyo? Wanafanya nini hasa?

4. Bainisha rasilimali za jamii zinazoweza kutumika kupatikana kwa suluhisho la matatizo yanayoikabili jamii:

- Rasilimali watu inayoweza kutegemewa na jamii
- Rasilimali uchumi zilizopo (Nani anazimiliki? Kuna kiasi gani kilichopo?)
- Miundombinu iliyopo hapo (upande gani; hali; nani anawajibika kuitunza?)
- Mitandao ya usaidizi iliyopo, kama vile familia, vikundi vya kidini, vyama, kamati, n.k.
- Wanaume na wanawake wanaoweza kushirikiana katika kutoa ulinzi kwa makundi yaliyo hatarini zaidi,
- Wanaume na wanawake wanaoweza kuchangia katika kuleta mabadiliko/mapatano ya amani,
- Rasilimali za jamii ambazo zingeweza kuwepo baada ya mafunzo/kujenga uwezo/kuendeleza ujuzi (kubaini vipawa).
- Je, wanawake tayari wameelemewa na kazi (kwa mfano, majukumu ya nyumbani na/au kazi nyingine?).
- Kigezo cha muda/ugawaji muda kwa matumizi ya rasilimali watu (hasa kwa wanawake ambao wanaweza kuhusishwa katika shughuli mbalimbali).

5. Kuhakikisha kwamba mahitaji mbalimbali ya watu yanabainishwa na kuzingatiwa:

- Kubaini na kuweka kipaumbele cha mahitaji ya msingi kwa wanaume na wanawake. (Mgogoro unaweza kuwafanya wanawake, watoto au wazee wakae ndani tofauti na ilivyo kawaida. Jitihada za pekee zinahitajika ili kuwasiliana nao na kujua mahitaji yao).

¹⁸ Parker, Rani, "Another Point of View: A Manual on Gender Analysis Training for Grassroots Workers" UNIFEM.

- Kupanga taratibu za usafi kadiri ya idadi ya watu.
- Tayarisha matukio ya kukusanya fedha kwa lengo la kusaidia makundi yaliyo hatarini zaidi.
- Pale inapofaa, weka visanduku vya Huduma ya Kwanza kulingana na muktadha na mahitaji ya watu wanaolengwa.
- Andaa misaada ya kisaikolojia na ipatikane kwa jamii nzima.
- Katika shughuli hizo, tumia njia mbalimbali kwa mujibu wa jinsi na umri wa watumiaji wa mwisho.
- Andaa miundombinu ya matibabu inayofikika kwa wote katika jamii.
- Kwa upande wa watu waliokimbia makazi yao, wahusishe wanaume na wanawake katika taasisi na usimamizi wa makazi/kambi ya muda.
- Andaa shughuli mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya kijamii, kisaikolojia na kiutamaduni.
- Walinde wanawake na wanaume dhidi ya ukatili (kwa mfano, wanawake: ukatili wa kingono; wanaume: kulazimishwa kuingia katika vikosi vya upiganaji).

- Wasaidie wanajamii kurejea kadri inavyowezekana katika maisha ya kawaida ya kila siku (huku ukiepuka kusisitiza au kuendelezwa kwa mitazamo potofu ya kimila na kijinsia).

4. Jedwali la Uchambuzi wa Jinsia

Jedwali la Uchambuzi wa Jinsia ni zana ya uchambuzi ambayo inatumia njia shirikishi kuwezesha ufafanuzi na uchambuzi wa masuala ya jinsia katika jamii zinazoathiriwa nayo. Kutumia Jedwali la Uchambuzi wa Jinsia kutatoa maelezo fasaha ya pekee ya masuala yanayoandaa uwezo wa uchambuzi wa jinsia kuanzia ngazi za chini kwenda juu.

Jedwali la Uchambuzi wa Jinsia limejikita katika kanuni zifuatazo:

- Maarifa yote yanayohitajika kwa uchambuzi wa jinsia yapo miongoni mwa watu ambao maisha yao ndio kiini cha uchambuzi.
- Uchambuzi wa jinsia hauhitaji ujuzi wa kiufundi kwa wale walio nje ya jamii inayochambuliwa, isipokuwa wawezeshaji.
- Uchambuzi wa jinsia hauwezi kuleta mabadiliko hadi uchambuzi ufanyike pamoja na watu wanaochambuliwa.

Makundi ya Uchambuzi					
Kundi la 1 la wadau	Kundi la 1	Kundi la 2	Kundi la 3	Kundi la 4	Kundi la 5
Kundi la 2 la wadau					
Kundi la 3 la wadau					
Kundi la 4 la wadau					

Mifano ya makundi:

Kazi: Hili linazungumzia mabadiliko katika majukumu, kiwango cha ujuzi kinachohitajika (wenye ujuzi dhidi ya wasio na ujuzi, elimu rasmi, mafunzo) na uwezo wa kazi (watu wa ngapi wanajua na wanaweza kufanya kiasi gani;

Je, watu wanahitaji kuajiriwa au wanafamilia tu wanaweza kuifanya?)

Muda: Hili linazungumzia mabadiliko katika kiasi cha muda (saa 3, siku 4, n.k.) unaohitajika ili kutekeleza jukumu linalohusiana na mradi au shughuli fulani.

Rasilimalia Hili linahusu mabadiliko katika kupata mtaji (kipato, ardhi, mkopo) kama matokeo ya mradi, na kiasi ambacho udhibiti wa mabadiliko katika rasilimali upo (kwa kiasi fulani) kwa kila ngazi ya uchambuzi.

Utamaduni: Vigezo ya kiutamaduni vinazungumzia mabadiliko katika mitazamo ya kijamii ya maisha ya washiriki (mabadiliko katika majukumu au hadhi) kama matokeo ya mradi.

Mifano ya makundi ya wadai:

Mtu angeweza kuunda makundi ya watu 10-30 wenye tabia zinazofanana, kwa mfano: wanaume, wanawake, wavulana, wasichana, wazee wanaume, wazee wanawake. (Zingatia: ili kupata uelewa mpana wa misukumo wezeshi ya ingeweza kuongeza makundi kama vile: viongozi wa kidini, askari polisi, mamlaka za jamii, wenye ulemavu, wafanyabiashara, wanawake, wajasiriamali, n.k.)

Bercovitch, J., Kremenyuk V, Zartman, W.I. *The Sage Handbook of Conflict Resolution*, 2009.

Bohm D. What is Dialogue. web. 26th Oct 2015

Community Peace Recovery and Reconciliation Handbook, Agency for Cooperation in Research and Development (ACORD), Kenya, 2011.

Galtung, Johan. 1996: *Peace by Peaceful Means: Peace and Conflict, Development and Civilization*. London: Sage.

Gugel G., *The Iceberg Model for conflict dynamic: [Tübingen Institute for Peace Education](#)*.

Kolb, Deborah M. *The Mediators*. Cambridge, 1983.

Mason S., Rychard S., *Conflict Analysis Tools*, Swiss Agency for Development and Cooperation (SDC), Bern, Switzerland, 2005

Rifaat S., *Conflict Transformation; Dynamics, Skill and Strategies*, Pakistan Institute of Legislative Development and Transparency, 2010.

Romney, P., *The Art of Dialogue*, Washington D.C 2005.

Saunders, H. *A Public Peace Process: Sustained Dialogue to Transform Racial and Ethnic Conflicts*. New York 2001.

UNDP, *Why Dialogue Matters for Conflict Prevention and Peacebuilding*, 2009.

UNDP Practical Guide on Democratic Dialogue, Panama, July 2013.

Robinson, D., *Sustained Dialogue; Proposal for a Programme on Sustained Dialogue in New Zealand*, October 2003.

MRADI WA UWEZESHAJI DEMOCRASIA 2013-2016

Mradi wa Uwezeshaji Demokrasia 2013-2016 unafadhiliwa na mfuko wa pamoja wa nchi za Canada, Denmark, Umoja wa Ulaya, Finland, Ireland, Norway, Sweden, Switzerland, UK na UNDP. Mradi huu unatekelezwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Tanzania



*Empowered lives.
Resilient nations*